**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**IDARA YA KISWAHILI**

# USOMAJI NA UFASIRI SASA WA *UTENZI WA MWANAKUPONA*

NA

**SIMIYU DENNIS MUNYOLE**

**C50/25240/2014**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**JUNI 2017**

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi kama mtahiniwa na haijawahi kamwe kuwasilishwa katika Chuo kingine kwa mahitaji ya shahada.

01/06/2017

**SIMIYU DENNIS MUNYOLE** **TAREHE**

**C50/25240/2O14**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa shahada za juu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

02/06/2017

**Dkt. MASINDE EDWIN** **TAREHE**

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

02/6/2017

**Dkt. TITUS KAUI** **TAREHE**

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

**Tabaruku**

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Samson Barasa na Marciana Simiyu, ndugu zangu Victor Napwora, Edwin Wanjala, Grace Simiyu, Philip Mwanja, Jane Simiyu, Metrine Nato, Andrew Simiyu, Godfrey Simiyu, Marystella Mugeni na mpenzi wangu Judith Dariah Wesonga. Uvumilivu, subira na nguvu mliyonipa ilinipa ari ya kukamilisha kazi hii.

iii

**Shukrani**

Kwanza kabisa, ninatoa shukrani zangu kwa mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuniwezesha kufika kiwango hiki na umbali huu. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Titus Kaui kwa kuchukua muda wao na kujitolea kunijenga na kuniongoza kwa busara na ukakamavu. Nawashukuru kwa maarifa mlionipa na ninawaombea maisha marefu ili mfae wengine.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa mwongozo na ushauri walionipa nilipohitaji msaada wao. Pia ninawashukuru wanafunzi wengine ambao tulianza nao safari ya usomi, Lawi, Maina Macharia, Selly, Penninah, Melvin, Mercy, Jacky, Dan na Ndung'u kwa kunisisimua akili kwa mijadala mingi. Tulifaana kwa mengi kuliabiri jahazi hili la elimu hadi ufuoni. Nawatakia kila la heri.

Hatimaye, ningependa kushukuru familia yangu hasa mama yangu Marciana Simiyu, baba yangu Samson Barasa na mpenzi wangu Judith Wesonga kwa kujitolea kwa hali na mali. Kuwalipa siwezi lakini nawaombea Rabana awatunuku heri na shari awaepushie kabisa. Kwa kanisa langu la marafiki la Kimilili na Kamusinga pamoja na jamii, nawashukuru kunitia moyo na msukumo wenu wa kuthamini masomo. Nawashukuru kwa stahamala zenu, hamtajuta kamwe.

Kwa wengine wote ambao sijaweza kuwataja, nawashehenezea shukrani za dhati kutoka kina cha moyo wangu kwa mchango wenu. Mungu awabariki.

## Ikisiri

Utafiti huu ulichunguza usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona* sasa. Uchunguzi huu uliongozwa na malengo, maswali ya utafiti, pengo la utafiti na mihimili ya nadharia. Malengo ya utafiti huu yalikuwa: kubainisha mazingira chipuzi ya *Utenzi wa Mwana Kupona*, kueleza maudhui yaliyowasilishwa na mtunzi katika *Utenzi wa Mwana Kuponzi* na kueleza usomaji na ufasiri wa utenzi huu kwa kuzingatia aina ya wasomaji mbalimbali katika mazingira ya sasa. Utafiti huu ulitokana na hali kuwa vipindi tofauti vya kihistoria vimepita tangu utunzi wa utenzi huu. Katika vipindi hivi vya kihistoria, kumekuwa na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kutokana na mabadiliko haya ilikuwa ni vyema kuchunguza usomaji na ufasiri wa utenzi huu katika mazingira ya sasa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Nadharia ya Uhistoria Mpya huangalia matini ya jadi katika muktadha wa wakati uliopo. Nadharia hii ilitumika katika kuchunguza nafasi ya mazingira katika usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Aidha nadharia ya Mwitikio wa Msomaji hutathmini upokezi wa wasomaji wa kazi mbalimbali za fasihi. Nadharia hii ilitumika kuchunguza usomaji na ufasiri. Nadharia hizi ndizo zilizouongoza utafiti huu. Muundo wa utafiti ulikuwa wa kisoroveya. Sampuli lengwa katika utafiti huu ilikuwa wasomaji kutoka jimbo la Lamu na Nairobi. Mbinu ya kusudio ilitumika ambapo wasailiwa ishirini (20) kutoka Lamu na wengine ishirini (20) kutoka Nairobi walishughulikiwa na watafiti kupitia mwongozo wa maswali. Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Mbinu kuu ya kukusanya data ilikuwa ni usomaji maktabani na mahojiano nyanjani. Data iliyokusanywa maktabani na nyanjani ilipangwa kulingana na vigezo maalum na uchanganuzi wake kuongozwa na maswali ya utafiti, malengo, pengo la utafiti na mihimili ya nadharia. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Ilibainika kwamba mazingira ya usomaji wa kazi fulani ya fasihi pamoja na tajiriba za msomaji huathiri kwa kiasi kikubwa jinsi anausawiri na kuona ulimwengu. Mtazamo wa msomaji wa kazi fulani ya fasihi humwelekeza jinsi anavyoifasiri kazi mahususi ya fasihi ambayo ameisoma. Aidha ilibainika kuwa ufasiri wa wasomaji mbalimbali wa utenzi huu umebadilika. Kwa hivyo, kadri mazingira na mienendo ya jamii inavyoendelea kubadilika ndivyo usomaji, ufasiri na upokezi wa kazi hiyo unavyobadilika.

## Abstract

This research intended to investigate *Mwana Kupona's Poem* reader response in contemporary context. This research was guided by the objective, statement of the problem, hypothesis questions and tenets of the theories. The research objectives were to discuss the environment and context under which *Mwana Kupona Poem* was authored, to analyze the themes in the poem and finaly to evaluate the reader response of *Mwana Kupona Poem* and interpretation basing on different types of readers in the contemporary context. The general view and belief of a reader of a particular literature work determines how the reader of that work will respond and interpret it. This means that as the context and environment of the reader changes the response and interpretation of the readers of that specific work also changes. The reason behind carrying out this research was to find out how different readers of *Mwana Kupona Poem* respond and interpret it in contemporary context. It was a survey research. The research was guided by the New Historicism theory and Reader Response theory. The research was done in the library and the field. The target sample was readers of *Mwana Kupona Poem* from Lamu and Nairobi County. Twenty (20) readers from each county were interviewed using an interview guide. The readers were identified through purposive sampling method. The data was collected from the library through reading and from the field whereby the targeted sample was interviewed using an interview guide. The collected data was analysed and presented through descriptive method. It was found out that context and environment of any reader of literature work affects his or her interpretation and response.

**Ufafanuzi wa Dhana Muhimu**

**Falsafa-** Itikadi au msimamo wa mtunzi wa kazi ya fasihi kuhusu suala fulani.

**Itikadi-** Imani katika jambo fulani.

**Matini-** Kifungu cha maandishi ya kazi ya fasihi.

**Mazingira-** Jumla ya vitu ambavyo vinamzunguka na kumuathiri mtunzi au msomaji wa kazi ya fasihi.

**Tabaka**- Kundi la watu wenye hali moja linalotokana na jamii yenye mfumo wa uchumi wa kinyonyaji ambao hugawanya watu kulingana na uwezo wao wa kumiliki na kutawala njia za kuzalisha mali.

**Utawa-** Hali ya wanawake kufungiwa nyumbani au kukaa katika mazingira ya nyumbani bila kutoka

## Tafsiri ya Istilahi

**Asilimia**- Percentage

**Asilimia limbikizi-** Cumulative percentage

**Asilimia matukio-** Percentage of cases

**Mtindo Changanuzi wa Tarakimu Sayansi-** Statistical Packages for Social Sciences (SPSS)

**Mwitikio wa Msomaji**- Reader Response

**Uhistoria Mpya-** New Historicism

**Vifupisho**

S.A..W- Sallahu alaihi wasalamu

M1-M10- Nambari abjadi za baadhi ya wahojiwa

YALIYOMO

Ikirari……....................................................................................................................... ii

Tabaruku ........................................................................................................................ iii

Shukrani ......................................................................................................................... iv

Ikisiri v

Abstract .......................................................................................................................... vi

Ufafanuzi wa Dhana Muhimu........................................................................................ vii

Tafsiri ya Istilahi .......................................................................................................... viii

Vifupisho......................................................................................................................... ix

SURA YA KWANZA ...................................................................................................... 1

1.0 Usuli wa Mada .......................................................................................................... 1

1.1 Suala la Utafiti ........................................................................................................... 3

1.2 Maswali ya Utafiti...................................................................................................... 4

1.3 Malengo ya Utafiti ..................................................................................................... 5

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........................................................................................ 5

1.5 Upeo na Mipaka ......................................................................................................... 8

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada..................................................................................... 9

1.6.1 Kuhusu Maudhui na Muktadha ................................................................................ 9

1.6.2 Kuhusu Nadharia na Ufasiri ................................................................................... 12

1.7 Misingi ya Nadharia.................................................................................................. 13

1.7.1 Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji......................................................................... 13

1.7.2 Nadharia ya Uhistoria Mpya ........ 17
1.8 Mbinu za Utafiti ........ 20
1.8.1 Muundo wa Utafiti ........ 20
1.8.2 Mahali pa Utafiti ........ 20
1.8.3 Sampuli Lengwa na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli ........ 21
1.8.4 Ukusanyaji wa Data ........ 22
1.8.4 Uchanganuzi wa Data ........ 23
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo ........ 23
1.9 Kiishilio ........ 23
SURA YA PILI ........ 24
2.0 Mazingira ya Utunzi wa Mwana Kupona na Usomaji Sasa ........ 24
2.1 Utangulizi ........ 24
2.1.1 Mazingira ya Mtunzi ........ 25
2.1.1.0 Historia ya Mwana Kupona Binti Mshamu ........ 28
2.1.1.1 Wazazi wa Mwana Kupona ........ 29
2.1.1.2 Kuzaliwa Kwa Mwana Kupona ........ 30
2.1.1.3 Itikadi na Imani ya Mwanamke Mswahili wa Kiislamu ........ 33
2.2 Mazingira ya Sasa ........ 37
2.3 Kiishilio ........ 43
SURA YA TATU ........ 46
3.0 Maudhui Katika Utenzi wa Mwana Kupona ........ 46

3.1 Utangulizi ........................................ 46
3.2 Maudhui ya Utegemezi ........................................ 49
3.3 Utangamano ........................................ 50
3.4 Mausio ya Mke Bora ........................................ 57
3.5 Dua ........................................ 60
3.6 Mke Aliyetimia ........................................ 62
3.7 Kiishilio ........................................ 64
SURA YA NNE ........................................ 65
4.0 Usomaji na Ufasiri Sasa wa Utenzi wa Mwana Kupona ........................................ 65
4.1 Utangulizi ........................................ 65
4.2 Njia za Usomaji wa Kazi ya Fasihi ........................................ 65
4.3 Maarifa ya Kimsingi na Tajriba ya Msomaji ........................................ 67
4.4 Aina ya Wasomaji wa Utenzi wa Mwana Kupona ........................................ 68
4.4.1 Msomaji wa Kukisiwa ........................................ 68
4.4.2 Msomaji Aliyelengwa ........................................ 70
4.4.3 Msomaji wa Kiwango Bora Zaidi ........................................ 71
4.5 Ufasiri Sasa wa Utenzi wa Mwana Kupona ........................................ 71
4.5.1 Kuhusu Wajibu wa Mke kwa Mumewe ........................................ 71
4.5.2 Kuhusu Mwenendo wa Mwanamke Aliyeolewa ........................................ 75
4.6 Uchanganuzi wa Data Katika Kaunti ya Lamu na Nairobi ........................................ 79
4.6.1 Utangulizi ........................................ 79

4.6.2 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Lamu ........................................................................ 79

4.6.3 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Nairobi........................................................................ 80

4.6.4 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Lamu na Nairobi kwa Ujumla.......................................... 81

4.6.5 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Lamu na Nairobi Kulingana na Jinsia............................ 82

4.6.5.1 Wanawake ................................................................................................................ 82

4.6.5.2 Wanaume.................................................................................................................. 83

4.6 Kiishilio............................................................................................................................... 84

SURA YA TANO .................................................................................................................... 85

Muhtasari, Matokeo na Mapendekezo...................................................................................... 85

5.0 Utangulizi ............................................................................................................................ 85

5.1 Muhtasari ............................................................................................................................ 85

5.2 Matokeo ya Utafiti ............................................................................................................... 87

5.3 Changamoto ........................................................................................................................ 92

5.4 Mapendekezo ....................................................................................................................... 92

Marejeleo ................................................................................................................................ 94

KIAMBATISHO A:.................................................................................................................. 102

Mwongozo wa Maswali Kwa Wasomaji Mbalimbali Kutoka Kaunti ya Lamu na Nairobi wa Utenzi wa Mwana Kupona.......................................................................................................... 102

KIAMBATISHO B .................................................................................................................. 103

Utenzi wa Mwana Kupona ( Nabhany, A. 1972)...................................................................... 103

KIAMBATISHO C .................................................................................................................. 121

Orodha ya Baadhi ya Waliohojiwa ........ 121

KIAMBATISHO D. ........ 123

Picha za Baadhi ya Wahojiwa ........ 123

KIAMBATISHO E. ........ 125

Ramani za Eneo la Utafiti ........ 125

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Usuli wa Mada

Katika usomaji wa kazi za fasihi, msomaji huwa na mawazo na hisi maalum kuhusu matini anayopitia. Hii ina maana kuwa, kila msomaji wa kazi ya fasihi ana uhuru wa kusoma na kufasiri matini au kazi ya fasihi apendavyo.

Murfin (1991) akizieleza fikra za Adena Rasmarini anaifananisha fasihi na kinyago ambacho hakichakamilika. Kinyago hiki ambacho ni kazi ya sanaa hukamilishwa na msomaji ambaye huijaliza kutokana na usomaji wenye makini.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa kazi za fasihi huwa na athari kwa mwandishi. Wanaendelea kufafanua kuwa athari hizi hufasiriwa na wasomaji tofauti kupitia njia mbalimbali. Naye Fish (1980) anaelezea kuwa ni wajibu wa wasomaji kuyafasiri matini husika katika mazingira tofauti. Hii ina maana kuwa ni wajibu wa msomaji kuipa matini husika maana namna anavyoelewa wakati huo maalum.

Usomaji na upokezi wa kazi za fasihi huweza kuathiriwa na matakwa ya kisiasa, kijamii na kibinafsi (Greenblatt1980). Maelezo haya ya Greenblatt yana maana kuwa mazingira huathiri upokezi wa kazi za fasihi. Kwa hivyo, hakuna budi athari hizi kujitokeza katika usomaji na upokezi wa kazi za fasihi.

Katika usomaji, mpokezi wa kazi ya fasihi hana budi kuchunguza upya dhana ya utamaduni. Kauli hii inatokana na maelezo ya Masinde (2003) kuwa: uongozi, mielekeo,

urazini, ujumi, thamani na mienendo ya jamii hubadilikabadilika na njeo kulingana na vile jamii inavyoendelea kiwakati.

Mbatiah (2001) anafafanua usasa kama fasihi inayochunguza maisha ya wakati huu. Anasema kuwa kipindi cha sasa kinaashiriwa na vita vya kwanza (1914-1918) na vya pili (1939-1945). Kwa mujibu wa Mbatiah, vita hizo zilisababisha maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ambayo iliziumba jamii mpya ambazo tunajua leo. Kutokana na haya mabadiliko, watu wengi walihamia mijini na kubuni mitindo mipya ya maisha na hivyo kuzalisha usasa.

Tangu utunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* yakisiwa mwaka wa 1860, karne nyingi zimepita (El-Maawy 2011: 137). Utenzi huu umejitokeza kuwa maarufu sana aghalabu kwa wahakiki wa fasihi na hata Wanasaikolojia wanaporejelea swala la mwanamke katika jamii za Kiafrika (Biersteker 1991). Utenzi huu umeibua hisia mbalimbali kuhusiana na nafasi ya mwanamke katika jamii hasa ya Kiislamu.

Tangu utunzi wa utenzi huu, baadhi ya wahakiki wa kazi za fasihi wamerejelea utenzi huu kama sumu kali ambayo inamdhalalisha Mwanamke na kutompa hadhi anayostahili katika jamii. Wengine kama Werner (1934) akirejelewa na Njozi (1990), walitetea msimamo wa Mwana Kupona na wanaunga mkono ushauri wa Mwana Kupona kwa bintiye.

*Utenzi wa Mwana Kupona* ni utenzi wa kipekee wa zamani ulioandikwa na mwanamke na ukaacha athari kubwa katika maisha ya ndoa Pwani ya Kaskazini. Allen (1971) anasema baada ya utunzi wa utenzi huu, ulisambazwa kwa njia ya masimulizi na athari

yake ikawa kuzidishwa au kupunguzwa jumla ya beti kufuatana na kumbukumbu za moyoni za wapokezi na wasambazaji.

Mtunzi wa kazi za fasihi huwa na uhusiano wa aina mbalimbali na jamii yake (Abdalla, 1978). Abdalla anaendelea kusema kuwa fasihi yoyote ile huupata uhai wake, miongozo na hata maudhui kutokana na hali ya kitamaduni, kiuchumi na kisiasa ya jamii husika iliyochimbuka nayo. Gibbe na Mvungi (1987) nao wanaeleza kuwa fasihi kama asasi nyingine za jamii zilivyo, haina budi kubadilika pindi asasi nyingine inavyobadilika. Hii ina maana kuwa hata wasomaji wa kazi hiyo mahususi ya fasihi wataisoma na kuifasiri kulingana na mabadiliko ya asasi hii

Tangu utunzi wa utenzi huu, miaka imepita, na katika maendeleo haya kumekuwa na vipindi tofauti vya kihistoria. Katika hali hii, usomaji na ufasiri umeathirika kiwakati na kimazingira. Kwa hivyo, kulikuwa na haja ya kuona namna usomaji na ufasiri wake ulivyo sasa kwani kila kipindi maalum cha kihistoria huwa na maarifa yake.

## 1.1 Suala la Utafiti

Katika usomaji wa kazi za fasihi, msomaji huwa na mawazo na hisi maalum kuhusu matini anayopitia. Wasomaji mbalimbali wana uhuru wa kusoma na kufasiri matini au kazi ya fasihi wapendavyo. Hali hii ya uhuru wa ufasiri inaweza kudhibitika kwa kuwabainisha wasomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona* kisha kuwachunguza pamoja na tendo zima la usomaji na ufasiri wa kazi husika (Iser 1974).

Kazi tofauti za fasihi huwa na maana mbalimbali ambazo hupewa na wasomaji baada ya kusoma na kufasiri kazi hizo. Maana hizi huweza kuwa za kijamii, kihistoria au kimazingira. Hata hivyo, wasomaji hufasiri na kuzipa kazi hizi maana yake kutegemea muktadha wa wakati wa utunzi na usomaji kwa kiasi kikubwa. Hii ina maana kuwa, usomaji na ufasiri wa kazi fulani utategemea mabadiliko ya wakati, mienendo na mitazamo katika jamii (Gakuo 2014).

*Utenzi wa Mwana Kupona* ulitungwa katika mazingira maalum ya jamii na ulilenga hadhira mahususi ya wakati wa utunzi wake. Hii ina maana kuwa fasihi hutokana na jamii (Warren na Wallek 1949). Utenzi huu ulitungwa na kuvuma sana mwaka 1858. Utenzi huu umebaki muhimu kwa jamii ya Waswahili (Chacha, 1987).

Tangu utunzi wa utenzi huu, miaka mingi imepita na katika maendeleo haya kumekuwa na vipindi tofauti vya kihistoria. Kila kipindi cha kihistoria huwa na maarifa yake, na haya maarifa huathiri mitazamo na mielekeo ya wanajamii. Jambo hili huathiri usomaji na hata ufasiri wa kazi za kifasihi. Katika hali hii, usomaji, ufasiri na upokezi umeathirika kiwakati na kimazingira. Kwa hivyo, kutokana na haya mabadiliko hasa wakati huu ambao kuna changamoto katika jamii nyingi, kulikuwa na haja ya kutathmini usomaji na ufasiri wa utenzi huu wa Mwana Kupona sasa.

## 1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

a. Je, ni mazingira yapi yaliyochipuza *Utenzi wa Mwana Kupona*?

b. Maudhui yapi yanayojitokeza katika *Utenzi wa Mwana Kupona*?

c. Utenzi huu sasa unasomwa na kufasiriwa vipi na wasomaji wa aina mbalimbali?

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga:

a. Kubainisha mazingira yaliyochipuza na ya usomaji sasa *Utenzi wa Mwana Kupona.*

b. Kueleza maudhui yanayojitokeza katika *Utenzi wa Mwana Kupona.*

c. Kueleza usomaji na ufasiri wa utenzi huu sasa kwa kuzingatia aina ya wasomaji.

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Historia ya ushairi wa Kiswahili ni ndefu. Historia hii inasawirika tangu utunzi wa tenzi mbalimbali kama vile *Utenzi wa Mwana Kupona*. Watunzi wa tenzi hizi waliweza kuyasawiri matukio ya kihistoria na imani yao katika jamii kupitia tenzi hizi. Pia walitumia tenzi hizi kusawiri utamaduni na maisha yao (Momanyi, 1991:6). Kupitia kwa hizi tenzi tunafahamu namna watunzi hawa walivyoweza kupata athari katika mazingira yao. Mazingira haya yamebadilika kiwakati tangu tenzi hizi kutungwa. Jambo hili limeathiri usomaji, ufasiri na upokezi wa kazi husika.

Tenzi hizi zinaweza kueleweka vyema kupitia usomaji na ufasiri wake katika mazingira ya sasa. Jambo la kusikitisha ni kuwa suala hili halijazingatiwa na kupigwa msasa ipasavyo katika zile kazi na tafiti ambazo zimefanywa tayari (Mulokozi na Sengo,

1995:26). Hii ina maana kuwa kuchunguza usomaji na ufasiri wa tenzi hizi kwa kuzingatia mazingira ya sasa kumesaidia uelewa na dhima ya tenzi hizi katika jamii ya sasa.

Utafiti huu ulichunguza usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kuangalia mazingira chipuzi na mazingira ya sasa. Kazi hii ilifanywa kwa madhumuni ya kusaidia uelewa wa mabadiliko katika fasiri ya utenzi huu kutokana na mabadiliko ya mazingira na wakati. Kwa kufanya hivi, *Utenzi wa Mwana Kupona* umepata kueleweka na kutathminiwa kulingana na mazingira ya sasa. Kwa hivyo, utafiti huu umetuonyesha uwiano uliopo kati ya ufasiri wa kazi za fasihi kutokana na usomaji wa kazi hizo na mazingira chipuzi kwa upande mmoja na mazingira maalum ambamo msomaji anafasiri kazi iyo hiyo kwa upande mwingine.

Umuhimu wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika fasihi ya Kiswahili ni kigezo muhimu. Utenzi huu unatupa taswira ya mwanamke katika jamii hasa za Kiafrika. Huu ni Utenzi wa awali sana kutungwa na mwanamke na pia kushughulikia masuala ya wanawake. Kutokana na changamoto katika jamii hasa ndoa na nafasi ya mwanamke wa kisasa katika jamii. Utafiti huu ulisaidia kubainisha ikiwa usomaji wa kazi za fasihi hasa *Utenzi wa Mwana Kupona* unaweza kuwa suluhu kwa baadhi ya changamoto katika ndoa za sasa.

Shariff (1988: 158-159) anaeleza kuwa kuna ufungamano kati ya tungo za Uswahilini na maisha ya watu wake. Naye Masinde (2003:14) anasema utungaji wa tungo zile zozote za ushairi zina misingi zake karne nyingi zilizopita katika mila ya Waswahili. Kwa hivyo,

kupitia utafiti huu tuliweza kupata hisi za Waswahili wenyewe kuhusu *Utenzi wa Mwana Kupona*. Pia tuliaangalia hisi ya watu wengine wasio Waswahili. Sababu ni kuwa, watunzi huwa sauti ya jamii yao.

Fasihi ni kioo cha jamii na huichora jamii jinsi ilivyo. Hata hivyo, fani na maudhui hubadilika kulingana na mabadiliko ya mifumo katika jamii (Gibbe, 1990). Kwa hivyo, kuuchunguza *Utenzi wa Mwana Kupona* katika mikabala ya mabadiliko ya mazingira, wakati na mienendo lilikuwa ni swala muhimu. Kwani mabadiliko ya kimazingira, kiwakati, kihistoria, mienendo ya watu na asasi za kijamii huathiri usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi za jamii ya wakati maalum (Masinde, 2003).

Matokeo ya utafiti huu yalitoa mchango mkubwa katika kuuelewa zaidi *Utenzi wa Mwana Kupona* kupitia fasiri za wasomi mbalimbali. Aidha, kazi hii itahamasisha wasomi na wataalamu wengine zaidi ili kuendeleza tafiti za tenzi na ushairi hususan kipengele cha usomi na ufasiri wa tenzi na mashairi ya kale. Vilevile umewawezehsa wataalamu kulinganisha mazingira chipuzi ya kazi mbalimbali na mabadiliko yake sasa na vile mabadiliko haya yanaathiri usomaji na ufasiri wa kazi hizo.

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu. Umepitia vipindi mbalimbali na kila kipindi kina maarifa yake na huathiri mitazamo na mielekeo ya wanajamii. Kwa hivyo, *Utenzi wa Mwana Kupona* uliweza kufasiriwa katika miktadha mbalimbali. Kazi hii ilituwezesha kufahamu utofauti wa wasomaji  mbalimbali katika miktadha hii.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Kuna tenzi nyingi za Kiswahili ambazo zingeshughulikiwa lakini utafiti ulichunguza *Utenzi wa Mwana Kupona.* Utenzi huu ulichaguliwa kwa sababu ni maarufu kwa fasihi ya Kiswahili na umewaathiri watu mbalimbali na kwa muda mrefu (El- Maawy 2011). Kwa kuwa umepitia vipindi mbalimbali, jamii imebadilika kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Kwa hivyo, kulikuwa uwezekano wa utenzi huu kusomwa na kufasiriwa kwa njia mbalimbali na wasomaji sasa. Kuna vipengele vingi ambavyo vingechunguzwa na watafiti kuhusiana na utenzi huu. Lakini watafiti walijikita tu katika:

a) Mazingira chipuzi na ya usomaji sasa ya *Utenzi wa Mwana Kupona*
b) Maudhui ya utenzi huu
c) Wasomaji mbalimbali na ufasiri wake sasa.

Utafiti huu ulijikita katika kushughulikia usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Usomaji na ufasiri huu ulichunguzwa kwa mtazamo wa Uhistoria Mpya na Mwitikio wa Msomaji. Watafiti walifanya utafiti huu katika majimbo mawili tofauti ambayo ni kaunti ya Lamu na Kaunti ya Nairobi. Maeneo haya ya Pwani na bara yaliteuliwa na watafiti kimakusudi. Jimbo la Lamu liliteuliwa ili watafiti waweze kupata habari ya kimsingi kuhusu mazingira chipuzi ya utenzi huu pamoja na maoni ya wasomaji wazawa wa Lamu.

Jimbo la Nairobi pia lilikuwa lenye manufaa katika utafiti wetu kwani lilikuwa na wakaazi wa asili mbalimbali na mazingira tofauti ambao wameusoma utenzi huu. Maeneo haya mawili yalitupa data ya kutosha iliyotusaidia kukamilisha utafiti huu. Mbali

na hii, yalitusaidia kulinganisha na kulinganua ufasiri na usomaji wa wasomaji mbalimbali wa utenzi huu wa Mwana Kupona katika mazingira ya sasa katika maeneo hayo mawili.

Utafiti huu ulijishughulisha na vile aina ya wasomaji mbalimbali wanavyoufasiri *Utenzi wa mwana Kupona*. Utafiti huu ulijumuisha wasomaji ishirini (20) wa utenzi huu kutoka Lamu na wengine ishirini (20) kutoka Nairobi. Wasailiwa hawa waliteuliwa kupitia mbinu ya kusudio

Kwa kuwa utafiti ulilenga wasailiwa wa umri tofauti, yaani: vijana miaka 18-35, umri wa makamo miaka 40-49 na wazee miaka 50 na kuendelea mbinu tabakishi ilitumika kuteua wasomaji katika makundi haya.

## 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

### 1.6.1 Kuhusu Maudhui na Muktadha

Ndungo (1985) alishughulikia vile *Utenzi wa Mwana Kupona* unavyomsawiri mwanamke. Aliiangalia kazi hii kwa kumulika mtazamo wa kitamaduni na kijamii wa Waswahili kuhusu mwanamke. Tofauti na kazi yetu, yeye alitoa tu maoni yake bila kuangalia vile wasomaji wa kazi hii ya Mwana Kupona wanavyoisoma na kuifasiri. Kazi yetu ililenga kutathmini usomaji na ufasiri sasa wa utenzi huu. Hata hivyo, mtazamo wake wa kijamii na kitamaduni ulikuwa mhimili muhimu katika utafiti wetu. Utafiti huu wa Ndungo ulitusaidia katika kuchunguza namna mabadilliko ya mazingira na utamaduni yalivyoakisi na kuathiri kiwango cha usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Masinde (1992) aliangalia kwa undani swala la dhamira na mtindo wa mashairi huru. Alisisitiza maana ya mabadiliko na maendeleo ya maudhui katika ushairi. Alibaini kwamba ni muhimu wasomaji kuhamisha maudhui na miktadha ya kitamaduni kwa lengo la kufanikisha uelewa wa mashairi huru. Utafiti huu wa Masinde ni tofauti na wetu kwa kuwa ulishughulikia tu athari ya mabadiliko ya mazingira kwa mtunzi wa mashairi na vile anawasilisha maudhui yake bila kuonyesha athari ya mabadiliko haya katika usomaji na ufasiri wa kazi husika. Hata hivyo, utafiti huu ulikuwa muhimu kwa kazi yetu kwa kuwa ulitusaidia kuonyesha nafasi ya mabadiliko ya mazingira katika kuathiri vile wasomaji mbalimbali wanafasiri *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Swaleh (1992) alifafanua maudhui yaliyomo katika *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kuzingatia kipengele cha dini. Katika kazi yake, Swaleh alifafanua kuwa maudhui ya *Utenzi wa Mwana Kupona* yamejikita ndani ya mafundisho ya dini ya Kiislamu ambayo yanampa mwanamke nafasi anayostahili katika jamii yake. Anaeleza kuwa hadhi ambayo imepewa mwanamke katika jamii yake inamstahiki. Swaleh anadai kuwa yale majukumu ambayo mwanamke hupewa katika jamii ndiyo yanachangia kumdhulumu. Tofauti na kazi yetu, tulionyesha mwelekeo wa usomaji na ufasiri wa sasa? Kazi hii ilitufaa sana katika utafiti huu wakati wa kuhakiki maudhui ya dini katika *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Gakuo (1996) aliangazia swala la fani na uelewekaji wa *Utenzi wa vita vya uhuru* uliotungwa na Shaaban Robert 1945. Katika utafiti wake, Gakuo alieleza kuwa ni muktadha wa kihistoria ndio uliomhamasisha Shaaban Robert kutunga utenzi huu. Anasema kuwa muktadha na mazingira yanayomzunguka mwandishi ikiwa pamoja na historia yake ndiyo hutumika kama mihimili na chemuchemu ya mawasiliano na

maudhui katika ushairi. Kazi hii ya Gakuo ni tofauti na utafiti wetu kwani yeye alishughulikia ufasiri na uelewaji kwa ujumla bila kuzingatia usomaji wa kazi hiyo. Hata hivyo kazi hii ilikuwa yenye umuhimu kwa utafiti huu kwani ilitusaidia katika kufafanua mazingira chipuzi ya *Utenzi wa Mwana Kupona* na athari yake katika maudhui ya utenzi huu.

Momanyi (1998) aliangalia usawiri wa mwanamke muislamu katika jamii ya waswahili. Alichanganua kazi hii kwa kuangalia mashairi ya Muyaka wa Muhaji, Shaaban Robert na *Utenzi wa Mwana Kupona.* Alifanya hivi kwa kuzingatia utamaduni na itikadi ya Waswahili. Kazi yetu iliangalia namna utamaduni na itikadi hii inaathiri usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona.*

Njogu na Chimerah (1999) walishughulikia ufasiri wa mashairi ya kiswahili kwa kuzingatia fani za maudhui, muktadha na wahusika. Katika kazi yao, walidhihirisha kuwa shairi  aghalabu huwa ni fumbo ambalo ufumbuaji wake hutatiza mawasiliano kati ya hadhira na mtunzi. Kwa hivyo walipendekeza kuwa, ufasiri lazima uhusishe udenguaji wa vipengele vya ushairi wakati ule ambapo mfasiri anaunda ujumbe upya kulingana na muktadha wa wakati ambamo shairi hilo lilitungwa na baadaye wakati uliopo. Kazi hii iliufaa sana utafiti wetu kwa kuwa iltusaidia kuchanganua vipengele muhimu vya fani na maudhui namna vimebadilika kwa nia ya kuoanisha na usomaji na ufasiri wa vipengle hivyo katika *Utenzi wa Mwana Kupona* wakati wa sasa ili kuona namna usomaji sasa wa utenzi huu unabainisha udenguaji wa mazingira yaliyochipuza utenzi huu.

El- Maawy (2011) aliangalia mausio ya mke wa sasa na wasia ya Mwana Kupona. Aliangazia kipengele cha dhima ya utenzi huu kwa mwanamke wa kisasa. Kazi hii iliangaliwa bila kutumia mwongozo wowote wa nadharia na malengo mahsusi. Kazi yetu iliangalia usomaji na ufasiri wa utenzi huu kwa kuzingatia nadharia na malengo maalum. Kazi hii itatusaidia kuchanganua baadhi ya vipengele vya sasa kumhusu mke.

### 1.6.2 Kuhusu Nadharia na Ufasiri

Mpesha (1995) aliweza kuchunguza upokezi wa watoto katika tanzu zote za fasihi ya watoto. Aliuangalia upokezi kwa njia ya kusoma tena, kuandika na kuigiza. Kazi hii ya Mpesha ni tofauti na yetu kwa kuwa hii ilishughulikia watoto katika kusoma, kuandika na kuigiza na yetu ilishughulikia upokezi kupitia usomaji. Hata hivyo utafiti huu ulitufaa katika kukadiria upokezi wa wasomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

King'ei na Kemoli (2001) wanafafanua kuwa kuna hatua mwafaka za kiufasiri ambazo sharti zizingatiwe ili msomaji wa shairi fulani aweze kuyafasiri na kuyadondoa maudhui. Kazi hii ni tofauti na yetu kwani iliangazia tu hatua za ufasiri bila kuhusisha kazi maalum katika shughuli nzima ya usomaji na ufasiri wa kazi hiyo. Hata hivyo, kazi hii ilitusaidia kupambanua uelewa wa wasomaji tofauti wa utenzi huu wa Mwana Kupona katika usomaji na ufasiri sasa.

Masinde (2002) aliangalia maendeleo na mabadiliko ya kimaudhui katika mashairi huru. Masinde alionyesha namna mabadiliko ya kijamii yanavyoathiri ushairi wa Kiswahili. Kipengele cha mabadiliko ya mazingira kwa mujibu wa nadharia ya Uhistoria Mpya

kilikuwa muhumu katika kuchanganua usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Karuga (2005) aliangalia uhakiki na upokezi wa fasihi ya watoto wa shule za msingi zinazopatikana nchini Kenya. Tofauti na kazi yetu ambayo ilihusu vile wasomaji tofauti wanapokea kupitia ufasiri wa utenzi maalum *wa Mwana Kupona* katika mazingira ya sasa. Hata hivyo, utafiti huu ulitusaidia kuelewa zaidi kuhusu nadharia ya Mwitikio wa Msomaji.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu ulipewa mwelekeo na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji na ile ya Uhistoia Mpya. Misingi na mihimili ya nadharia hizi iliongoza katika kuhakiki, kufafanua na kutathmini usomaji, ufasiri na upokezi wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

### 1.7.1 Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji

Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji iliteuliwa kwa kuwa utafiti ulichunguza usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Nadharia hii huchunguza kitendo cha usomaji na kumchukua msomaji kama mwenye maana ya yale ayapatayo katika kazi ya fasihi. Kwa hivyo, nadharia hii ilituwezesha kubainisha aina mbailimbali ya wasomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Waasisi wakuu wa nadharia hii ni Iser (1974, 78), Tompkins (1980) na Fish (1980). Wakielezea nadharia hii, usomaji na upokezi wa matini katika vipindi au awamu ya

miaka ya hivi karibuni ilisitizwa. Waitifaki wa nadharia hii ni pamoja na: Hawthon (1987) na Cahill (1996)

Wahakiki na wataalamu ambao walizingatia mwelekeo huu huamini kuwa msomaji wa kazi maalumu ndiye huamua maana inayojitokeza katika kazi hiyo (Wamitila 2002). Mtazamo huu humpa msomaji hadhi kuu kwani humsawiri msomaji kuwa ndiye mwenye mchango wa juu katika uvyazaji na ubunifu wa maana katika kazi husika.

Umuhimu wa hadhira ya wasomaji katika kazi za fasihi unatambuliwa katika mtazamo huu Senkoro (1987:3). Senkoro anaendelea kufafanua kuwa nadharia tangulizi kabla ya Mwitikio wa Msomaji ziliwekea mkazo umuhimu wa mtunzi wa kazi ya fasihi. Tofauti na nadharia hii ambayo inashikilia mkazo kwa umuhimu wa hadhira.

Kwa mujibu wa nadharia hii, wasomaji hunasabishwa na kubashiri yale wanayoyapata ndani ya matini na matukio ambayo hao huyashuhudia maishani mwao (Bennet, 1995). Hii ina maana kuwa, nadharia hii hujaribu kuchunguza kitendo kizima cha usomaji huku msomaji akiwa ameangaliwa kama ndiye mwenye maana, imani na amali ambazo huweza kuthibitishwa na yale ayapatayo ndani ya kazi ya fasihi (Davies na Scleifer, 1986). Kwa mujibu wa nadharia hii, msomaji huchuja na kupanga yote yanayomzukia kama yenye dhana kwake binafsi kutokana na yale anayoyapata wakati wa usomaji wake.

Hawthon (1987) akimrejelea Iser (1960) anabainisha aina tatu za wasomaji ambao ni msomaji wa kukisiwa, msomaji aliyelengwa na msomaji wa viwango vyote. Wasomaji lengwa na wakisiwa watakuwa wenye umuhimu katika kuangalia wasailiwa ambao ni wazawa wa mazingira chipuzi na wana mawazo sawa na ya mtunzi. Wasomaji wa

viwango vyote watakuwa wenye manufaa katika kuangalia wale wasailiwa ambao sio wakisiwa wala lengwa bali wamesoma utenzi huu na kuelewa kwa undani wake.

Cahill (1996) akirejelea Iser (1960) anaainisha mirengo minne ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Mirengo yenyewe ni: Mwitikio msomaji husishi. Mrengo huu huchukuliwa kuwa ufasiri wa msomaji huhusisha hisia na mwelekeo pamoja na maarifa aliyonayo msomaji huyo. Mrengo wa pili ni Mwitikio wa Msomaji dhahania ambao unahusishwa na David Bleach. Mrengo huu unachukulia upokezi kama njia ya kuendeleza ufasiri wa kazi husika ya fasihi. Katika hali hii, ufasiri wa kazi fulani huangaliwa kwa kulenga dhamira ya mtunzi na kulinganisha ufasiri wa kazi hiyo katika muktadha wa sasa ili kuchunguza uendelezaji wa fasiri ya kazi mahsusi ya fasihi.

Holland (1968) aliendeleza mrengo wa Mwitikio wa Msomaji Kisaikolojia . Kwa mjibu wa mrengo huu, ufasiri wa kazi fulani hutegemea kile kilichomchochea au kumsukuma mtu kuisoma kazi hiyo.

Mwitikio wa Msomaji jamilishi ambao ni mrengo unaozingatiwa na Stanley Fish. Mrengo huu unachukulia kuwa ufasiri wa kazi husika hutegemea mtazamo katika jamii fulani. Fish (1980) anaeleza kuwa muono huu wa jamii hutegemea mila, desturi na utamaduni wa jamii husika. Katika hali hii wasomaji huongozwa na mtazamo ambao unachukuliwa na wanajamii katika kufasiri kazi hiyo.

Mirengo hii yote itakuwa yenye manufaa katika utafiti huu na itatumika pale itahitajika. Hata hivyo, mrengo wa Mwitikio wa Msomaji jamilishi ndio utatiliwa maanani sana na watafiti katika kazi yao.

Kwa mujibu wa Iser (1960) nadharia hii ina mihimili ifuatayo iliyotusaidia kuchambua kazi yetu:

1. Nadharia hii huzingatia msomaji, usomaji na upokezi. Muhimili huu ulisaidia mtafiti kuwabainisha wasomaji na kisha kuchunguza usomaji na ufasiri wao wa *Utenzi wa Mwana Kupona* sasa.

2. Huchukulia usomaji kama tendo ambalo hufanyika na kutekelezwa kwa wakati maalum. Mhimili huu unashikilia kuwa wakati wa kusoma au kupitia matini fulani mazingira huwa na athari katika maana au ufasiri wa kazi hiyo ya fasihi. Fish (1967) anaeleza kuwa wasomaji hufanya mikataba fulani na matini husika katika miktadha tofauti. Mhimili huu ulitusaidia katika kufafanua maudhui ambayo mtunzi alidhamiria na vile yamebadilika kutokana na mabadiliko ya wakati na mazingira.

3. Kuna hatua ambazo msomaji ambaye anatumia nadharia kusoma anafaa kufuata katika weledi wa kazi za fasihi:

a) Kubainisha muktadha wa matini usiyohusiana moja kwa moja na maandishi jinsi unavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.

b) Kudhihirisha kwamba yale maoni ya msomaji yana muumano na mada muhimu katika kazi husika ya fasihi.

Mhimili huu ulitusaidia kutathmini jinsi msomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona* ameweza kuathirika na utenzi huu sasa katika mazingira tofauti sana na yale chipuzi. Pia

kutathmini ikiwa ufasiri wa Mwana Kupona wa msomaji unahusu utenzi huu bali si kazi nyingine yeyote.

4. Kuna wasomaji wa aina mbalimbali kwa kila matini: msomaji aliyelengwa, kukisiwa na msomaji wa viwango vyote. Mhimili huu ulitusaidia kubainisha aina ya wasomaji katika utenzi huu.
5. Maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi husika. Mhimili huu ulitusaidia kubainisha nafasi ya tajriba na maariba ya wasomaji katika usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Mihimili hii ilikuwa na dhima kubwa tulipowachukuwa wasomaji kama waumbaji wa kazi zao wenyewe. Kwa kuwa hao huumba kazi yao wenyewe ya fasihi, hawakuwa na budi kuipa maana jinsi wanavyoielewa.

### 1.7.2 Nadharia ya Uhistoria Mpya

Nadharia nyingine ambayo ilikuwa nguzo ya utafiti wetu ni ile ya Uhistoria Mpya. Kulingana na Murfin (1991) aliyeungwa mkono na Rice (1993:259) Nadharia ya Uhistoria Mpya ni nadharia ya kisasa. Baadhi ya wataalamu wameeleza nadharia hii kama ya uyakinifu wa kitamaduni. Nadharia hii hutoa misingi ya uchambuzi wa matini katika miktadha ya kihistoria.

Nadharia ya Uhistoria Mpya inatofautiana na nadharia ya Uhistoria Mkongwe. Nadharia hizi zinatofautiana katika maswala ya udumaji na upendeleo. Wana- Uhistoria Mkongwe walizingatia na kusawiri wakati na historia iliyopita. Kwa upande mwingine Uhistoria Mpya huangalia mbinu geni katika usawiri wa matukio ya jadi katika muktadha wa sasa

(Faucault 1972). Kwa hivyo nadharia ya Uhistoria Mpya ilitumika katika utafiti huu kwa kuwa lengo letu lilikuwa tu kuangalia ufasiri wa utenzi huu kwa muktadha wa Kihistoria lakini kuchanganua ufasiri wake wakati wa sasa.

Waasisi wakuu wa nadharia hii ni Raymond Williams na Michel Faucault. Waitifaki wake ni pamoja na Hayden White, Bakhtin, Jacques Derrida, Roland Barthes, Gadamer, Marilyn Butler na Greenblatt.

Nadharia za kiufafanuzi na za kuhakiki ndizo zilisababisha kuibuka kwa nadharia hii. Nadharia za Mwitiko wa Msomaji, Uana wa Upambanyaji na Uchanganuzi Nafsia ni nadharia za hivi karibuni ambazo zimekuza, kuindeleza na kuchangia ukuwaji wa nadharia ya Uhistoria Mpya (McGann 1985).

Nguzo za nadharia ya Uhistoria Mpya zimejikita katika mawazo ya Michel Faucault (1972, 1977). Nguzo zenyewe ni:

i) Ni jambo la busara uchunguzi ufanywe kuhusu jamii halisi ambazo huzalisha fasihi katika mahala na wakati maalumu (Butter 1987).

ii) Utoaji na upokezi wa kazi za fasihi huathiriwa na matakwa za kisiasa na kijamii (Greenblatt 1980). Mtunzi yeyote hupata athari za mazingira ambazo aghalabu hujitokeza katika utunzi wake

iii) Isemavyo nadharia hii, kazi za fasihi haziwezi kutengwa na historia ambayo inahusika nayo kwani inarejelea vingine vilivyomo kwenye mazingira. Kwa hivyo maana ya utamaduni haina budi kuchunguzwa upya kwa sasabu

mielekeo, ujumi, usanii, maongozi urazini na thamani za jamii huwa zinabadilika kila uchao kiwakati kulingana na mabadiliko ya jamii

iv) Uchipukaji wa fasihi hutokana na tajriba ya maisha ya wanajamii na mtagusano wao kisiasa, kiuchumi na kijamii. Jamii ndiyo hujenga mazingira ambayo ni nguzo kuu ya msomaji wa kazi ya fasihi na uhakiki wake (Wafula na Njogu 2007).

**Mihimili ya Nadharia ya Uhistoria Mpya**

1. Kazi zote za kifasihi zina miktadha ya kijamii. Miktadha hii ya jamii husika huwa na mahusiano yanayoingiliana. Mhimili huu ulikuwa muhimu katika uchunguzi kuhusu jamii halisi ya mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* ambayo ilizalisha kazi hii mahali na wakati maalum na ambayo inapokea sasa kupitia usomaji na ufasiri (Butler 1987).
2. Historia ya wakati wa upokezi wa kazi ya fasihi, hadhira na baadaye lengo la uhakiki ni muhimu. Mhimili huu ulitufaa wakati wa kuangazia historia ya *Utenzi wa Mwana Kupona*, usomaji, ufasiri na upokezi wake wakati huo na upokezi wake wakati huu sasa kwani fasihi haiwezi kutengwa na historia yake kwa ambavyo historia hurejelea uwezo wa kiuchumi kijamii na kisiasa (Foucalt 1980).
3. Suala la miktadha na utamaduni wa kijamii lazima liangaliwe upya. Mhimili huu ulikuwa na manufaa tulikapokuwa tunaangalia maana ya utamaduni ambayo haina budi kuchunguzwa tena. Sababu ya kufanya hivi ni kutokana na hali ya

kubadilika badilika kwa maongozi, usanii, urazini, ujumi, mielekeo za thamani za jamii kuhusu asasi zote za jamii za kiwakati kutokana na maendeleo ya jamii. Pia ulitusaidia kutathmini usomaji, ufasiri na upokezi wa utenzi huu sasa.

4. Dhamira ya mwandishi huathiriwa na maendeleo ya kihistoria ya kazi ya fasihi ambayo inahakikiwa pamoja na ya jamii husika. Mhimili huu ulitufaa katika kuyachunguza mazingira yaliyochipuza*Utenzi wa Mwana Kupona.*
5. Muktadha wa chimbuko la kazi ile yoyote ya fasihi huwa na athari kwa ufasili wa matini ya kifasihi. Muhimili huu ulituezesha kuangalia muktadha uliotungiwa utenzi huu na namna wasomaji katika mazingira yale wanaupokea katika mazingira ya sasa.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti huwa ni nguzo inayozungusha utafiti husika. Utafiti huu ulikuwa wa aina ya usoroveya wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Mugenda (2008), utafiti wa aina hii huhusu kuchunguza hali ya mambo na kutolewa maelezo yake bila ya kulinganisha na mambo mengine.

### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Maktabani, watafiti walipata maelezo ya kimsingi kuhusu masuala ya kinadharia, usomaji kuhusu mazingira chipuzi na maudhui ya Utenzi wa Mwana Kupona pamoja na historia yake kwa ujumla. Watafiti walidurusu

miswada, tasnifu, majarida na makala tofauti tofauti yenye data inayohusiana na data yao ya utafiti.

Nyanjani watafiti walijikita katika jimbo la Nairobi hususani Chuo Kikuu cha Kenyatta na jimbo la Lamu. Utafiti wa nyanjani ulisaidia watafiti kukusanya data ya uchanganuzi wa utafiti wake.

### 1.8.3 Sampuli Lengwa na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Sampuli lengwa ya utafiti huu ilikuwa ni wasomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona* sasa katika jimbo la Lamu na Nairobi. Mbinu ya kusudio ilitumika kuchagua wasomaji ishirini (20) kutoka jimbo la Lamu na wengine ishirini (20) kutoka jimbo la Nairobi. Mbinu hii ilikuwa yenye umuhimu kwa kuwa utafiti ulihitaji sampuli mahususi iliyochaguliwa kimakusudi. Utafiti ulihitaji wasailiwa ambao wameusoma *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Kwa kuwa watafiti walilenga wasailiwa wa umri tofauti, yaani: vijana miaka 18-35, umri wa makamo miaka 35-49 na wazee miaka 50- mbinu tabakishi ilitumika kuteua wasomaji katika makundi haya. Mugenda (2008) anaeleza mbinu hii kuwa ile ambayo mtafiti hutumia akiwa amelenga makundi tofauti kutoka katika sehemu lengwa ya ukusanyaji data ya utafiti. Makundi haya huchaguliwa kulingana na nafasi yao katika jamii. Pia mbinu bahatishi ilitumika na watafiti ili kupata sampuli ambayo ni wakilishi kutoka mahali pa utafiti. Mbinu hii ni ile ambayo kila mhusika kutoka mahali pa utafiti alikuwa nafasi ya kuchaguliwa katika sampuli lengwa.

Watafiti waliteua sampuli kimakusudi kutokana na kile kinachowaongoza, ambazo ni sababu fulani maalumu za kiuchunguzi (usomaji na ufasiri). Aidha, Uteuzi pia

uliamuliwa na upeo na mipaka, malengo na maswali ya utafiti. *Utenzi wa Mwana Kupona* ulitumiwa ambapo mtafiti alitathmini usomaji na kukadiria ufasiri wa utenzi huu katika jamii ya sasa.

*Utenzi wa Mwana Kupona* uliteuliwa na watafiti kutokana na umuhimu wake katika jamii ya Waswahili hasa kipengele cha mwanamke katika jamii. Hata hivyo, utafiti haukulenga jamii ya Waswahili pekee kama sampuli bali ulilenga wasomaji tofauti kutoka jimbo la Nairobi na Lamu. Pia watafiti wanaamini kuwa kupitia utenzi huu, watapata data ya kutosha kulingana na malengo ya utafiti.

### 1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Watafiti walikusanya data yao maktabani na nyanjani. Nyanjani, wasailiwa walihojiwa kwa kuongozwa na maswali maalum yanayotokana na dhamira ya mtunzi wa utenzi huu. Majibu na maelezo ya wasailiwa yalirekodiwa ili kuchanganuliwa baadaye.

Watafiti walikusanya data maktabani na nyanjani. Maktabani tulisoma majarida, tasnifu na tahakiki ya *Utenzi wa Mwana Kupona* ili kuimarisha tathmini ya wale wanaousoma na kufasiri utenzi huu sasa.

Mihimili ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji na Uhistoria Mpya ilitumika katika ukusanyaji wa data lengwa. Mihimili ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ilitumika kukusanya data iloyohusu usomaji, ufasiri na upokezi wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Nayo nadharia ya Uhistoria Mpya iilichangia kukamilisha mambo kama dhamira, maudhui, mazingira ya kazi lengwa pamoja na mabadiliko ya maudhui ya fasihi na ufasiri wake kutoka awamu moja ya kihistoria hadi nyingine kutokana na mabadiliko ya wakati.

### 1.8.4 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa maktabani na nyanjani ilipangwa kulingana na vigezo maalum ambavyo ni pamoja na:

a. Mazingira
b. Dhamira na maudhui
c. Usomaji na ufasiri

Uchanganuzi wa data uliongozwa na maswali ya utafiti, malengo, pengo na mihimili ya nadharia.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Data yote iliyokusanywa na kuchanganuliwa iliwasilishwa: kwa njia ya maelezo, utoaji mifano na vilevile matumizi ya takwimu (asilimia), majedwali na michoro duara kuwasilisha matokeo ya uchanganuzi wa utafiti.

## 1.9 Kiishilio

Sura hii imeweka wazi suala la utafiti wa usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Imetathmini umuhimu na ufaafu wa suala la utafiti pamoja na malengo na maswali ya utafiti. Imeweka wazi mkondo na mchakato mzima wa utafiti huu huku nadharia, mbinu za kukuzanya data, kuchanganua na kuwasilisha matokeo zikitiliwa mkazo. Mambo haya yote yalituandaa na kutupelekea kutalii na kuchunguza maeneo ambayo utafiti unastahili kufanywa.

## SURA YA PILI

### 2.0 Mazingira ya Utunzi wa Mwana Kupona na Usomaji Sasa

### 2.1 Utangulizi

Kulingana na nadharia ya Uhistoria Mpya, historia ya wakati wa upokezi wa kazi ya fasihi, hadhira na baadaye lengo la uhakiki ni muhimu. Sura hii ilichunguza historia, mazingira ya mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona*, dhamira ya mtunzi, mazingira ya sasa na falsafa ya mtunzi ili kuelewa msingi na muktadha wa chimbuko la *Utenzi wa Mwana Kupona*. Hali hii inatokana na sababu kuwa mazingira ya mtunzi kwa ujumla, dhamira yake pamoja na falsafa huwa na athari katika utunzi wake. Masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa huupa utunzi mkondo na mwelekeo maalum. Vipengele hivi pia huathiri aina mbalimbali ya wasomaji hasa katika usomaji na ufasiri wa kazi husika.

Utunzi huathiriwa na kupewa mwelekeo fulani na mazingira ya kijamii na kihistoria. Sura hii inajadili mazingira ya kijamii na kihistoria katika kisiwa cha Lamu kilichoko kaunti ya Lamu hadi wakati wa utunzi wa *Utenzi waMwana Kupon*a mwaka wa 1960. Ufafanuzi wa historia ya mazingira chipuzi ya utenzi huu umetuezesha kufafanua dhamira na maudhui ya mtunzi. Hali hii ilituwezesha kueleza athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui, pamoja na usomaji na ufasari wa *Utenzi wa Mwana Kupona.*

### 2.1.1 Mazingira ya Mtunzi

Mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* sawa na msanii yeyote wa kazi ya fasihi, ni zao la jamii hiyo. Mabadiliko na maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii humwathiri (Masinde 1992). Athari za aina hii ndizo humpa mshairi hamu au jazba ya kutunga kuhusu lile linalomchoma moyo. Hii ina maana kuwa wasanii hawawezi kuepuka athari za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aidha, mtunzi wa kazi za fasihi hawezi kuepuka athari ya mikinzano ya kitabaka inayojidhihirisha katika jamii hiyo.

Masuala ya kijamii ni muhimu, kwa hivyo mtunzi yeyote hawezi kujiepusha kamwe na masuala ya kiijamii yaliyomzunguka anapoitunga kazi yake. Hii inatokana na ukweli kuwa mwandishi ni mwanajamii na hana budi kupata athari ya jamii yake kwa kiasi kikubwa na mambo anayoyapitia, kuyasoma, ambiwa au kuyashuhudia yakiwa yanawakumba wanajamii wenzake. Hali hii humpa mtunzi msukumo wa kuyatungia masuala ya kijamii ambayo yanampendeza au hata kumchukiza.

Kwa mujibu wa King'ei (2000: xv) maudhui ya fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo wakati wake. Kwa hivyo, hali hizi hazina budi kuwaathiri watunzi. Kwa ambavyo yanayotendeka katika mazingira humuathiri, mtunzi hujenga tajriba, hupata mguzo, msukumo mshawasha na ilhamu ya kutunga kuhusu suala fulani. Mazingira ya mtunzi na mambo anayopitia mtunzi maishani mwake huwa na athari katika utunzi (Syambo na Mazrui, 1992). Ufafanuzi huu unaenda sambamba na mhimili wa nadharia ya Uhistoria Mpya unaodai kuwa kazi za fasihi haziwezi kutengwa na historia ambayo nayo kwa kuwa hurejelea vingine vilivyomo kwenye mazingira.

Sanchez (1973) anafafanua kuwa utunzi huendelezwa na mtunzi katika jamii kwa mipaka inayozunguka au inayohusika na jamii hiyo. Kwa hivyo, fasihi inahusu usanii unaoonyesha maingiliano, hali, mikinzano na mivutano baina ya binadamu na mazingira yake.

Fischer (1959) anasema kuwa kazi yoyote ya fasihi ina umuhimu kwa jamii. Anafafanua baadhi ya majukumu ya fasihi kama vile kuzindua, kuwaidhi na kuburudisha kwa nia ya kuwatia jazba wanaoisoma kazi hiyo ili kuleta mazinduzi na mageuzi yanayohitajika katika jamii. Msanii katika kufanya mambo haya, huongozwa na itikadi na imani ya jamii ambayo hujibainisha katika umbuji wake (Masinde 2003). Kulingana na Mwitikio wa Msomaji, katika usomaji na ufasiri msomaji hana budi kubainisha dhamira ya mtunzi kwani usomaji na ufasiri wa kazi mahususi hubadilika kutoka msomaji mmoja hadi mwingine na wakati hadi wakati kulingana na mabadiliko ya kimazingira na kijamii. Haya yamebainika katika usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* (Taz. Sura ya 4).

Mpokeaji huathirika pakubwa kifikra na kihisia baada ya kusoma kazi fulani ya fasihi (Masinde 2003). Fasihi bora ni ile ambayo inahimiza uboreshaji wa uimarishwaji wa ujenzi wa jamii imara yenye usawa na uadilifu. Kwa mujibu wa Uhistoria Mpya, msomaji wa kazi mahsusi hana budi kuichunguza hadhira ya sasa na hata ya baadaye kwa kueleza lengo na mazingira ya usomaji wake. Hali hii inatokana na ukweli kuwa kazi ya mtunzi ni kiungo chake na jamii anayoilenga. Kauli hii ina maana kuwa mtunzi huwa na matarajio kwamba ataandamana na hadhira ambao kwa muktadha huu ni wasomaji kulingana na jinsi anayosawili uhalisi ulipo (Fischer 1959, Sauchez 1973). Haya

yameweza kujitokeza kupitia wasomaji wa kuakisiwa na lengwa wa *Utenzi wa Mwana Kupona* ambao wamebainishwa kupitia nadharia ya Mwitikio wa Msomaji.

Kwa mujibu wa Ngugi (1981) kazi yoyote hiyo ya fasihi huwa na uhalisi na hushawishi watu kuufuata mwelekeo fulani unaohusiana na huo uhalisia. Kwa hivyo, fasihi hujaribu kutoa mwanga namna jamii fulani inavyouona ulimwengu kwa ujumla. Jambo hili lilibainika kupitia ndharia ya Uhistoria Mpya ambayo inachukulia fasihi kama nguzo na sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii. Aidha, kauli hii ya Uhistoria Mpya inatiliwa msisitizo na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji kupitia kipengele ambacho kinafafanua kuwa usomaji sawa na utunzi ni tendo ambalo hufanyika na kutekelezwa katika wakati maalum. Inashikilia kuwa wakati msomaji anapopitia kazi mahsusi kwa nia ya kufasiri, basi mazingira huwa na athari katika ufasiri wa kazi hiyo. Hii ina maana kuwa ni vyema kuzingatia muktadha wa utunzi, wa msomaji na ule ambamo kazi lengwa imekita ili kuelewa ufasiri ipasavyo.

Wasanii wengi kutoka Pwani ya Kenya waliotunga tenzi kama vile *Utenzi wa Mwana Kupona*, *Inkishafi*, na *Fumo Liyongo* wanatambuliwa kupitia mazingira yao ya utunzi. Hii inatokana na kauli kuwa utunzi ni njia moja ya kujitambulisha na itikadi na utamaduni wa jamii. Ngugi wa Thiong'o anaeleza uhusiano wa mtunzi na mazingira yakeifuatayo.

> …. Mtunzi hurejelea mazingira yake kibanafsi kwa kuwa ni suala lenye umuhimu mkubwa, hushughulikia usala hili kwa umakini akizingatia mabadailiko katika maingira ya jamii yake… hali hii inatokana na ukweli kuwa mtunzi huchongwa na mazingira ya jamii… (Ngugi 1972:47) "tafsiri yangu"

Kupitia utunzi, msanii hufafanua jamii yake kwa kuweka wazi mengi yanayohusu jamii. Kwa hivyo, mtunzi anapoandika huwa anafafanua jamii yake. Kutokana na maelezo haya, *Utenzi wa Mwana Kupona* utaeleweka vyema sasa ikiwa mazingira chipuzi yatawekwa wazi.

Kwa mujibu wa Gakuo (2014), ushairi kama kipengele cha fasihi ni kihifadhi cha kihistoria. Kauli hii ya Gakuo inaafikiana na kipengele cha Uhistoria Mpya kisemacho, hitoria hurejelewa katika fasihi ambayo hurejelea mambo yaliyomo katika jamii. Kwa hivyo katika usomaji na ufasiri, msomaji hana budi ya kurejelea historia na mazingira ya jamii yake.

**2.1.1.0 Historia ya Mwana Kupona Binti Mshamu**

Mwana Kupona alizaliwa miaka ya 1830 (Hitchens 1935). Alikuwa ni mtunzi wa tenzi za Kiswahili ukiwemo *Utenzi wa Mwana Kupona.* Alizaliwa katika kisiwa cha Pate na alikuwa mke wa mwisho wa Sheikh Bwana Mataka ambaye alikuwa Sultan wa Siu. Mwana Kupona na Bw. Mataka walikuwa wamezaa watoto wawili kabla ya kifo chake mwaka wa 1958. Mwaka wa 1960, Mwana Kupona alitunga utenzi huu maarufu wa Mwana Kupona kwa mtoto wake msichana wa miaka 14-17 aitwaye Hishima Bint Mataka. Mwana Kupona alitungia bintiye akiwa amelazwa hospitalini kwa nia ya kumpa wosia mtoto wake wa kike kuhusu masuala ya ndoa na nafasi ya kiuana ya mwanamke katika jamii.

Msailiwa M1 ambaye nilimhoji tarehe 12/11/2017 kule Lamu mjini, alieleza kuwa huenda utenzi huu haukutungwa na Mwana Kupona ila Mwana Kupona alitumia wosia

wa Umama binti Harithi kwa bintiye Ummu Uyas. Msailiwa huyu alidai kuwa wosia wa Umama binti Harithi ulitungwa kabla ya ujio wa Uislamu katika lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, kwa kuwa ni suala la mjadala na ambalo linahitaji utafiti zaidi, utafiti huu ulichukulia kuwa Mwana Kupona ndiye mtunzi halisi wa Utenzi wa Mwana Kupona.

Kwa mujibu wa Ndung'o (1985) mumewe Mwana Kupona alijulikana kama Muhamaad Is-haq bin Mbarak bin Muhammad bin Umar I' Famau na alikuwa mashuhuri katika jamii yake. Hata hivyo, alifahamika sana kwa jina la Bw. Mataka ambaye alikuwa Sheikh wa Siu. Bwana mataka alikuwa na wake wanne, Mwana Kupona akiwa mmoja wao. Wake wengine, watatu ni pamoja na Mwana Pepo, Mwana Harusi wa Dena na Mwana Kikau. Bwana mataka alizaa watoto wawili na Mwana Kupona, Muhamed Sheikh ambaye alikuwa wa kiume na Mwana Hashima binti Sheikh ambaye ni wa kike aliyetugiwa utenzi huu. Utenzi huu ulitungiwa Mwana Kupona, Mwana Hishima akiwa na miaka 16-17 (Weaner 1915).

#### 2.1.1.1 Wazazi wa Mwana Kupona

Mwana Hashima bint Nasiri bi Abdalla Abdisalam aliolewa na Bwana Mshamu wa Bwana Kombo Mshamu Mbatawi katika kiasi 1220 AH (1805/06AD) katika mji wa Pate. Kwa mujibu wa Kirkman (1964) wakati huo mji wa Pate ulikuwa ukitawaliwa na Fumo Maadi wa Bw. Tamu (mtoto) wa Bw. Mkuu Nabhahani ambaye alikuwa mfalme 1191 - 1224AH (1777-1809AD). Fumo Maadi anasemekana kuwa ndiye alikuwa wa mwisho katika wafalme wa mwisho na wenye nguvu wa Pate. Aidha El- Maawy (2011) anabainisha kuwa yeye ndiye alikuwa babu wa daraja ya pili wa Mwana Hashima Bint Nasiri, mamake Mwana Kupona na ndiye mwanzilishi wa ujenzi wa Ngome ya Lamu.

### 2.1.1.2 Kuzaliwa Kwa Mwana Kupona

El- Maawy (2011) anaeleza kuwa Mwana Kupona alizaliwa baina ya 1225-1227AH, (1810-1812BK) kulingana na umri wake. Kwa mujibu wa mhojiwa M6 niliyehoji tarehe 25, Novemba 2016 katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, jina la Kupona katika Waswahili hupewa mtoto aliyezaliwa baada ya wazee kupitia shida, au mtoto aliyezaliwa dhaifu hata akahofiwa kutoishi. Kusudio huwa ni kumtakia heri njema na kumuombea mola anapoitwa.

Ingawa hakuna ushahidi wa kuonyesha chanzo cha jina kupona kwa Mwana Kupona, hueda lilitokana na maafa yaliyotokea mwaka wa 1227AH (1812BK) aliyozaliwa Mwana Kupona ambapo kulitokea vita kati ya wa-Amu na wa-Pate (El-Maawy 2011). Vita hivi vilitia hasara na mashujaa wengi kutoka Pate waliuwawa kwa hivyo huenda katika wa-Pate jamii ya wazazi wa Mwana Kupona ilikuwemo na hivyo kuitwa jina hilo. Kwa upande mwingine, huenda babake Mwana Kupona alikuwa mmoja wa wanajeshi wa Pate walioshambulia Lamu, yeye pamoja na watu wake walisalimika na janga la vifo vilivyotokea na hivyo kumuita mwanawe Mwana Kupona.

Huenda kukawa na sababu nyingine zilizosababisha yeye kuitwa hivyo. Kwa mfano kuwepo kwa bibi kutoka kizazi cha aitwaye Kupona ingawa sikupata ikiwa kuna yeyote aliyeitwa hivyo.

Mwana Kupona alikuwa wa asili ya Wabatawi. Kwa mujibu wa Chittick (1967) Wabatawi ndio walikuwa watawala wa asili kabla ya kuja kwa utawala wa Nabhahani.

Hapo awali, watawala wa miji ya Waswahili walibainika kama mwenye mui na baadaye ikageuzwa na kuwa sulutani.

Shekhe Mataka wa Mbaraka bin Muhammad I'shaka bin Umari bin Mataka bin I'shaka bin Mbaraka Mataka alikuwa Msiu aliyezaliwa Siu. El- Maawy (2011) anamtaja Mwana Hadie wa Msinji kuwa mamake Mataka. El- Maawy anabainisha takribani 1252 AH. (1836AD) kama wakati wao (Mwana Kupona na Bw. Mataka) wa kuoana. Bw. Mataka alikuwa mtetezi mkubwa, kiongozi na jemedari wa majeshi ya vita katika kupinga uongozi wa nchi za kigeni na mij jirani katika uongozi wa Siu (El- Maawy 2011).

Sababu za umaarufu wa utenzi huu zinahitilafiana baina ya wanaumme na wanawake (Topan 2006). Wanaume wanachukulia kuwa ni wajibu wa mwanamke kumpa wosia mtoto wake wa kike. Kwa upande wa wanawake, utenzi huu unaonyesha wosia wa mama anayejali mtoto wake kabla hajafa. Maelezo ya Topan yalidhibitishwa na kazi hii katika sura ya nne ambapo wanaume wengi waliunga mkono Mwana Kupona. Hata hivyo, wanawake hawakukubaliana na mawazo mengi ya Mwana Kupona.

Nafasi ya mumewe Mwana Kupona kama Sheikh inamueka katika tabaka la juu. Kwa mujibu wa Mulokozi (1982) jamii ya Mwana Kupona ilikuwa yenye umwinyi ambao ulikuwepo kabla wareno kuwasili.

> …Utabaka ulikuwepo kitambo kabla ya waneno kuwasili na ushahidi wake unapatikana katika maandishi ya karne ya kumi hadi kumi na nne… (Mulokozi 1982)

Ndung'o (1985) akimnukuu mulokozi (1982) anaeleza kuwa maingiliano kati ya wageni kutoka bara Hindi na Waafrika ndiyo yalianzisha umwinyi Uswahilini. Wageni hawa walikopa lugha na baadhi ya mila za Waswahili. Kwa upande mwingine, walileta itikadi na mila za kiislamu katika jamii ya waswahili.

Kutokana na maingilianio ya Waswahili na wageni hawa, tabaka la matajiri lilijitokeza. Maisha ya Waafrika hawa yaliimarika kutokana na hali yao ya uchumi. Hali hii ilipelekea Waafrika hawa kuishi maisha tofauti ambayo ni bara kuliko wenzao walioishi kando ya miji. Harakati hizi ndizo zilizaa au kuanzisha jamii zenye umwinyi katika upwa wa afrika mashariki. Kutokana na uwezo wa kiuchumi, matajiri waliamua kununua ardhi kubwa ambapo walihitaji Waafrika wenzao wa vijijini waje kuwafanyia kazi katika hayo mashamba. Hali hii ndiyo ilisababisha kutokea  mgawanyiko wa kitabaka ambapo wafanyikazi katika mashamba haya wakawa kwenye tabaka moja nao matajiri wakawa katika tabaka lingine.

Mulokozi (1982) anabainisha kwamba tabaka tawala lilikuwa lile lenye ardhi nao wafanyikazi wakawa tabaka la watwana mbao walifanya kazi katika mashamba ya matajiri ili kupata riziki. Tabaka la watwana liligandamizwa, kuonewa na kunyanyaswa kwani walilazimishwa kufidia sehemu ya ardhi ambayo walipewa kwa mtumizi yao, walitakiwa kugharamia sehmu ya ardhi waliopewa kwa matumizi yao waliotakiwa kugharamia sehemu ya ardhi waliopewa kwa kumfanyia kazi mwenye ardhi.

Kuhusu utunzi, Mulokozi (1982) anaeleza kwamba tabaka tawala lilitunga mashairi ya kutoa wosia kwa nia ya kuendeleza serikali ya umwinyi. Kwa upande mwingine,

watwana walitoa maoni yao kupitia fasihi simulizi. Hivyo, wosia wa Mwana Kupona kwa bintiye kuwa asitangamane na watumwa ovyo ovyo ilikuwa njia ya kuendeleza umwinyi. Mwana Kupona katika ubeti wa 20 anasema:

> …Sitangane na Watumwa,
> Ila mwida wa khuduma,
> Watakuvutia tama,
> La-buda nimwkwambiya…

Ubeti huu unatuonyesha kuwa Mwana Kupona anatokana na tabaka la wamwinyi na inaafikiana na maoni ya Allen (1978) aliyefafanua kuwa bwanake Mwana Kupona Bw. Mataka aliitawala Siu mwaka wa 1810-1848.

#### 2.1.1.3 Itikadi na Imani ya Mwanamke Mswahili wa Kiislamu

Mwana Kupona alikuwa mwanamke mfuasi wa dini ya Kiislamu (Werner, 1934). Kutokana na ukweli huu, ni vyema kuelewa itikadi na imani ya mwanamke Mswahili wa kiislamu pamoja na nafasi yake. Uelewa kuhusu vipengele hivi vya mwanamke ulituwezesha kufahamu dhamira ya mtunzi. Aidha ilituwezesha kuafiki ukweli wa kipengele cha nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ambacho kinabainisha wasomaji katika makundi kulingana na namna wanafasiri kazi maalumu. Kwa kuwa tulilenga usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona* wa wazawa wa mazingira chipuzi na wale wa mazingira tofauti ya Nairobi, kufahamu mwanamke wa Kiislamu kulisaidia katika uchanganuzi wa wasomaji na wafasiri wa maeneo haya tofauti.

Kwa mujibu wa Mbaabu (1985) kuja kwa waarabu na uislamu maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki, kulikuwa na athari kubwa kwa jamii ya Waswahili. Katika hali hii, itikadi za jamii hii ziliathiriwa pakubwa na dini ya kiislamu.

Dini ya Kiisilamu ilizingatia usawa baina ya wanawake na wanaume. Kulingana na Momanyi (1998) usawa katika uana ulidhihirika wakati wa mtume Muhamaad ambapo wanawake walipewa majukumu maalum ya umma. Kulingana na kumbukumbu ambazo zinahusu matamshi na matendo ya Mtume Muhamaad (hadith) ambazo zilihifadhiwa na Aisha ambaye ni mmoja wapo wa wake za Mtume. Ali (1998) anaeleza kuwa Zainabu Umm- ul- Muwayiid ambaye ni mwanamke aliyesifika kama hakimu katika karne ye kumi. Aidha Fatuma ambaye alikuwa bintiye mtume muhamaad na mkewe Khalifa alikuwa mshairi na mhubiri mashuhuri. Dhibati hii inahitilafiana na vikwazo vya utawa ambavyo vimewekewa sasa katika jamii za Kiislamu, Waswahili wa pwani ya Kenya wakiwemo.

Katika *The Challenge of Islam*, kitabu kilichoandikwa na Aisha Lemu na kuhaririwa na Gauhar (1978:267) inaelezwa kwamba maandiko ya kurani sura 33:32-33 ndio chanzo cha utawa. Maandiko yenyewe yanasema:

> … Nyinyi wanawake ambao ni wa mtume, Ninyi si tofauti na wanawake wale wengine… make majumbani mweni na msidhubutu kuonyesha nyuso na mapambo yenu jinsi walivyofanya wanawake wa ujahili… (Gauhar 1978:276).

Strobel (1979) anaeleza kuwa katika enzi zile, utawa haukuwahusu wanawake wengine ila wanawake wa akraba ya mtume. Hata hivyo anasema desturi hii ya utawa ilisambaa katika jamii zote za kiislamu duniani wakati wa taathira za Kiislamu. Kauli hii ya Strobel inaungwa mkono na Ndung'o (1985) ambaye anasema ni wakati huu ambapo dhana ya kumwona mwanamke kama kiumbe ambaye anapaswa kutawishwa ilinea. Anasisitiza kuwa ingawa kurani iliendelea kuhubiri usawa, jamii ambazo ni za Kiisilamu ziliendeleza asasi ya utawa kwa kisingizio cha dini kwa nia ya kumwekea mwanamke mipaka. Katika hali hii mwanamke aliwekwa katika kitengo tofauti na mwanamume, siku zilivyosonga jamii ya waislamu wakafanya utawa itikadi yao.

Kurani sura 2:229 inampa mme uhuru wa kumpa talaka mkewe anavyopenda hata bila taarifa. Kutokana na hali hii mwanamume ana haki ya kidini ya kuoa hadi wake wanne. Kwa mujibu wa msailiwa M1 niliyehoji tarehe 13 Novemba, 2016 Lamu mjini, wanawake wa sasa wasio na uwezo wa kiuchumi hufanya bidii ya kuwatumikia waume wao ili wasipewe talaka. Alibainisha kuwa uhuru wa mwanamume wa kuoa wake zaidi ya mmoja huleta mashindano baina ya wake wenza katika mapambo ya nyumba na mapishi. Dhima ya mashindano haya ni kuhifadhi mapenzi ya mumewe. Jambo hili ni la lazima katika jamii ya kiislamu baina ya wake wenza. Huenda hali hii ndiyo ilimpelekea Mwana Kupona kumuusia bintiye kuhusu jinsi ya kuishi na kumlinda mumewe.

Inyani (1934:31) anasema panapotokea haja, ndoa za Kiislamu hushirikisha mke zaidi ya mmoja. Kutokana na suala hili, mwanamke huweza kutayarishwa kwa majukumu ya ndoa akifahamu jambo hili. Majukumu muhimu huwa ni kuipamba nyumba,

kujirembesha na kumpikia mume wake vyakula vitamu. Kwa hivyo Mwana Kupona alikuwa tu anayafanya majukumu yake kama kwa bintiye.

Kulingana na Abdul-Bahal ambaye alikuwa mmoja wa mitume wa Muhamaad, Mungu aliumba binadamu wote bila utofauti wowote (Ahmed, 1992). Anasema kuwa binadamu wote ni sawa. Anasema hivi:

> … Binadamu ni kama ndege walio na mabawa mawili. Moja ni ya mke na nyingine ni mume. Mabawa yote mawili yasipokuwa na nguvu sawa basi ndege huyo hawezi kupaa kuelekea mbinguni…(Ahmed 1992)

Kuna ushahidi kuwa wanawake walioishi wakati Muhamaad, walihusika katika shughuli zote za kijamii. Hata hivyo Ahmed (keshatajwa) anaeleza kuwa wanawake waliokuwa na uhuru huu zaidi walikuwa wa tabaka la juu. Anafafanua kuwa wanawake kutoka tabaka la juu walihudhuria sala katika miskiti, walihusika katika masuala ya vita. Kwa mujibu wa hadithi za kale, muhamaad aliyachukulia maoni ya wanawake katika jamii kuhusu dini na masuala ya kijamii kuwa yenye umuhimu mkubwa. Kwa mujibu wa Ahmed, baada ya kifo cha Muhamaad wanaume waliona kuwa kumpa mke usemi katika jamii ni hatari kwa wanaume na hivyo haifai. Waliona kuwa hii itakuwa kama kumpa mwanamke uwezo juu ya mume wake.

Utamaduni wa Waswahili ambao ni waislamu unahitaji mwanamke awe mnyenyekevu. Kwa mujibu wa Momanyi (1998) hali hii inatokana na athari ya dini ya kiislamu. Hata hivyo, baadhi ya wasailiwa kutoka Nairobi walibainisha kuwa suala la unyenyekevu wa mwanamke kwa mwanamume lipo katika kila jamii ambayo ni ya kuumeni.

## 2.2 Mazingira ya Sasa

Uhalisi wa jamii umo katika chimbuko la sanaa (Senkoro 1987). Mtazamo wa Senkoro unatufafanulia dhahiri namna ambavyo sanaa ni zao la mazingira ambayo pia hushughulika na uzalishaji mali. Kwa mujibu wa Chacha (1997) uchumi una uhusianio mkubwa na fasihi. Hali ya uchumi katika jamii fulani na wakati maalum huathiri sanaa iliyopo. Kadri mfumo wa uzalishaji mali unavyoendelea kubadilika ndivyo pia fasihi inavyodhihirisha hayo mabadilikio. Kulingana na Mwitikio wa Msomaji ni muhimu msomaji kubainisha muktadha wa matini usiyohusiana moja kwa moja na maandishi jinsi unavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.Kwa hivyo, mabadilikio haya pia huathiri usomaji na ufasiri wa kazi husika ya fasihi (Taz. sura ya 4). Hii ina maana kuwa hali ya uchumi ndiyo huelekeza fasihi.

Kutokana na hali ya kijamii, fasihi huelekezwa na msukumo na nguvu za kihistoria na kijamii. Kwa hivyo haiwezi kujiepusha kamwe na masuala ya siasa, uchumi, jamii na tabaka. Maswala haya huwa yenye umuhimu kulingana na wakati kwa kuwa hujishughulisha na jamii na kuiathiri katika muktadha huo. Hali hii inatokana na ukweli kuwa fasihi yoyote ile nzuri ni lazima ijumuishe hali ya jamii katika uhakiki wake (King'ei 2000). Kwa mfano, *Utenzi wa Mwana Kupona* ulitungwa wakati wake na kusawiri masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ya wakati huo. Hata hivyo msomaji wa utenzi huu katika mazingira ya sasa hana budi kuathiriwa na masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika usomaji na ufasiri wake wakati wa sasa kama inavyojitokeza katika sura ya nne. Kulingana na Uhistoria Mpya, matakwa ya kijamii na kisiasa huwa na athari katika usomaji na ufasiri wa kazi za fasihi.

Fasihi huathiri hisia na fikra za mpokeaji. Kwa mujibu wa Masinde (2003), fasihi nzuri ni ile ambayo inahimiza, kuimarisha au kuboresha ujenzi wa jamii ambayo ni imara na yenye kuendeleza uadilifu wa usawa na haki.

Mtunzi hutarajia kuwa yuko pamoja na hadhira yake kihisia na namna anavyousawiri uhalisia uliopo. Hali hii inawiana na kipengele cha nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambacho kinainisha aina mbalimbali ya wasomaji (Taz. sura 4).

Kipindi (1810-1960) ambacho Mwana Kupona binti Mshamu alitunga *Utenzi wa Mwana Kupona*, alilazimika kutunga kwa kuzingatia mafundisho ya dini ya kiislamu kwa kuzingatia masuala ya maisha ya wakati wake (Mulokozi 1999). Utunzi huu ulitokana na kaida za utamaduni wa zama hizo na utungo wenyewe unawakilisha mawaidha na tungo za utamaduni wa kipindo hicho.

Katika ushauri wake kwa bintiye, Mwana Kupona anamuusia amheshimu mumewe wala asiwe mshindani. Pia anamfafanulia kuwa hatima yake siku ya kiama ifikapo imo mikononi mwa mumewe. Aidha, anamshauri ampapase, ampepee, amnyoe ndevu na kumsifu. Kwa mujibu wa Masinde (2003), utenzi huu ulitiliwa maanani sana na ndio maana maadili yake yaliendelea kutumiwa katika matendo ya kimila. Wanawake na jamii ya Uswahilini iliitikia vizuri wito wa Mwana Kupona na kuutumia katika malezi na mafunzo ya binti zao (Mulokozi 1999). Kutokana na hali ya mazingira ya wakati huo, wanawake hawakuona chochote kibaya.

Tofauti wakati huu, hali ya mwanamke imebadilika kutokana na mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mabadiliko haya ambayo yametokana na mabadiliko ya kimazingira

ndiyo yamesababisha mabadiliko katika usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika mazingira ya sasa (taz. sura ya 4). Hii ina maana kwamba, mwanamke wa sasa ni tofauti na mwanamke wa enzi za Mwana Kupona.

Kutokana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa mwanamake wa sasa haheshimu nafasi ya mumewe na hivyo kusababisha ndoa nyingi kukumbwa na vikwazo na changamoto nyingi na kutodumu. Hali hii inatokana na mabishano na mashindano mengi (Masinde 2003). Matukio haya ni kinyume cha mwanamke wa zama za Mwana Kupona ambaye alikuwa wa kutii na wa heshima kwa mumewe. Huenda hali hii ya mabadiliko ndiyo ilisababisha Robert (1967) katika *Insha na Mashairi* kwa shairi la "*Mwanamke wa Sasa*" (uk. 11) kusema:

> …Walakini, mambo yamebadilika sasa, kazi ya mwanamke si utii. Hutaka usawa wa cheo na wa haki. Mwanamke wa sasa ni asi… (Robert 1967)

Ni la muhimu tukubali kuwa ulimwengu unaendelea kubadilika na wakati. Hivyo jamii ya sasa haina budi kuwa na mwelekeo na mtazamo tofauti kuhusu mwanamke na nafasi yake. Katika mazingira ya sasa wanawake wengi wanaona na kuhisi kuwa wananyanyaswa na wanaume. Hali hii inatokana na mvutano wa usasa na ukale ambapo katika enzi za Mwana Kupona, mwanamke aliishi chini ya umwamba wa mwanamume kutokana na utamaduni na itikadi za jamii. Katika enzi za sasa, mwanamke ameendelea kiuchumi na kisiasa na anaweza kujisimamia.

Wanaume wengi wamemsawiri mwanamke wa sasa kama muasi kutokana na ile hali ya kutozingatia kaida za kijadi ambazo mwanamke wa sasa anaona kuwa zilikuwa za

kumlemaza na kumfanya mpumbafu wa kukubali kuchezewa akili kwa kupagazwa sifa zilizogubika uhalisia wa ubinadamu wake. Hata hivyo, lazima ikumbukwe kuwa nyakati za sasa zimekuwa na msisimuko mkubwa ambapo watu wanataka kujikomboa dhidi ya dhuluma za kila aina na unyanyasaji. Hivyo, imesababisha wanawake wengi katika jamii ya sasa kutaka mapinduzi na mageuzi kwa madai kuwa wamenyimwa haki, wameonewa wamedharauliwa, wamepuuzwa na kunyonywa.

Katika jamii ya sasa, ruwaza za kijamii na familia zimeathiriwa na utamadani wa kisasa, ukoloni, ustawi wa miji na viwanda na ubepari wa sasa (O'connel 1997). Athari ya vitu hivi imesababisha njia mpya ya maisha. Hii ni thibitisho kwamba jamii zinaendelea kupitia mabadiliko mengi. Kwa hivyo jinsi isemavyo nadharia ya Uhistoria Mpya, suala la utamaduni halina budi kutazamwa upya ili kuenda sambamba na hali ya maisha ya wakati huu. Hii inatokana na ukweli kwamba utamaduni na jamii huthiriana (Veeser 1989)

Kwa mujibu wa Masinde (2003) suala la wanawake wa sasa wanayaigiza tu yale yanayofanywa na wanaume kwa kupapia usawa. Hali hii ya sasa imesababisha kubomoka kwa misingi ya kijamii na kitamaduni ambayo iliwezesha ndoa kudumu enzi za Mwana Kupona. Suala hili la kutaka usawa ikatika ndoa limechangia huzuni, fujo na matatizo mengi ya ndoa za sasa.

Katika *Kichomi* (1974), Kezilahabi anasisisitiza kuwa yale yanayoonekana wakati wa sasa, zamani hayakuwepo. Hapa alijaribu kuonyesha kuwa kufaulu kwa ndoa za sasa kunategemea watu binafsi. Anasema linalosabisha haya ni usasa ambao umevuruga

mambo. Kwa sasa, maadili ya jamii yamebadilika. Kumezuka mitafaruku ya kiuchumi, kitamadanu na kijamii. Masuala yanayohusu utandawazi wa kijinzia yametanda kote. Wakati wa sasa, suala la haki za wanawake limekita mizizi, mtazamo wa dini ya Kiislamu na Kikristo jinsi ilivyo katika Mwana Kupona kuwa mwanamke ni mtiifu, mnyenyekevu, msaidizi wa mumewe na mwenye upendo limepoteza maana

Katika jamii ya sasa, wanawake wamepewa umuhimu wa kiuchumi, kisiasa na kijamii sawa na wanaume. Kwa hivyo mabadiliko ambayo yametokea katika ndoa hasa usawa wa mwanamke na mwanamume tangu zama za Mwana Kupona katika jamii yameweza kutathminiwa na kuelezwa katika muktadha wa mabadiliko ya kihistoria. Murfin (1991) anasema dhana ya utamaduni haina budi kuchunguzwa upya katika nyakati tofauti kwa kuwa thamani za jamii na mielekeo yake hubadilika na wakati. Kipindi maalum cha historia ya jamii hueleza sababu zinazoathiri kazi ya kisanaa. Kwa hivyo, historia hupeana fasihi umbo kimaudhui, kifani na vile vile kuamua utaratibu na mwelekeo wake.

Ulimwengu wa sasa umebadilika kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ugumu wa kiuchumi maishani hauruhusu mke wa sasa kukaa tu nyumbani akimtaraji mumewe kumuridhisha na kumkimu kwa kila jambo kama vile kumvisha, kumgharamia matibabu na kumlisha. Gharama ya sasa imepanda na mke hafai kuzaa tu kama hayawani. Aidha suala la mke wa sasa kubaki kama mtumishi na mtumwa wa mumewe haliwezekani (Masinde 2003).

Mugomba na Nyagah (1980) wanabainisha elimu ya kimagharibi kama moja wapo ya sababu ya uozo katika jamii ya sasa. Elimu ya kimagharibi inatumiwa kwa kuwatenganisha wasomi na uhalisi wa mazingira yao kiuchumi, kisiasa, kijamii na

kitamaduni. Kwa mfano hapo awali katika enzi za Mwana Kupona, mwanamke wa Kiislamu hakustahili kuchanganyika na wanaume. Pia nafasi ya mwanamke ilikuwa nyumbani. Tofauti na wakati huu ambapo watoto wa kike na wa kiume wanatangamana mashuleni na hata wanaketi katika dawati moja. Pia, elimu imeleta mabadiliko ya kiuchumi ambapo kutokana na elimu, wanawake wanapata vyeo na maongozi mbalimbali katika jamii na hivyo kujisimamia kiuchumi. Kwa mujibu wa Kezilahabi (1974) kutokana na mafunzo ya elimu ya kimagharibi wasomi wameiga mila na desturi na tamaduni za nchi za kimagharibi na kudharau mila zao. Hali hii imeathiri mwanamke wa sasa. Hivyo, mwanamke wa sasa ni kinyume cha yule wa zama za Mwana Kupona.

Katika hali hii ni wazi kwamba katika mazingira ya sasa, mambo yamebadilika kutokana na mabadiliko na maendeleo ya kijumuia kwa mujibu wa wakati, vijana wamepata zinduko na tajriba mpya kupitia elimu ya kigeni (Hoogvelt 1976). Kwa hivyo wamejizika na kubobea zaidi ndani ya utamaduni wa kigeni ambapo wamekengeuka. Mabadiliko hayo ndiyo yamesababisha mabadiliko katika usomaji na ufasiri sasa wa utenzi wa Mwana Kupona (taz. sura ya 4).

Kutokana na ugumu wa kiuchumi katika jamii ya sasa. Baadhi ya wanawake wa sasa hujiingiza katika uzinifu ili kuuza miili zao. Jamii ya sasa inaabudu pesa na hivyo pesa inapokosekana katika ndoa baadhi ya wanawake hujitoza katika usinzi ili kupata pesa. Hali hii inasababisha kutokuwepo uaminifu. Tabia ya aina hii ni tofauti sana na zama za Mwana Kupona

Tukio la mwanamke wa sasa kubadilika limeathiri sera ya maisha katika jamii ya sasa. Wanawake wanaendelea kuwa na msisimko mkubwa ambapo sasa wanapigania nafasi zao katika jamii. Wanadai haki sawa na wanaume katika nyanja mbali mbali za maisha ya jamii na maendeleo. Kutokana na hali hii, mielekeo ya wanajamii wengi imebadilika ili kuakisi maendeleo ya jamii. Kwa hivyo maisha ya sasa kuhusu ndoa yamepata ufafanuzi mpya ili kuafikiana na maendeleo ya kijumuiya (Taz. sura ya 4). Matukio haya ni ya kijamii na kihistoria na yanaathiri usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika mazingira ya sasa.

Jinsi imeonyeshwa katika sura ya nne, usomaji na ufasiri wa utenzi wa Mwana Kupona umefanywa na wasomaji mbalimbali kulingana na wakati. Masuala ambayo wamezungumzia yanafungamana na jamii ya sasa. Hali hii inaafiki kipengele cha nadharia iliyoongaza utafiti huu kuwa wakati wa usomaji mazingira huwa na athari katika ufasiri wa kazi ya fasihi.

**2.3 Kiishilio**

Uchunguzi kuhusu historia ya mtunzi ni muhimu kwa kuwa fasihi huzaliwa katika mazingira mahsusi ya kihistioria (Msokile 1993). Sura hii imedhihirisha kwamba fasihi haiwezi kamwe kutengwa na maswala ya kijamii kwa kuwa ni kama kielelezo cha hali halisi za kijamii. Msanii huishi katika jamii na huathiriwa na maswala tofauti ambayo yamo katika jamii yake. Hii inaonyesha kuwa matukio ya kijamii na sanaa ni sehemu mbili za sarafu moja. Aghalabu, msanii hufanya utunzi wake kulingana na hali halisi ambayo inapatikanana katika jamii yake, na hali hii huwa chimbuko la kazi yake.Sura hii

pia imetoa maelezo kuhusu mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* pamoja mazingira ambayo yalimzunguka ili kubainisha nafasi ya mazingira katika utunzi, usomaji na ufasiri wa kazi husika. Wellek na Warren (1949) wanabainisha kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya mazingira ya mwandishi na imani yake katika kazi yake ya sana. Namna mwandishi anavyobainisha matukio hutegemea jinsi falsafa yake inavyoathiri namna anavyochora uhalisia wa maisha. Tukizingatia maelezo haya, kazi ya Mwana Kupona inaakisi kuwa ni zao la amali za mazingira ya wakati fulani. *Utenzi wa Mwana Kupona* ni kioo au kielelezo ambacho kinatoa ushahidi wa itikadi na mwenendo wa kijamii yake, kidini, kiuchumi, kiitikadi, kisiasa na kitamaduni. Ni kielelezo kinachoonyesha uwiano baina ya muktadha mzima wa jamii ya wakati wake na sekta hizo. Kutokana na uchanganuzi huu, itikadi ya mtunzi imebainika. Itikadi hii imejadiliwa ili kuona iwapo ina athari yoyote kwa aina mbalimbali ya wasomaji wa sasa katika ufasiri wao (Taz. sura ya 4)

Aidha sura hii imeonyesha mazingira ya sasa ambamo utenzi huu unasomwa na kufasiriwa. Imebaini kuwa tukio la mwanamke wa sasa kubadilika limeathiri sera ya maisha katika jamii ya sasa. Wanawake wanaendelea kuwa na msisimko mkubwa ambapo sasa wanapigania nafasi zao katika jamii. Wanadai haki sawa na wanaume katika nyanja mbalimbali za maisha ya jamii na maendeleo. Kutokana na hali hii, mielekeo ya wanajamii wengi imebadilika ili kuakisi maendeleo ya jamii. Kwa hivyo maisha ya sasa kuhusu ndoa yamepata ufafanuzi mpya ili kuafikiana na maendeleo ya kijumuiya (taz. sura ya 4). Matukio haya ni ya kijamii na kihistoria na yanaathiri usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika mazingira ya sasa.

Sura inayofuata inashughulikia maudhui katika *Utenzi wa Mwana Kupona*.

# SURA YA TATU

## 3.0 Maudhui Katika Utenzi wa Mwana Kupona

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti umeshughulikia maudhui katika *Utenzi wa Mwana Kupona na* namna mazingira yameathiri ubainishaji wa maudhui haya. Maudhui yaliyoshughulikiwa ni pamoja na maudhui ya utegemezi, utangamano, mausio ya mke bora, maudhui ya dua na hatimaye maudhui ya mke aliyetimia. Jinsi tulivyoonyesha katika sura ya pili, sawa na fasihi yenyewe, utunzi wa fasihi ni zao la mazingira maalum katika kipindi mahsusi cha historia ya jamii. Aidha, sura hii imebainisha kuwa mfumo wa jamii ya mtunzi huathiri namna anavyousawiri na kuuona ulimwengu wake. Hii ina maana kuwa fasihi hupewa mwelekeo, umbo, pamoja na eno la kushughulikia na nguvu za kisiasa, kiuchumi na kijamii kulingana na jamii husika (Odaga 1985).

Kazi za fasihi huweza kueleweka na wasomaji wake kupitia maudhui yake ambayo yanahusu jamii na wakati fulani. Magaju (1974:4) akinukuliwa na Ndung'o (1985) katika makala yake ya *The East African Literature and East African writer*, anaifafanua fasihi kama kielelezo cha hali halisi ya maisha. Kulingana na Uhistoria Mpya, msanii kama mwanajamii, husimulia na kuandika kutokana na tajriba anayoipata katika jamii anamoishi.

Maudhui katika fasihi yoyote ile huzalika kutokana na jinsi jamii ilivyo wakati wa utunzi (King'ei, 2000:xv). Kwa hivyo, matukio katika nyanja mbalimbali za maisha hayakosi kamwe kuwa na athari kwa watunzi. Watunzi huwa wameathiriwa na mambo mengi

maishani mwao. Mambo haya hayana budi kujitokeza katika tungo zao (Ngugi 1981). Ukweli huu unaafikiana na kipengele mojawapo cha nadharia ya Uhistoria Mpya kinachodaikuwa fasihi haiwezi kamwe kutengwa na ile historia ambayoinahusika nayo.

Odaga (1985:xi) anaifananisha fasihi na kioo cha jamii kwa madai kuwa unaposoma kazi yoyote ile ya fasihi ya jamii husika, basi msomaji hujifunza kutokana namaudhui mengi kuhusu jamii hiyo. Utamaduni na imani za kisiasa, kijamii na kiuchumi hujidhihirisha katika fasihi yao. Hii ina maana kwamba, fasihi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Katika hali hii, fasihi huendeleza falsafa, historа na imani ya wabuni wake pamoja na yale yajumuishayo urathi wao kitamaduni katika wakati maalum. Hivyo, binadamu hukulia katika jumuia mahususi na kwa kawaida mtazamo wake hufinyangwa kwa kiasi na utamaduni au mazingira yake.

King’ei (2000) anasema maudhui katika fasihi yoyote ile hutokana na hali iliyomo katika jamii husika kwa wakati wake. Masuala ya kisiasa, kiuchumi na tabaka ni yenye umuhimu kwani huishughulisha jamii na kuathiri katika muktadha wa utunzi. Hii inatokana na ukweli kuwa fasihi yoyote nzuri, ni ile inayojumlisha hali ya jamii katika uhakiki wake. Kwa mfano, mashairi ambayo yanatungwa wakati wa sasa yamesanifu ujumuia wa maisha yetu yote. Hali hii inatokana na kipengele cha Uhistoria Mpya, kuwa matakwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii huathiri utunzi na upokezi wa kazi za fasihi. Kwa hivyo, hakuna budi athari hizi kujitokeza katika kazi ya mtunzi yeyote kwa mujibu wa wakati.

Falsafa ya kimsingi ya mtunzi kuhusu maumbile na hali ya jamii huathiri jinsi mtunzi anavyouchora uhalisi wa maisha kupitia maudhui. Jambo hili ndilo humwelekeza mtunzi katika ubainishaji wa matukio kiutengano au kihusisho; yakibadilika au katika utuvu. Hii ina maana kuwa falsafa ya maisha ya msanii ndiyo huwa msingi wa itikadi yake.

Fasihi ni taaluma ambayo hujengwa na maneno katika fani mahususi ili kutolea maudhui yanayomzingatia binadamu maishani (Kirumbi 1975). Maneno hutumiwa kisanaa kwa kumtazama binadamu na uhusiano wake na wenziwe, viumbe vingine, itikadi na mazingira kwa jumla. Kwa mujibu wa Njogu (1997 a) lugha hutumiwa kibunifu katika fasihi ilikusheheni matukio na imani ya msanii katika jamii yake. Kulingana na Uhistoria Mpya, fasihi hurejewa na wakati huo nayo kurejelewa na vitu kando yake katika mazingira. Hivyo ndivyo ilivyo katika *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Fasihi huwa na wajibu wa kuonya, kufunza, kuburudisha, kurudi, kustarehesha, kuzindua, kuadilisha miongoni mwa mambo mengine. Kwa mujibu wa Kirumbi (1975:11)

> … Fasihi humushugulisha mtu na mazingira yake. Humuonyesha mazingira yale ili ayaone... humtazamisha ili kumfanya afikirie kuyabadilisha mazingira hayo, hali yamambo na tabia kwa manufaa yake mwenyewe ili ajiendeleze kiuchumi, kisiasa, kijamii na kisanaa…(Kirumbi 1975:11)

Aidha Kirumbi (keshatajwa) anasema fasihi ni taaluma ambayo hujengwa kwa maneno katika fani maalum kwa nia ya kutolea maudhui ambayo huzingatia maisha ya bindamu.

Maneno hutumiwa kisanaa katika kuangalia uhusianio wa binadamu na wenzake, viumbe vingine, mazingira yake na itikadi kwa ujumla.

Katika misingi hii, maudhui ya *Utenzi wa Mwana Kupona* yalichanganuliwa. Maudhui yaliyoshamiri katika utenzi huu ni:

### 3.2 Maudhui ya Utegemezi

Utegemezi wa mwanamke kwa mumewe unajitokeza katika *Utenzi wa Mwana Kupona* kupitia majukumu ya mke kwa mume wake. Utenzi huu unatuonyesha kuwa majukumu ya mwanamke yanatokana na ile hali ya mwanamke kuendelea kumtegemea mume wake. Utegemezi huu unamisingi yake katika mfumo wa kuumeni wa jamii ya Waswahili ambayo iliupea uhalisi wa kidini. Uhalisi huu unatokana na jukumu katika kurani ambalo linampa mume wajibu wa kutunza watoto na mke (Momanyi 1998).

Wosia huu wa Mwana Kupona unatokana na itikadi ya jamii ya Waswahili (taz. sura ya 2). Itikadi ambayo ilikuwa imejikita ndani ya jamii kwamba mke alistahili kutumishwa nyumbani na hangeruhusiwa kamwe kushiriki katika majukumu ambayo yalikuwa yanapatikana katika mipaka iliyoko nje ya nyumba. Utenzi huu unaonyesha kuwa kazi za nje zilikuwa za mwanamme ambaye aliwezeshwa kuwa na nguvu za kiuchumi.

Kwa mujibu wa Msailiwa M4 aliyehojiwa tarehe 17-11-2016 katika Kisiwa cha Pate, utaratibu huu wa kuwapa wanaume nguvu za kiuchumi na kuwafungia wanawake katika mazingira ya nyumbani uliwanyima wanawake uhuru wa kiuchumi na hivyo kuendeleza utegemezi wa wanawake kwa wanaume. Katika hali hii, alifafanua kwamba ingawa dini

ya Kiislamu inamhitaji mwanamume kuikimu nyumba yake na kuweka milki ya mke kuwa nyumbani, haina maana kuwa mwanamke hawezi kushiriki katika majukumu mengine. Hali hii imebadilika katika mazingira ya sasa jinsi imeonyeshwa katika sura ya nne.

Mwanamke wa Kiislamu jinsi Mwana Kupona anavyomshauri bintiye kuvaa hijabu na kuweza kufungiwa nyumbani ni itikadi ambayo inaendelezwa kwa kisingizio cha dini (Ngung'o 1985). Itikadi hii inapunguza uhuru wa mwanamke ili asiwe na nafasi ya kushiriki katika shughuli zingine zozote katika nje ya nyumba yake.

Kutokana na hali hii, ni wazi kwamba Mwana Kupona alichota maudhui ya utegemezi wa wanawake kutoka mazingira yake. Katika jamii ya Mwana Kupona sawa na tamaduni nyingi za kiislamu mwanamke hakuwa na nguvu za kiuchumi na hivyo kumfanya ategemee mwanamume.

### 3.3 Utangamano

Utangamano katika jamii ni suala muhimu lenye kutiliwa maanani. Kila jamii ina mila na desturi zake kulingana na jinsi wanajamii hao wanastahili kutangamana. Masuala ya utangamano katika jamii hujikita katika hali ya jamii hiyo kisiasa, kiuchumi na kijamii.Maudhui ya utangamano katika utenzi huu yamejikita katika wosia wa Mwana Kupona kwa bintiye Mwana Hashima jinsi ya kuishi na watu kwa jumla.

Mwana kupona katika wosia wake anachora mume kama ndugu wa karibu kwa mwanamke. Katika ubeti wa 57 anasema:

…Mausio ya mvuli,
Allah Allah yaamili,
na nduguzo na ahali,
Wapende na kuusiya…

Katika kazi hii Mwana Kupona anamuueleza Mwana Hashima umuhimu wa utangamano baina yake na mvuli na nduguze. Anachukulia mume kama mkono wa pili na mshirika mkuu wa maisha ya mke. Hii inatokana na ukweli kuwa mke na mume wanapooana huwa wamefanya mkataba wa kufanya kazi pamoja, kujenga shirika moja na nyumba moja yenye mawazo ya pamoja. Ushirika huu hauwezekani kamwe bila ya mashauriano, masikizano, kuaminiana, kutoshana, kukubaliana na kupendana.

Kwa kawaida maisha ya ukoo hutengemea matumizi ya fikra za mke na mume. Ama ndugu ambao msingi wa uhusiano ni mapenzi. Hali hii ni tofauti katika wasomaji wa sasa (Taz. sura ya 4.).

Mwana Kupona alikuwa katika jamii ya Wamwinyi (Taz. Sura ya 2). Hali hii inaonyesha kuwa jamii ya Mwana Kupona ilikuwa ya utabaka ambapo tulikuwa na watumwa waliofanya kazi katika mashamba ya  wamwinyi. Katika ubeti wa 20 Mwana Kupona anasema:

…Sitangame na watumwa,
Ila mwida wa khuduma,
Watakuvutia tama,
la-buda nimekwambiya…

Katika ubeti huu Mwana Kupona anamshauri bintiye asitangamane na watumwa au watu wa tabaka la chini isipokuwa anapowapa kazi. Ubeti huu unabainisha kuwa Mwana Kupona alikuwa katika tabaka la juu (taz. sura ya 2.).

Kwa mujibu wa msailiwa mmoja niliyemhoji tarehe 15/11/2016 eneo la Lamu mjini, kuna hali ya uoga baina ya jamii ya Waswahili kuzungumzia utumwa. Wengi wanaukumbuka kwa ubaya na uchungu. El Maawy (2011) anaeleza kuwa enzi za Mwana Kupona, watumwa na watu wengine hawakuwa katika daraja moja ingawa waliishi kama ndugu kulingana na dini ya kiislamu ambayo inaenziwa sana na jamii ya Waswahili.Hali hii ya utumwa wa zama za Mwana Kupona ilitokana na hali ya siasa na uchumi ambapo wasiojiweza katika jamii walichukuliwana kuwa wahudumu wa wale wa tabaka la juu.Hata hivyo, ubeti wa 37 unabainisha kuwa watumwa hawakuwachiwa kazi zote ubeti huu unasema.

…Mwanangu siwe mkoo,
Tenda kama uonao,
Kupea na kosha choo,
Sidharau mara moya…

Ubeti huu unaonyesha kwamba ingawa Mwana Kupona alikuwa na watumishi, yeye mwenyewe alihakikisha kuwa vioo na nyumba yake iko safi. Alimuusia Mwana Hashima aufuate mfano wake kwa kutowategemea watu na kuihudumu nyumba yake.

Wakati wa utumwa watu walifanyishwa kazi nyingi sana (Momanyi 1998). Katika utumwa, watu walikuwa sehemu ya vifaa vya kazi. Hivyo, kulikuwa na matumizi ya amri kwa lengo la kufaulu pamoja na kutumia njia za uhusiano katika muda wa kazi. El-

Maawy (2011) anasema hii ndiyo ilikuwa sababu ya watu wa tabaka la juu kujiepusha na wale waliokuwa katika utumishi wao.

Katika ubeti wa 21, Mwana Kupona anamuonya bintiye asitangamane na waovu. Anasema:

> …Siandamane na wainga,
> wasoyuwa kuitunga,
> ziumbe wasioyo change,
> wata kuwaqurubiya…

Kwa mujibu wa Mwana Kupona anaposema "wainga-ziumbe wasiyo change" alilenga kuonyesha kuwa hawa ni watu ambao hawana akili, wanyang'anyi, Wezi au wahuni. Watu sampuli hii hakuna dogo kwao na sio wa kutosheka, na wakiingia ubovuni huingia kwa wingi. Kutokana na msisitizo huu wa Mwana Kupona, ni wazi kwamba hangependa Mwana Hashima akurubiane nao kabisa.

Kwa kawaida, binadamu huwa na tabia ya kujivuna na kujiona yeye ni bora kuliko mtu mwingine yeyote. Hali hii inapotokea huonyesha jinsi watu hawajali heshima au usawa na wengine. Kuchanganyika au kutangamana hufunza binadamu namna ya kutukuzana na kutangulizana. Hakuna yeyote aridhikaye kwa kuvunjiwa heshima. Hakuna akubaliaye kufanywa duni ya mwingine. Hali hii ndiyo alipelekea Mwana Kupona kumuusia bintiye kuhusu umuhimu wa unyenyekevu kwa utukufu. Katika ubeti wa 15 Mwana Kupona anasema;

> …Tena mwanangu idhili,
> mbee za maqabaili,

uwaonapo mahali,
angusa kuwenukia…

Mwana Kupona anaposema “mbee za maqabaili” alikuwa na nia ya kumkumbusha Mwana Hashima kuwa ingawa anatokana na koo za kifalme za Pate na Lamu, kuna wale wenye vyeo na ni lazima awaheshimu. Katika hali hii, Mwana Kupona alimkumbusha binti yake madhumuni ya mwenyezi mungu ya kuwaumba watu mbalimbali. Anasema lengo kuu lilikuwa ni kuheshimiana, kujuwana na kutambua jinsi ilivyo katika Kurani takatifu.

> … Enyi watu! Ukweli ni kwamba tumewaumbeni kutokana na Adam (mwanamume) na Hawwa (mwanamke). Tumekufanyeni makabila na mataifa ili mfahamiane… aheshimiwaye sana kati yenu ni Yule amchae mungu zaidi katika nyingi (Kurani tukufu :49:13) (tafsiri yangu)

Mwana Kupona anamuusia bintiye awe na unyenyekevu wa kiwango cha juu cha kustaarabika baina ya mke na mme. Anaposema “idhili” kwa mujibu wa El- Maawy (2011) ni kumuusia bintiye aigize kuwa mpole, mnyenyekevu, asiyejivuna au kujisifu, mtulivu na mwenye kuheshimu wengine. Kwa hivyo, ikiwa atagandamizwa katika ndoa atakuwa au unyonge rohoni lakini aonyeshe unyenyekevu mbele ya watu.

Mwana Kupona anamuonya bintiye kuwa hakuna haja ya kunena jambo ikiwa litasababisha ubaya. Anamfahamisha kuwa, jambo hili linapotokea, ni vyema kunyamaza kimya. Mausio hayo yanajitokeza katika ubeti wa 18 anaposema:

…Neno nao kwa mzaha,

yaweteao furaha,
Yawapo ya ikraha,
Kheri kuyanyamaliya…

Maudhui haya yanaoana na shairi la Muyaka lenye mada *Kimya Kina Mshindo,* katika shairi hili Muyaka anafafanua umuhimu wa kimya. Anasema;

…Kimya chataka kumbuu, viunoni mutatile,
Kimya msikidharau, nami sikidharawile,
Kimya kina mambo mbele, tahadhari na kimya…
(Abdulaziz 1979).

Katika hali hii, Mwana Kupona alitaka kumfahamisha bintiye kuwa ndani ya usemi kuna uhodari wa kusikiliza na uhodari huo hupatikana kupitia kimya. Alitaka bintiye afahamu kuwa ni vyema kuchunga ulimi wake kwa kuwa ndani ya usemi huwa kuna kushutumiana, kufitiana na kusingiziana. Kwa mujibu wa Masinde (2003) hizi ni sifa mbovu za uzungumzi.

Mwana Kupona katika ubeti wa 19 anamuusia bintiye kuwa asiyachukuwe yale mambo ambayo hayana ushahidi wa kutosha. Anasema:

…Wala witukue dhana,
kwa mambo usoyaona,
na kwamba na kunong'ona,
tahadhari na kwambia…

Tumeona mara nyingi watu wakibabaishwa na mambo yasiyo na msingi. Hata sheria hubabaishwa kwa kufuata dhana za uovu ambazo huwaweka wengi taabuni kwa dhuluma

bila kudhibitishwa. Mausio haya yalitokana na mafunzo ya kurani tukufu ambayo inasema:

> …enyi mlioamini mtu mwenye mambo yasiyokuwa tu kutegemewa. Msikubalie tu akikuja na harai yeyote, lakini fanyeni upelelezi kwanza ili msije mkawadhuru watu kwa ujahili na kujuta mliyoyatenda…(Kurani takatifu 1969).

Jumla ya utukufu wa Mwana Kupona ilikuwa ni msimamo wake wa tabia nzuri, ada njema, kufuata dini na kudumu kwa silka ya kiungwana pamoja na uchukivu wa vitendo visivyokuwa na maana. Alikuwa anataka bintiye apuuze na kuepukana na tabia za wanawake wawili au zaidi kuambatana bila uoga na kukaa kando wakinong'ona. Suala hili lilifafanuliwa na Mwana Kupona jinsi ilivyo kulingana na mazingira ya wakati wake. Hata hivyo, mambo yamebadilika katika mazingira namna imebainishwa katika sura ya nne.

Katika ukurasa wa (61) Mwana Kupona anamtahadharisha bintiye dhidi ya kuchanganyika au kutangamana na wakubwa. Anasema:

> …Watu wote waumini,
> kwako na wawe wendani,
> sipende masalatini,
> washinde ukiwepua…

Kwa mujibu wa Uhistoria Mpya, mazingira ya mtunzi huathiri pakubwa utunzi wa kazi ya fasihi. Mawazo ya Mwana Kupona kuhusu suala hili la utangamano na faume linatokana na hali kuwa mumewe Bw. Mataka alikuwa ni wa tabaka la juu na alifanikiwa

kutokana na uaminifu baina yake na wafuasi wake. El Maawy (2011) anasema kuwa Mwana Kupona aliwatazama Masulutani wa Pate kwa tashwishi ndipo akamuonya bintiye dhidi ya kupendana na kutangamana nao. Aliona kuwa matakwa ya Masulutan ni kutawala na wako tayari kuadhibu au kupigana na yeyote asiyetii. Pia El- Maawy anabainisha kuwa Mwana Kupona alitaka bintiye ajitahadhari na fitina za Masulutani baina yao katika ukoo wa kifalme ambazo zilikuwa na lengo la kugawanya jamii na kuvunja mikataba. Aidha lililomfika Mwana Kupona mwenyewe baada ya mumewe kuaga lilisababisha amuonye bintinye. Mwana Kupona alipokataa kuolewa na mmoja wa masultani ilisababisha kufanyiwa kinyume na akataka kumdhili lililosababisha Mwana Kupona ahame Pate. Hata hivyo, Mwana Kupona anamfahamisha bintiye kuwa watu wote wawe marafiki bila kubaguliwa. Mawazo haya ya usawa yanajidhihirisha katika ubeti wa 61 na 62 ambapo anamuonya kuwa hakuna mawazo ya ubwana au udhahabu juu yawengine. Hapa anabainisha kuwa ubora wa mtu hutegemea vitendo bali sio kizazi wala uhodari wake

### 3.4 Mausio ya Mke Bora

Kulingana na Uhistoria Mpya, uchipukaji wa fasihi hutokana na tajriba ya maisha ya wanajamii na mtagusano wao kisiasa, kiuchumi na kijamii. Jamii na tajriba ndiyo hujenga mazingira ambayo ni nguzo kuu ya msomaji wa kazi ya fasihi na uhakiki wake (Wafula na Njogu 2007).

Mwana Kupona  na mawazo yake kuhusu mke bora yanategemea maisha yake. Kwa mfano, mausio katika utenzi huu ni mwendo wa maisha yake ambayo amefupisha katika

ubeti wa 51 hadi 56. Ndani ya beti hizi, ameyaeleza maisha yake na mumewe ya kutolalamika hata siku moja. Hili linabainika wazi katika ubeti wa 55 anaposema:

…Tangu hapo hata yeo,
siyanyamaa kilio,
nikumbukapo pumbao,
na wingi wa mazoea…

Mwanamke bora ni lazima aombe radhi kwa mumewe. Katika ubeti wa 24 mtunzi anasema "…Naawe radhi mumeo, Siku zote mukao…" ubeti wa 25: "…Na ufapo… wenda uitukuzie, ndipo upatapo ndia…"ubeti wa 26: "…Siku ufufuliwao, nadhari nda mumeo…" na ubeti wa 27: Kipenda wende peponi… kinena wende motoni, huna budi utatiwa…" Mishororo hizi zinamlika nafasi ya kuomba radhi katika ndoa. Ni vyema kutaja kuwa haya yote ni mawazo ya dini ya kiislamu ambayo ndiyo ilikuwa dini ya Mwana Kupona.

Jinsi tulivyoonyesha katika sura ya pili, utumishi wa mke kwa mume wake kulingana na mfunzo ya Kiislamu ni itikadi inayotiliwa juu ya mwanamke kuwa mtiifu, mwenye malezi mema na uke wema. Kulingana na msailiwa M2 niliyemhoji tarehe 11/11/2016 eneo la Shela, suala la mke kumtii mume ni kweli kulingana na usemi wa mtume (S. A. W) na hilo ndilo waume walitumia. Jinsi tulivyoonyesha sura ya pili, pia alisistiza kuwa dini ya kiislamu inatilia maanani wajibu wa mke kuzihifadhi vitu, haki na pato la mumewe pamoja na kumtumikia ili aweze kutimiza wajibu wake. Katika hali hii mke ana nafasi kubwa katika kuilinda na kuendesha vyema vyumba yake ili mumewe anufaike. Kwa mujibu wa mhojiwa huyu, ikiwa mume atatimiza masharti yote na mke amkosee

basi mume atakuwa na haki ya kumdai mkewe siku ya kiama hata kama ni kutiwa motoni. Sababu hizi za kidini ndizo zilimpelekea Mwana Kupona kutunga kuhusu suala la mke kuenda jehanamu kuamuliwa na mume.

Katika ubeti wa 28, Mwana Kupona anamuusia bintiye namna ya kukaa na mumewe, anasema;

> …Keti nao kwa adabu,
> usimtie ghadhabu,
> akinena si mjibu,
> itahidi kunyamaa…

Anamfahamisha Mwana Hashima umuhimu wa kuwa na adabu kwa mumewe. Anabainisha kuwa adabu hii hujitokeza kupitia namna mke anavyozungumza na mumewe. Kwa kawaida matamshi ya mke yanaweza mletea mumewe fahari au ghadhabu. Kwa hivyo Mwana Kupona anamuonya bintiye asiwe wa kumjibu mumewe kwani akimjibu wakati mwingine huenda akamtia ghadhabu. Hivyo anamuusia ajitahidi kunyamaza hasa mumewe akiwa na hamaki. Hata hivyo jinsi imebainishwa katika sura ya nne, mambo yamebadilika. Chambilecho Uhistoria Mpya, suala la miktadha na utamaduni wa kijamii lazima liangaliwe upya.

### 3.5 Dua

Dua ni sehemu muhimu sana katika jamii ya Waswahili. Dhana hii ina misingi yake katika dini ya kiisalamu ambapo lazima mtu aombe dua kutoka kwa mwenyezi Mungu kabla ya kufanya lolote.

Mwana Kupona alipotunga utenzi huu, anaanza katika ubeti wa 65 kwa kuesema "… Mama haya yasikize tafadhali sinipuze..." Kisha akahitimisha katika ubeti wa 66 kwa kusema kuwa"…Tamati maneno yangu kukusia mwanangu..." Hii inaonyesha kuwa nia yake kuu ilikuwa baada ya kutoa wosia wake ni kumsisitizia binti yake ayashike. Hamu ya kufanya hivi inajitokeza anaposema*:* "…tafadhali sinipuze..." katika ubeti wa 65. Hamu hii ya Mwana Kupona ndiyo inajitokeza katika ubeti wa 68 anapomuomba mwenywezi mungu ayatilie nguvu maneno yake. Kwa hivyo hii ilikuwa dua ya kutia kikomo na kuombea dua wosia.

Mwana kupona anaendeleza maudhui ya dua katika ubeti 70-75. Hapa anawaombea mungu wanawe, nduguze pamoja na jamii ya watu wengine. Kuanzia ubeti wa 70 anawaombea wanawe na nduguze waweze kupata maisha marefu, mema na kuwa watu bora na maarufu. Katika ubeti wa 71 anasema:

> …Rabi waweke nduzangu,
> na wana wa nduzangu,
> wenee na ulimwengu,
> kwa jamala na sitawa…

Kutokana na ukarimu wa moyo wa Mwana Kupona tunaona akiwaombea rehema jamii yote ya miji ya kwao. Hali hii inapatikana katika ubeti wa 72 anaposema "...Na jamii

Islam... " akiwa amelenga jamii yote ya Pwani ambao ni wa dini ya kiislamu. Kulingana na msailiwa M3 aliyehojiwa tarehe 22/11/2016 kaunti ya Nairobi katika Chuo kikuu cha Kenyatta, moyo huu wa ukarimu wa Mwana Kupona wa kupenda na kusaidia wengine ni jambo ambalo mila ya Waswahili ilitilia nguvu. Alisema suala la kuombeana Mungu lilikuwa ni lazima kuombea kila mtu katika jamii na ni moja ya yale ambayo yalifuata ubora wa mila ya wakaazi Waswahili wa Pwani.

Mwana Kupona anamuomba mungu amuondolee ndwee mbovu. Kwa mujibu wa Ndung'o (1985) Mwana Kupona aliugua ugonjwa wa tumbo kutoa damu. Huu huwa ni ugonjwa wa kivimbe katika sehemu ya uzazi.Dua lake kwa mwenyezi Mungu katika ubeti wa 78 anaposema: "…Nondolea ndwee mbovu…" ubeti wa 79: "…nepulia uvukuto…" ubeti 80 "…Unondolee makhafu …" ubeti (85) "…nyingi takalufu..." linaonyesha mawazo ya mashaka, masumbuko na wasiwasi yaliyotokana na ukosefu wa dawa za kuuwa viini vya ndwele kama hiyo iliyokuwa ikiuma ndani na kusababisha kushikwa na homa. Kwa mujibu wa El- Maawy (2011) huu ndio "uvukuto" ambao Mwana Kupona aliomba uondoke.

Kulingana na msailiwa M5 niliyehoji tarehe 12/11/2016 saa nne asubuhi katika eneo la Lamu Magharibi kule Langoni, ugonjwa wa kifua kikuu ndio uliyoitwa "maradhi makhafu" kwa kuwa katika enzi za Mwana Kupona haukuwa na dawa. Watu waliokuwa na ugonjwa huu walitengwa mbali, pia vitu walivyotumia havingekuzwa kamwe. Kwa hivyo, Mwana Kupona kuufananisha ugonjwa wake na "makhafu" ni dhibitisho kuwa ugonjwa huu ulikuwa mbaya. Kutokana na haya mahangaiko akatoa dua katika ubeti wa 87 akisema;

…Ya Rabi nitimiliza,
mabo nisiyoyaweza,
wala moyoni kuwaza,
kwamba yatasikiliya…

Kutokana na ubeti huu ni wazi kwamba Mwana Kupona kama mwanadamu yeyote haikumpita moyoni kwamba magonjwa na misukosuko yangemfika. Dua liliendelezwa na Mwana Kupona hadi ubeti wa 89 na kumalizia ubeti wa 102.

### 3.6 Mke Aliyetimia

Kila wakati huwa na mambo yake. Kwa mujibu wa Durkhem (1897) mtu akitaka kuwa hakimu wa kusema ubaya au wema wa mtu wakati wowote, lazima ajiweke katika nafasi yake kwanza kabla ya kulinganisha na mtu mwingine. El- Maawy (2011) anakubaliana na Durkhem kuwa kufikia karne ya 19 jamii ya Waswahili ilikuwa na mambo yaliyotumika kupimia utu wa mtu. Kwa hivyo, yeyote yule ambaye angetimiza mambo haya angeitwa "mwenye utu." Baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa ni pendo la wazazi na jamaa yote, dini, adabu njema, wema wa mume kwa mke na mke kwa mume. Mwana Kupona katika kumpa, wasia, bintiye, alizingatia haya yote.

Mwana Kupona alibainisha mizani ya kupimia mke mwema. Mizani hizi zimebainishwa kupitia ubeti wa 12, 13 na 14. Mwana kupona anasema:

La kwanza kamata dini… (mk. 12),
Pili uwe na adabu… (mk. 13),
La tatau uwe sadiki… (mk. 14)

Suala la mwanadamu kumtafuta mwenyezi Mungu hutegemea imani yake. Masuala yanayohusu dini ni muhimu sana katika maisha ya mwandamu. Mwanadamu hutumia dini kama nguzo ya imani ya kudhibitisha matumizi yake juu ya nafsi yake. Durkhem (1897) anafafanua kuwa imani huwa na nafasi kubwa kwa mwanadamu. Anaonyesha kuwa katika dini ya Uislamu, Muislamu huwa na ungamano na Mungu na yanapokuwa mazito naye humuachia mwenyezi Mungu na akapata usingizi akalala.

Mtu hufuata dini kwa vitendo vya wema, tabia njema maishani na ibada. Katika ubeti wa 12 Mwana kupona alivitaja vifungu vilivyoikabili zama zake na kwa watu wake, vifungu vyenyewe ni “faradhi” “suna” na “Wajibu” (El- Maawy (2011). Kwa hivyo, kulingana na Mwana Kupona mwanamke hawezi kutimiza kuwa mke ikiwa hashiki dini.

Kuhusu adabu, utovu wa nidhamu katika mwanadamu huonekana kupitia kwa tabia na vitendo ambavyo hubainisha adabu ya mtu mahususi. Mambo haya hubainika kupitia malezi. Mtu anapozungumza au mienendo yake hubainisha malezi mema, ubora wa tabia au elimu. Kupitia shughuli za binadamu za kila siku, ukamilifu au upungufu wa nidhamu ya mtu hubainika. Mwana Kupona anamuusia bintiye kuhusu umuhimu wa kuwa na adabu. Anaonyesha athari ya usemi kwa kufafanua kuwa “...Ulimi wa thawabu, uwe mtu mahabubu…” (ubeti 13)

Suala muhimu la mwisho ni kwamba, bintiye lazima “awe sadiki” ili afuzu kuwa mke mwema. Neno sadiki lina maana ya ukweli, wema, uaminifu, kusadikika, itikadi na udhabiti (El- Maawy 2011). Mwana kupona anamuonya Mwana Hashima kuwa awe mtu wa kupenda ukweli na haki. Hapa kuna ukweli wa kutimiza ahadi na ukweli wa kusema.

Kwa hivyo anamuusia aamini nafsi yake ili adumishe imani na itikadi yake bila kuwazingatia wale wasiopenda haki.

## 3.7 Kiishilio

Sura hii imetalii maudhui katika *Utenzi wa Mwana Kupona.* Tumechunguza na kudhihirisha jinsi mazingira ya mtunzi yalivyochangia katika ubainishaji wa maudhui. Utafiti umeonyesha jinsi masuala ya kijamii, kiuchumi na kihistoria yalichochea na kuchangia katika dhamira na maudhui ya *Utenzi wa Mwana Kupona*. Hivyo, fasihi haistawi wala haikuwi katika ombwe tupu. Kutokana na ukweli huu, imebainika kwamba *Utenzi wa Mwana Kupona* ni kazi ya utunzi wenye uyakini uliofungamana na mazingira, wakati na mfumo wa jamii. Aidha, chanzo cha maudhui ya utenzi huu ni mazingira halisi ya jamii kwa mujibu wa wakati maalum kihistoria.

Ni kutokana na uchunguzi huu ndipo tumeandaa msingi wa kutazama usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kuzingatia wasomaji wa aina mbalimbali. Hiki ndicho kiini cha sura ambata ya nne ambayo kwayo tumechunguza usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona* miongoni mwa wasomaji mbalimbali katika kaunti za Lamu na Nairobi.

## SURA YA NNE

## 4.0 Usomaji na Ufasiri Sasa wa Utenzi wa Mwana Kupona

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia mambo mawili makuu. Jambo la kwanza ni uchunguzi wa usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Katika hali hii tumeanza kwa kuangalia njia za usomaji wa kazi za fasihi, maarifa ya ufasiri na kisha kuchambua ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kurejelea wasomaji mbalimbali. Hii imetokana na kipengele cha Mwitiko wa Msomaji kisemacho kuwa kila matini huwa na wasomaji wa aina mbalimbali. Msomaji wa kukisiwa, lengwa na msomaji bora. Tulichukuwa hatua hii ilikubaini tofauti iliopo baina ya wafasiri hawa wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika mazingira ya sasa.

Pili, sura hii inahusisha uchanganuzi wa data kuhusu maeneo ya utafiti ambayo ni kaunti ya Lamu na Naiorbi. Wasailiwa kutoka katika kaunti hizi teule zilizotafitiwa walipelekea kuibuliwa kwa data ya uchanganuzi. Data hii ilihusisha mwongozo wa maswali kwa wasailiwa katika kaunti zote mbili.

### 4.2 Njia za Usomaji wa Kazi ya Fasihi

Kulingana na Mwitikio wa Msomaji, maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi husika. Fish (1980) anaeleza kuwa kuna njia mbili kuu za usomaji wa kazi za fasihi. Anasema kuna ule usomaji wa kutaka tu kujua kile anachosema mtunzi au kusoma ili kujihamasisha na kujichochea ili kujigundulia mengi.

Baadhi ya wasomaji wa utenzi wa Mwana Kupona walikuwa wasomaji wa juu juu. Kwa mfano, msailiwa mmoja tuliyemhoji tarehe 11/11/2016 eneo la Lamu mjini alituarifu kuwa yeye anaufahamu *Utenzi wa Mwana Kupona* na ameusoma. Hata hivyo anachoelewa tu ni kuwa utenzi huu unatoa wosia kwa mwanamke na unaendelezwa kidini. Kwa hivyo yeye aliusoma tu kwa nia ya kupitisha muda.

Usomaji wa juu juu hutokea pale msomaji hutaka tu kusoma ili kupata yaliyomo katika matini (Simiyu 2016). Katika kubainisha aina ya usomaji kati *Utenzi wa Mwana Kupona*, tulibainisha kwamba wasomaji wengi wa aina hii ni wale waliousoma utenzi huu kwa minajili ya kuupita mtihani shuleni. Hata hivyo, usomaji wa aina hii ni muhimu katika kubainsiha yaliyomo. Usomaji huu unaweza msaidia msomaji kufasiri kazi ya fasihi jinsi apendavyo kwani huwa na muumano na mada jinsi ilivyojitokeza katika ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika sura hii.

Kwa upande mwingine, *Utenzi wa Mwana Kupona* unaweza kusomwa na msomaji kwa njia ambayo inachochea kugundua kwamba mwandishi alikuwa na dhamira ya kumuusia bintiye jinsi ya kuishi na mumewe na jamii. Njia hii ya usomaji hubainishwa kupitia ufasiri wa msomaji ambaye huangazia mtaguzano wake na hali ya maisha na jinsi ilivyo wakati wake na wakati wa mtunzi kwa nia ya kubainisha athari ya mtunzi wakati wake na athari kwa maisha ya msomaji na kwa watu wengine sasa.

Aina hii ya usomaji ilibainika kwa kuzingatia wasomaji waliozingatia ufasiri wao kwa mazingira ya utunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* na mazingira ya sasa. Wasomaji wa

aina hii walifasiri utenzi huu kwa kurejelea mabadiliko ya uchumi, siasa na jamii. Kwa hivyo wasomaji wa aina hii husoma kwa umakini ili kujigundulia na uhakiki.

### 4.3 Maarifa ya Kimsingi na Tajriba ya Msomaji

Kulingana na Mwitikio wa Msomaji, maarifa ya kimsingi na tajriba ambayo msomaji anayo huathiri namna atakavyoifasiri matini husika. Rosenblatt (1969) anaeleza kwamba Mwitikio wa Msomaji huwa unaongozwa na maadili, mielekeo na asili ya msomaji husika bali haitegemei maoni kutokana kwa mwalimu au mwelekezi wake. Hivyo, kazi ile ile inaweza fasiriwa na wasomaji tofauti kwa njia tofauti au ikafasiriwa tofauti na msomaji yule yule mmoja ikiwa ataisoma katika vipindi tofauti vya wakati katika maisha yake.

*Utenzi wa Mwana Kupona* unatalii hali jinsi ilivyokuwa katika zama za Mwana Kupona. Unatuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii ya Uswahilini enzi hizo. Pia unatufunulia jinsi ndoa na dini ya kiisalamu vilivyoathiriana katika mazingira hayo.

Msomaji wa utenzi huu katika mazingira ya sasa atauelewa vyema ikiwa atahusisha tajriba yake ya mambo jinsi yalivyo katika jamii yake. Uhusisnao huu ndio huwawezesha wasomaji kuelewa dhamira na maudhui ya mtunzi. Kwa hivyo, iliwahitaji wasomaji wawe waliusoma utenzi huu kwa jicho pevu ili kubaini ufasiri wa mswala yote muhimu katika utenzi huu na kuyahusisha na hali ya sasa. Kulingana na Simiyu (2016), ufasiri huu wa matini kwa kuzingatia maarifa ya kimsingi na tajriba yake msomaji ndiyo hasa hali ambayo Njogu na Chimera (1999) walisema kuwa ya kuiandika upya matini wakati unayasoma.

### 4.4 Aina ya Wasomaji wa Utenzi wa Mwana Kupona

Kila matini huwa na wasomaji wa aina mbalimbali, hii ni kulingana na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Mwana Kupona alitunga utenzi huu mwaka 1860. Hata hivyo, ingawa alilenga bintiye katika wakati wake, hakukusudia kwamba utenzi huu umfaidi bintiye na wasomaji wa kipindi chake pekee. Maelezo haya yanaafiki mtazamo wa Iser (1978) kuwa kuna aina tatu ya wasomaji, msomaji aliyelengwa msomaji wa kukisiwa na msomaji bora zaidi au wa viwango vyote.

#### 4.4.1 Msomaji wa Kukisiwa

Wakati mwingine kazi ya fasihi huwa haionyeshi uainisho wowote wa msomaji fulani. Wasomaji wakisiwa ni wasomaji ambao usomaji na ufasiri wao ulitokana na msimamo wa Mwana Kupona. Ufasiri wao huambatana au kukubaliana na maoni ya mtunzi. Aghalabu wafasiri ambao ni wasomaji wakisiwa hutoka katika mazingira chipuzi ya mtunzi. Hali hii ilidhihirika katika uchanganuzi wa data ambapo wengi wa wasomaji wakisiwa walikuwa wasailiwa kutoka kaunti ya Lamu ambayo ndiyo mazingira chipuzi ya utenzi utenzi huu. Wasomaji hawa ni wa mrengo wa mwitikio wa msomaji jamilishi. Kulingana na Fish (1980) msomaji wa aina hii hufasiri kazi husika kwa kuegemea mtazamo katika jamii fulani ambayo unatokana na mtazamo wa mtunzi. Kwa mujibu wa Fish mkondo huu hutegemea mila, desturi na utamaduni wa jamii husika. Katika hali hii wasomaji wa kukisiwa huongozwa na mtazamo ambao ulichukuliwa na mtunzi pamoja na mtazamo wa wanajamii katika kufasiri kazi husika.

Kwa vile *Utenzi wa Mwana Kupona* ulitungwa mwaka wa 1860 katika mazingira ya Lamu basi utenzi huu ulilenga binti yake. Mwana Kupona alipotunga kazi hii alikuwa

anatazamia kwamba binti yake angeweza kuoleka karibuni, ambaye baadaye aliolewa na Bwana Aballa Kombo mwaka 1864, kisha kwa Bw. Bakari wa Bwana Madi wa Nyegogo mwaka 1878 baada ya kifo cha Abdalla Kombo (El- Maawy 1978).

Kutokana na tajriba aliyokuwa ameipata katika ndoa, Mwana Kupona alikuwa ameona changamoto katika ndoa na hangependa bintiye ashindwe kuepuka changamoto hizo. Alikuwa na matumaini kuwa Hashima angepata mume hivi karibuni na alikuwa na matarajio makubwa kwa bintiye. Hata hivyo, alifahamu kuwa kutokana na mabadiliko ya wakati huenda kukawa na mkengeuko ambao ungeharibu ndoa za watu. Hali hii inajitokeza katika ubeti wa 65 anapomsisitizia bintiye kuwa amsikize bila kumpuuza ifuatavyo:

…Mama haya yasikize,
tafadhali sinipuze,
utaona nafuuze,
za akhira na duniya…

Mwana Kupona katika kauli ya hapo juu inaonyesha kwamba alikuwa na matumaini makubwa kwamba bintiye ambaye aliwakilisha kizazi cha sasa hangefaulu ndani ya ndoa kama angepuuza na kutofuata wosia wake. Hata hivyo, dalili hizi hazikuwa wazi kwa msomaji wakipindi chake au kwa bintiye. Katika kipindi hiki yale Mwana Kupona alimfahamisha bintiye yalikuwaya kawaida na muhimu kwa mwanamke yeyote aliyekuwa katika ndoa na alitazamiwa kuyazingatia hayo yote. Mwana Kupona alikuwa anamuusia bintiye ambaye alikuwa bado hajaingia katika ndoa bali alikuwa anatarajiwa kuoleka. Kutokana na hali hii mengi ya masuala aliyoyaibua Mwana Kupona kwa bintiye ambaye alikuwa hajaolewa hangeyafahamu wakati huo. Kwa hivyo, wasomaji wa kipindi

hiki ni wa kukisiwa kwa kuwa aliyozungumzia Mwana Kupona yalikuwa kama utabiri kwa bintiye ambaye yangetukia miaka minane baadaye alipooleka, hali ambayo msomaji wa kukisiwa wa 1860 hangeiona na kuifasiri jinsi inavyofasiriwa sasa.

### 4.4.2 Msomaji Aliyelengwa

Kwa mujibu wa Iser (1978) msomaji aliyelengwa ni yule mtunzi alidhamiria. Mtunzi anaweza tunga kulenga vijana, watoto, waze, jinsia fulani, viongozi au watu wazima. Msomaji aliyelengwa na Mwana Kupona ni kijana wa kike ambaye yupo karibu kuolewa ama wa makamo ambaye yumo katika ndoa. Hii inatokana na kauli kuwa utenzi huu ulitungwa na Mwana Kupona alipokuwa anaugua. Alitunga ili kumpa wosia bintiye ambaye alikuwa hajaolewa jinsi yeye kama mwanamke anaweza kuishi na mumewe katika ndoa pamoja na jamii kwa jumla. Kwa hivyo msomaji huyu ni yule ambaye angeshuhudia mambo ambayo Mwana Kupona alikuwa anasema na hivyo angeongozwa na wosia wa Mwana Kupona.

Mwana Hashima Bint Shee Mataka ndiye ametumiwa kuashiria kuwa utenzi huu ulilenga vijana wa kike. Kwa kuwa masuala haya katika utenzi wa Mwana Kupona yanaathiri ndoa nyingi katika jamii ya sasa, basi wasomaji wote wa kike ambao ni vijana na wa makamo wa utenzi huu ni wasomaji walengwa. Ingawa alilenga wanawake wa jamii ya Uswahilini kwa kuzingatia dini ya kiislamu, kutokana na maingiliano ya jamii kupitia ndoa, biashara na elimu. Wasomaji walengwa ni wale wanawake wote ambao wameusoma hata kama sio kwa Kiislamu wala hawatoki Pwani ya Kenya.

### 4.4.3 Msomaji wa Kiwango Bora Zaidi

Msomaji wa aina hii huwa ni wa viwango vyote na anaweza kuifafanua na kuifasiri kazi ya fasihi kwa undani. Foster (2003) anamfafanua msomaji huyu kama wa kiwango cha juu na ambaye ana uwezo mkubwa wa kufasiri kazi ya fasihi. Msomaji huyu huweza kuhusisha mtaguzano wake na mambo anayoyajua na maelezo yotolewayo katika matini. Kwa mujibu wa Iser (1978), msomaji huyu huwa ni wa viwango vyote na anaweza kuhusisha kazi ya fasihi na uhalisia wa mambo katika mazingira ya wakati anamoishi. Kwa hivyo, wasailiwa ambao wamefasiri utenzi huu kwa kuzingatia mazingira ya sasa kwa pamoja na uhalisia uliopo na kuufananisha na zama za Mwana Kupona. Hii ina maana kuwa msomaji wa aina hii hana athari ya mazingira chipuzi.

Wasailiwa wengi waliochukua mkondo huu walikuwa wasomi kama vile wahadhiri na wanafunzi wa vyuo ambao wamekulia nje ya mazingira ya Uswahilini. Jinsi imebainishwa katika uchanganuzi wa data, asilimia kubwa ya wasomaji hawa ilitokana na data ya kaunti ya Nairobi.

## 4.5 Ufasiri Sasa wa Utenzi wa Mwana Kupona

### 4.5.1 Kuhusu Wajibu wa Mke kwa Mumewe

Msomaji mmoja wa kuakisiwa M2 kutoka eneo la Shela kule Lamu ambaye pia ni ustadhi alieleza kuwa ndoa nyingi zinaendelea kuvunjika sasa kutokana na wanawake kutojua wajibu wao kwa waume zao. Alisema kuwa mwanamke popote aendapo yuko chini ya mumewe. Alibainisha kwamba (S. A. W) alisema kuwa ili mke apate nafasi peponi lazima amtii mumewe. Kwa hivyo, wosia ya Mwana Kupona kwa bintiye kuwa

amtii mumewe ni sheria chini ya dini ya Kiislamu. Anaunga mkono wosia huu kwa kusema kuwa Mwana Kupona alikuwa na maana kwamba binyiye afuate amri zote za mumewe kwa mujibu wa dini. Hata hivyo alibainisha kuwa mwanamke hafai kutii amri za mumewe ikiwa amri hizo ziko kinyume na dini. Amri hizi za mumewe hata kama hazimridhishi mke atalazimika kuzifuata ili kumfurahisha mumewe na kuboresha ndoa bora zisikinzane na dini.

Wasomaji bora zaidi pia walinifahamisha kuwa jambo liwe baya au zuri lazima mwanamke amtii mumewe. Walibainisha kuwa Mwana Kupona kusema kuwa bintiye amtii mumewe alimaanisha kuwa amsikize katika hali zote. Walibainisha kuwa mwamume sio mtu wa kufokea. Wasomaji bora zaidi walibainisha kuwa ingawa katika ndoa hapakosi mafarakano, ndoa husimama tu ikiwa mke atamtii mumwe kwa vyovyote vile.

Suala la mke kumtii mumewe ni muhimu. Wasomaji lengwa (vijana wa kike) walisema kuwa ili kudumisha heshima na uelewano hasa katika ndoa lazima mke amtii mumewe na vivyo hivyo  mume amtii mkewe. Hawakukubaliana na wosia kuwa mke amtii mumewe kwa vyovyote vile. Walisema kuwa katika jamii ya sasa, mke hafai kumtii mumewe kwa mambo ambayo yatamdhalalisha, kumnyanyasa au kumtesa.Walibainisha kuwa mke azingatie tu mambo ambayo yataendeleza uhusiano wao na kujenga jamii. Ilibainika kwamba mambo yamebaidilika kiuchumi, kihistoria na kijamii. Kwa hivyo walionyesha kuwa mwanamke ana ruhusa ya kutotii mumewe kuhusu mambo kadhaa kama vile: mume kumtaka mke akae tu nyumbani bila kufanya kazi na kuendeleza utegemezi. Kwa mujibu wa wasomaji lengwa, suala kama hili linageuka haki zao na kuwagandamiza

kwani wanachukulia kuwa mwanamke ni nguzo ya uchumi wa jamii na ana haki ya kufanya kazi sawa na mumweze.

Kuhusu suala la mwanamke kumyoa na kumfukiza udi, wasomaji wakisiwa walisema suala hili ni muhimu katika jamii ya Waswahili. Walifafanua kuwa ni jambo muhimu katika furaha ya ndoa ya Waswahili. Walibainisha kuwa mwanamke ndiye kioo cha mwanamume. Walichukulia wosia wa Mwana Kupona kwa bintiye kuwa alikuwa na maana kwamba usafi wa mumewe utategemea mkewe. Kwa hivyo, mumewe atapimwa na jamii kutokana na mkewe. Katika dini ya Kiislamu, kila muislamu anafaa kulinda usafi wake. Hata hivyo wasomaji wakisiwa walibainisha kuwa ni fahari kwa mke kuwa amechangia katika usafi wa mumewe. Kulingana na mafundisho ya dini ya Kiislamu, watu wanapoenda msikitini Ijumaa kusali lazima wawe safi. Kwa hivyo, Mwanamume anapoenda msikitini na ndevu ambazo hazijanyolewa na kanzu chafu basi lawama huwa kwa mkewe. Kwa hivyo Mwana Kupona alifahamu kuwa usafi ni muhimu na bintiye angefahamika vyema katika jamii ikiwa angemshughulikia mumewe kwa kumfukiza udi na kumnyoa ndevu ili kuimarisha usafi wake anapotangamana na watu katika jamii.

Kwa upande mwingine, wasomaji bora zaidi na wasomaji lengwa walikuwa na fasiri tofauti. Kulingana nao, suala la kumnyoa ndevu na kumfukiza udi mumewe halina nafasi katika jamii ya sasa. Hali hii inatokana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi. Kwa mujibu wa wasomaji lengwa wanawake wa sasa wana majukumu mengi sawa na wanaume. Wanawake pia huenda kazini ili kujiendeleza kiuchumi. Kwa hivyo, wanaporudi nyumbani huwa kazi za nyumba zimewangoja na hivyo hawana nafasi au wakati wa kufukiza udi na kumnyoa mume ndevu. Wanasema kuwa kwa sasa kuna

mabadiliko ya kiteknolojia ambapo kuna mashine za kunyoa ambapo mume anawezaenda kinyozi na anyoa ndevu. Aidha, kwa sasa kuna manukato ya aina mbalimbali ambayo mume anaweza kujipuliza yeye mwenyewe. Kwa hivyo wanaona wosia huu wa Mwana Kupona kama uliopitwa na wakati hata kama unadumishwa na wachache katika eneo la Pwani.

Wasomaji lengwa walibainisha kuwa mambo kama haya kufukiza udi na kunyoa wanaume ndevu katika jamii ya sasa yanaendeleza ubabadume na taasubi ya kiume dhidi ya wanawake. Wanasema hali ya kumnyoa mume ndevu na kumfukiza udi ilikuwa sawa katika zama za Mwana Kupona tofauti na sasa ambapo wanasema mwanamume ana wajibu wa kuchunguza usafi wa mwili wake kibinafsi na kuudumisha.

Mwana Kupona katika ubeti wa 30 anamuusia bintiye amuage vizuri na kumpokea kwa furaha mumewe anaporejea. Kulingana na El- Maawy (2011) kuagana huathiri moyo wa wawili wanaoagana; hubakisha akilini ungamano la mawazo linalozagaa moyoni na kumhisi karibu aliye mbali.

Wasomaaji wakisiwa walibainisha kuwa Mwana Kupona aliposema "…akitoka agana naye…" alimaanisha kuwa kule kuagana ni kujua mipango ya mume ya siku nzima na kumfanya mume auhisi ulatifu wa mukewe na kushughulika kwake kwa yanayompendeza mumewe.

Aidha katika ubeti wa 30 Mwana Kupona anasema, "…kiingia mkongowee…"Kulingana na msailiwa mmoja, Kumkongowea ni kumkaribisha kwa furaha. Kulingana na wasomaji wakisiwa hali hii ya kumkaribisha mume kwa furaha ni kumuonyesha kuwa mke alikuwa

na hamu na yeye kurudi. Wasomaji walengwa walibainisha kuwa kumkaribisha kwa furaha katika mazingira ya sasa kuna maana kumtandikia mume, kumpa maji baridi au kinywaji cha kuburudisha cha kusisimua pamoja, na kumpiga pambaja.

### 4.5.2 Kuhusu Mwenendo wa Mwanamke Aliyeolewa

Katika ubeti wa 44, Mwana Kupona anamuusia bintiye asitoke bila ya kupata ruhusu ya mumwe. Kutokana na msailiwa M10 niliyemhoji tarehe 23/11/2016 katika Chuo Kikuu cha Nairobi, suala la mke kutoka baada ya ruhusa ya mumewe ni amri ya dini ya Kiislamu. Kulingana na muhojiwa huyu, kidini mwanamke yeyote aondokaye nyumbani bila idhini ya mumewe hupata laana kutoka kwa malaika katika kila guu au hatua anayopiga anapotembea. Mhojiwa huyu ambaye alikuwa mmoja wa wasomaji wakisiwa alibainisha kuwa ingawa wakati wa sasa wanawake wanafanya kazi, ni lazima kuwepo masikizano. Ikiwa mwanamke amepata la dharura na angependa kutoka, na mume wake hayupo basi ni vyema apige simu kumfahamisha kuwa anaondoka.

Wasomaji lengwa walipinga wosia huu wa kupata idhini kutoka kwa mume kabla ya kutoka. Wanaona kuwa mke sawa na mume wana haki ya kutoka kwa shughuli za kibinafsi kama vile kuwatembelea marafiki, makundi ya murungi na hata kuenda klabuni. Kwa mujibu wa Bell (1985) ingawa wanawake wengine huomba ruhusa ili kutembelea sehemu hizi, waume zao hukataa na hivyo kusababisha wanawake hawa kuondoka wakati waume zao wameondoka. Hali hii imepelekea kutokuwepo uaminifu na kuvunjika kwa ndoa nyingi.

Kulingana na wasomaji bora zaidi, katika enzi za sasa hakuna haja ya kumpinga mkeo kuondoka ikiwa ameomba idhini. Walibainisha umuhimu wa idhini kwani huenda jambo likampata mke kule nje na mume asifahamu alikokwenda. Walibainisha kwamba mambo mengi yamebadilika, mambo haya hayakuwepo wakati wa Mwana Kupona. Mwanamke katika enzi zake Mwana Kupona angekubaliwa tu kutoka kwa matembezi, sherehe au msiba (El. Maawy 2011).

Kulingana na dini ya Kiislamu, mwanamke kugombana na mumewe si ishara nzuri. Mwanamke hafai kumpigia mumewe kelele watoto na jirani wasikie. Kwa mujibu wa kurani tukufu, ikiwa kuna shida baina ya mke na mume na wameshindwa kutatua basi mke na mume waite familia zao ili wajadiliane kwa nia ya kupata suluhu. Mwanamke kumgombanisha au kumfokea mumewe ni dalili au ishara ya mke ambaye si mzuri. Kwa hivyo, Mwana Kupona alikuwa amebainisha umuhimu wa bintiye kutojibizana na mumewe. Wasomaji bora zaidi walieleza kuwa hali ya kujibizana baina ya mke na mume ndio imesababisha kuvunjika kwa ndoa. Walibainisha kuwa mume anapokuwa nyumbani hutaka mke awe mkarimu bila ya kujibizana naye. Hata hivyo, mwanamume anapojibizana na mke huwa hakuna amani pale nyumbani na hivyo kuanza kutafuta mahali atapata amani. Katika hali hii, mume hujipata ametoka na kupata mke mwingine na hivyo kuzua msukosuko katika ndoa yao.

Ingawa dini ya Kiislamu inabainisha kuwa kila binadamu yu sawa na mwenzake, wasomaji wakisiwa kutoka Lamu walibainisha kuwa usawa upo katika mambo machache tu. Ilibainishwa kuwa haiwezi kamwe kubadilishwa eti mume awe na haki sawa na mke kwa maana hiyo ni mipango ya Mungu. Mmoja wa wasomaji hawa alieleza kuwa

wanaume wa Kiislamu kihaki wako mbele kuliko wanawake na hivyo mwanamke hana ruhusa ya kutaka haki sawa na mumwe. Kwa mfano, ilisemekana katika dini ya Kiislamu, mwanamke hawezi kupata uridhi zaidi ya mumewe. Hata hivyo, Momanyi (1998) anabainisha kwamba haki ambazo wanaume wanadai kuwa nazo zaidi ya wake hazitokani na dini bali zinatokana na utamaduni ambao uliingizwa katika jamii ya Waswahili na waarabu ambao huchukulia kuwa nafasi ya mke ni nyumbani. Kwa hivyo kulingana na maoni yake, Momanyi anasema wanaume Waswahili walikopa itikadi hii ya uarabuni na kutumia dini kama kigezo cha kuihalalisha.

Joinet (1997) anaeleza kuwa swala la demokrasia na uhuru limekita katika kila sehemu ya maisha ndoa ikiwemo. Kwa hivyo anaonyesha kuwa watu wa sasa wanataka kuwa na sauti katika maamuzi yote yanayowahusu. Wasomaji lengwa ambao ni wanawake wa makamo na vijana walipinga hali ya Mwana Kupona kutaka bintiye asiwe na haki sawa. Kundi hili lilidai kwamba wanawake wajikomboe na wafanye mageuzi miongoni mwao dhidi ya makucha ya waume zao kwa kupigania haki zao. Maoni haya ya wasomaji lengwa yanaoana na maoni ya Nyenyembe (1997) kuwa wanawake wa sasa hawavumilii taasubi ya kiume wala udunishwaji wowote.

Hali ya mkinzano baina ya wanawake na wanaume katika jamii ya sasa ndiyo ilimpelekea Robert (1967) kusema kwamba kuna haja ya watu kubadili mielekeo kuhusu ndoa na wanawake ili kuwa razini na maendleo ya jamii. Kwa kuzingatia kipengele cha haki za wanawake, maoni ya Shabaan Robert yanashabihiana na wasomaji lengwa kuwa wanawake ni wanyonge na hawafai haki sawa na wanaume yanafaa kuondolewa katika jamii kwani yalipandikizwa na mila na desturi kongwe. Hivyo, inasisistizwa kwamba

wanawake wana haki sawa na wanaume. Ufasiri huu wa wasomaji lengwa unatokana na kipengele cha Mwitikio wa Msomaji kisemacho kuwa usomaji ni tendo ambalo hufanyika na kutekelezwa wakati maalum ambapo ufasiri unaotokana na usomaji huo huathiriwa na mazingira ya wakati husika.

Masinde (2003) anabainisha kuwa haki ya mume na mke haina budi kupimwa katika mizani ili kila mmoja wao apewe anachostahiki. Wanaume hufanya mambo mengi mabaya kwa wake zao ambayo huacha alama kwa mawazo ya wake zao. Hivyo haifai kumlaani mwanamke tu bila kuzingatia matendo ya mumewe.

Mmoja wa wasailiwa ambaye ni msomaji bora zaidi akirejelea suala la mwanamke kutaka haki sawa na mwanamume, alitilia mkazo kuwa baadhi ya wanaume hutoka na kupiga hodi kwa milango ya wanawake wengine. Kutokana na hali hii ilibainisha kwamba wanaume wa aina hii wasipigwe na mshangao wakiona wake zao wakipigiwa hodi na waume. Hali hii inashabihiana na usemi wa mmoja wa wasomaji lengwa kuwa: "Hakuna haja mke kutii sheria za mume ambazo mume mwenyewe hazifuati." Msomaji huyu kutoka kaunti ya Nairobi alitaja usemi huu kama kilio cha haki ya usawa baina ya wake. Alibainisha kuwa wanawake hawastahili kuonewa na kukandamizwa bila sababu. Ilibainishwa kuwa yaliyosemwa na Mwana Kupona kwa bintiye yalikuwa ya zama za kale na yamepitwa na wakati. Hivyo, ni vyema mke na mume wachukuliane kwa haki, usawa na upendo.

Msimamo wa wasomaji lengwa kuhusu haki za mke ndio Newton (1990), anasema unatingiza itikadi za msimamo batili na kusababisha mabadiliko katika muktadha wa

sasa. Hali hii inawiana na Uhistoria Mpya kwamba utamaduni hauna budi kufafanuliwa upya kulingana na mazingira na wakati.

## 4.6 Uchanganuzi wa Data Katika Kaunti ya Lamu na Nairobi

### 4.6.1 Utangulizi

Data iliyoibuliwa katika utafiti huu kwa minajili ya uchanganuzi ilihusisha mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya na Mwitikio wa Msomaji. Data tuliyoipata ilijumuisha usaili wa wasomaji wakisiwa, wasomaji lengwa na wasomaji bora zaidi kupitia kwa mwongozo wa maswali ulioandaliwa kimbele na kimakusudi na mtafiti. Wasailiwa waliohusika walitoka sehemu teule ambazo ni kaunti ya Lamu na Kaunti ya Nairobi. Mtindo uliotumiwa katika uchanganuzi wa data hii ni mtindo wa uchanganuzi wa tarakilishi wa uchanganuzi wa tarakimu sayansi za jamii. Mtindo huu hutumiwa kuchunguza kategoria za uchanganuzi na kutathmini idadi ya wasailiwa pamoja na asilimia matukio na asilimia jumla.

### 4.6.2 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Lamu

| | Idadi marudio | Asilimia | Asilimia Limbikizi |
|---|---|---|---|
| WasomajiWakisiwa | 12 | 60.0 | 60.0 |
| Wasomaji Lengwa | 06 | 30.0 | 90.0 |
| Wasomaji bora zaidi | 02 | 10.0 | 100.0 |
| Jumla | 20 | 100.0 | 100.0 |

Kiwango hiki cha uchanganuzi kilikusudia kutathmini usomaji na ufasiri wa Utenzi wa *Mwana Kupona* katika kaunti ya Lamu. Asilimia sitini ya wasailiwa walikuwa wasomaji wakisiwa. Wasomaji hawa walifasiri utenzi huu kwa kuunga kikamilifu wosia wa *Mwana Kupona*. Asilimia thelathini ya wasailiwa kutoka Lamu walikuwa Wasomaji Lengwa. Hawa walikuwa wanawake ambao ni vijana na wa umri wa makamo ambao ufasiri wao ulichukulia kuwa wosia wa *Mwana Kupona* umepitwa na wakati kutokana na mabadiliko ya kisissa, kijamii na kiuchumi.

Asilimia kumi ya wasailiwa walibanika kuwa wasomaji bora zaidi ambao waliunga na wakati huo huo kuupinga. Wasomaji wakisiwa walikuwa na asilimia ya juu zaidi katika kaunti ya Lamu kwa kuwa ndio mazingira chipuzi ya utenzi huu na hivyo wengi wa wasailiwa hawa waliunga mkono utenzi huu kwa kuwa unatokana na mazingira yao

**4.6.3 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Nairobi**

| | Idadi Marudio | Asilimia | Asilimia Limbikizi |
|---|---|---|---|
| Wasomaji Wakisiwa | 03 | 15.0 | 15.0 |
| Wasomaji Lengwa | 06 | 30.0 | 45.0 |
| Wasomaji bora zaidi | 11 | 55.0 | 100.0 |
| Jumla | 20 | 100.0 | 100.0 |

Kama inavyodhihirika kutokana na jedhali hili, asilimia kumi na tano ya wasailiwa walikuwa wasomaji wakisiwa. Asilimia thelathini walikuwa wasomaji lengwa. Asilimia kumi na moja walikuwa wasomaji bora zaidi. Ilijidhihirisha kwamba asilimia kubwa ya wasomaji hawa waliusoma utenzi huu kwa minajili ya kufanya mitihani chuoni au kufunza. Kutokana na hali hii waliufasiri kwa kuainisha mazingira ya zama za *Mwana Kupona* na zama za sasa. Kwa hivyo, ufasiri wao uliegemea kuunga mkono vipengele kadhaa kama vile mwanamke kutii mumewe na kupinga vipengele vingine ambavyo walidai haviwezi kamwe kukubalika katika mazingira ya sasa. Asilimia kubwa ya wasailiwa walikuwa wasomaji bora zaidi kutokana na hali kuwa wengi wao waliusoma utenzi huu Chuoni kwa nia ya kupita mtihani au kuuhakiki.

#### 4.6.4 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Lamu na Nairobi kwa Ujumla

| | Idadi marudio | Asilimia | Asilimia Limbikizi |
|---|---|---|---|
| Wasomaji Wakisiwa | 15 | 37.50 | 37.50 |
| Wasomaji Lengwa | 12 | 30.0 | 67.50 |
| Wasomaji bora zaidi | 13 | 32.50 | 100.0 |
| Jumla | 40 | 100.0 | 100.0 |

Jumla ya wasailiwa arobaini walihojiwa. Asilimia thelathini na saba nukta tano walikuwa wasomaji wakisiwa. Asilimia thelathini walidhihirisha kuwa wasomaji lengwa na asilimia thelathini na mbili nukta tano ya jumla ya wasailiwa walikuwa wasomaji bora zaidi.

### 4.6.5 Aina ya Wasomaji Katika Kaunti ya Lamu na Nairobi Kulingana na Jinsia

Kigezo hiki kililenga kubainisha aina ya wasomaji wa kike na wa kiume katika kaunti ya Lamu na Nairobi.

#### 4.6.5.1 Wanawake

| | Idadi marudio | Asilimia | Asilimia Limbikizi |
|---|---|---|---|
| Wasomaji Wakisiwa | 04 | 20.0 | 20.0 |
| Wasomaji Lengwa | 12 | 60.0 | 80.0 |
| Wasomaji bora zaidi | 04 | 20.0 | 100.0 |
| Jumla | 20 | 100.0 | 100.00 |

Hapa tuliwahoji jumla ya wasailiwa ishirini kutoka kaunti zote mbili (Lamu na Nairobi). Asilimia ishirini ya wasailiwa wa kike walikuwa wakisiwa. Asilimia sitini ya jumla ya wasailiwa walikuwa wasomaji lengwa. Wasomaji lengwa walidhihirisha kuwa

mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika mazingira ya sasa ndio chanzo cha wao kutokubaliana na wosia wa Mwana Kupona. Wasomaji bora zaidi walichukua asilimia ishirini ya jumla ya wasailiwa wa kike. Wasomaji lengwa walichukua asilimia kubwa kwa kuwa wote walikuwa vijana wa kike ambao Mwana Kupona alidhamiria alipotunga utenzi huu.

**4.6.5.2 Wanaume**

| | Idadi marudio | Asilimia | Asilimia Limbikizi |
|---|---|---|---|
| Wasomaji Wakisiwa | 15 | 75.0 | 75 |
| Wasomaji Lengwa | - | 00.0 | - |
| Wasomaji bora zaidi | 05 | 25.0 | 100 |
| Jumla | 20 | 100.0 | 100 |

Kiini cha data hii kilikuwa kuchunguza aina ya wasomaji wa kiume na ufasiri wao. Asilimia sabini na tano ya wasailiwa walikuwa wasomaji wakisiwa. Wasomaji hawa walidhihirisha kuwa utenzi wa *Mwana Kupona* ni utenzi wenye manufaa. Walishikilia kwamba wosia wa *Mwana Kupona* ni kielelezo bora cha mwanamke wa sasa.

Hapa, hakukuwa na wasomaji lengwa kwa kuwa tuliwalenga wasailiwa wa jinsia ya kiume pekee. Kiwango cha asilimia ishirini na tano ya wasailiwa wanaume walikuwa wasomaji bora zaidi.

## 4.6 Kiishilio

Sura hii imechunguza usomaji na ufasiri wa Utenzi wa *Mwana Kupona* kwa kuzingatia aina ya wasomaji katika kaunti ya Lamu na Nairobi. Uchunguzi huu ulitokana na uchanganuzi wa data ya utafiti huu iliyokusanywa kutoka kaunti hizo mbili ambazo zilikuwa maeneo ya utafiti huu. Data hiyo ilihusu kipengele kimoja maalum; mwongozo wa maswali. Kutokana na uchanganuzi huu, ilibainika kuwa asilimia kubwa ya wasailiwa wa kiume walikuwa wasomaji wakisiwa. Wasomaji hawa waliunga kikamilifu utenzi wa Mwana Kupona kwa madai kuwa mwanamke anayetenda kinyume na wosia wa Mwana Kupona atakuwa anaenda kinyume na maadili ya Kiafrika. Hali hii ililihitilafiana na wasomaji lengwa ambao ni vijana wa kike waliouona utenzi huu kama uliopitwa na wakati.

Tumetalii na kufafanua kila kigezo cha uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Pia, data hii ilitusaidia kubainisha aina mbalimbali za wasomaji na ufasiri wao sasa. Sura inayofuata ya tano ndiyo itakayokuwa ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii ilijikita katika kufafanua na kuyatolea maelezo masuala yanayohusu matokeo, changamoto na mapendekezo ya utafiti.

## SURA YA TANO

## Muhtasari, Matokeo na Mapendekezo

### 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti huu. Aidha, imeshughulikia matokeo ya utafiti ambayo yalitokana na uchanganuzi wa data iliyokusanywa na matokeo kuwasilishwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Mbali na haya, sura hii imeyaeleza matatizo ambayo mtafiti alikumbana nayo, pamoja na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

### 5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulichunguza usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Utafiti uliongozwa na malengo matatu ya utafiti. Kwanza, utafiti ulilenga kubainisha mazingira yaliyochipuza *Utenzi wa Mwana Kupona* na usomaji wake sasa. Pili, utafiti ulidhamiria kueleza maudhui ambayo yanajitokeza katika *Utenzi wa Mwana Kupona*. Lengo la tatu lilihusu kueleza usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Nadharia changamano iliyohulutisha misingi ya nadharia ya Uhistoria Mpya na Mwitikio wa Msomaji ilitumika katiwa ubainishaji na uelezaji wa usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Utafiti huu umeyatekeleza malengo yake kupitia sura tano za tasnifu.

Sura ya kwanza imefafanua msingi wa utafiti. Sura hii iliangazia usuli wa utafiti ambao uliuwekea msingi utafiti huu kwa kuonyesha nafasi ya msomaji katika ufasiri wa kazi za fasihi. Pia ilionyesha nafasi ya mabadiliko ya mazingira kiuchumi, kijamii na kisiasa

katika usomaji na ufasiri wa kazi za fasihi. Aidha ilibainisha athari ya mazingira kwa mtunzi katika uwasilishaji wa maudhui ya kazi yoyote ya kifasihi. Isitoshe, sura hii ilijadili suala la utafiti, masuali ya utafiti na sababu zilizopelekea mada hii kuchaguliwa. Aidha, sura hii ilijadili upeo na mipaka ya utafiti. Vilevile yaliyoandikwa kuhusu mada yamejadiliwa ili kubainisha mchango na nafasi ya kazi ambazo zimetajwa katika utafiti huu.

Sura hii ya kwanza pia imejadili nadharia ambayo ilitumiwa kuuongoza utafiti huu. Nadharia yenyewe ni ya Uhistoria Mpya na Mwitikio wa Msomaji. Utafiti uliangazia waasisi wa nadharia hizi mbili na kuonyesha mihimili muhimu ya nadharia hizi zilizoufaa utafiti. Hali kadhalika, sura hii ilijadili mbinu za utafiti ambazo zilijumuisha usomaji wa maktabani na utafiti nyanjani. Pia, kitengo cha sampuli na uteuzi wa sampuli kilijadiliwa katika sura hii.

Sura ya pili ilichunguza mazingira ya *Utenzi wa Mwana Kupona* na usomaji sasa kwa lengo la kubainisha nafasi ya mazingira ya wakati wa utunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika utenzi huu. Pia iliangalia historia ya Mwana Kupona Bint Mshamu ambayo ilihusu wazazi wa Mwana Kupona, kuzaliwa kwa Mwana Kupona na kuolewa kwake. Sura hii pia imejadili itikadi na imani ya mwanamke Mswahili wa Kiislamu pamoja na ufafanuzi wa mazingira ya wasomaji wa sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona.*

Sura ya tatu ilijadili maudhui katika *Utenzi wa Mwana Kupona*. Maudhui ya utegemezi, utangamano, mausio ya mke bora, maudhui ya dua na maudhui ya mke aliyetimia yalifafanuliwa. Maudhui haya yalibainishwa kwa kuzingatia muktadha na mazingira ya

mtunzi ili kuwezesha kueleza athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Sura ya nne ilishughulikia uchanganuzi wa data iliyokusanywa kutoka eneo la kaunti za Nairobi na Lamu kuhusu usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kuzingatia wasomaji wa aina mbalimbali. Sura hii pia ilijadili njia za usomaji wa kazi ya fasihi, maarifa ya kimsingi na tajriba ya msomaji, aina ya wasomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona* na jinsi wanavyoufasiri utenzi huu. Uchanganuzi wa data ya utafiti huu ulifanywa kwa mtindo wa tarakilishi ujulikanao kama mtindo wa uchanganuzi tarakimu sayansi za jamii pamoja na wa kimaelezo.

Katika sura ya tano ambayo ndiyo ya mwisho, utafiti uliangalia muhtasari wa kila sura ya utafiti huu na matokeo ya utafiti kwa kina. Katika kuangazia matokeo, kila lengo la utafiti lilichunguzwa na kukadiriwa iwapo lilitimizwa. Aidha sura hii ilijadili changamoto za utafiti huu na mapendekezo ya utafiti zaidi.

### 5.2 Matokeo ya Utafiti

Kutokana na uchanganuzi wa data zilizotokana na aina mbalimbali ya wasomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona*, imebainika kwamba usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika mazingira ya sasa umebadilika. Mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ndicho chanzo cha mabadiliko haya. Mabadiliko haya yanatokana na kipengele cha nadharia ya Mwitikio wa Msomaji kuwa maarifa ya kimsingi na tajriba ambayo msomaji anayo katika mazingira husika huathiri usomaji na ufasiri wa kazi husika.

Utafiti huu uligundua kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kiwango kikubwa ni zao la amali za mazingira ya wakati wake. Utunzi huu ni kielelezo kinachotoa ushahidi wa itikadi na mwenendo wa kijamii, kidini, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Ni kielelezo kinachoonyesha uwiano baina ya muktadha mzima wa jamii ya wakati wake Mwana Kupona na sekta hizo. Kutokana na uchanganuzi huu, itikadi ya mtunzi imebainika. Itikadi hii imebainika katika wasomaji wakisiwa wa mazingira ya sasa.

Utafiti huu uligundua ya kwamba tukio la mwanamke katika mazingira ya sasa limebadilika, na hivyo limeathiri sera ya maisha katika jamii ya sasa. Imebainika kwamba wanawake wameendelea kuwa na msisimko mkubwa ambapo sasa wanapigania nafasi zao katika jamii. Wanadai haki sawa na wanaume katika nyanja mbalimbali za maisha ya jamii na maendeleo. Kutokana na hali hii, mielekeo ya wanajamii wengi imebadilika ili kuakisi maendeleo ya jamii. Maendeleo haya yamepelekea jamii ya sasa kupata ufafanuzi mpya kuhusu ndoa ili kuafikiana na maendeleo ya kijumuia. Matukio haya ni ya kijamii na kihistoria na hivyo yaliathiri usomaji na ufasiri wa *Utenzi Mwana Kupona*.

Aidha fasihi hutoa mdundo ambao una misingi yake katika jamii. Hali hii inatokana na ukweli kuwa fasihi ina uhai (Masinde 2003). Aghalabu fasihi huelekezwa na msukumo na nguvu za historia ya jamii. Kwa hivyo, athari mbalimbali za kimaudhui na kifani katika *Utenzi wa Mwana Kupona* zilitokana na mazingira ya mtunzi. Mazingira haya yalijumuisha vitu, watu na mawazo yao pamoja na hali ya maisha kwa jumla.

Kupitia kwa taarifa hizi, tunapata mwanga kumhusu mtunzi wa Mwana Kupona pamoja na mazingira yake. Kadhalika utafiti umetuongezea maarifa zaidi kuhusu ubunifu wake

hasa chanzo cha utunzi wake. Pia utafiti umeweza kuonyesha kuwa Mwana Kupona aliweza kuathiriwa na mafunzo ya kidini katika utunzi wake. Kupitia maoni ya wasomaji wakisiwa, ilibainika kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* sawa na *Utenzi wa Shufaka, Utenzi wa Inkisafi* na *Utenzi wa Miraji* unaakisi mafunzo anuai yaliyomo katika Kurani. Aidha ugunduzi huu umezingatia mwelekeo kwamba *Utenzi wa Mwana Kupona* umesheheni maudhui ya dini ya Kiislamu. Ufafanuzi huu unabainisha kuwa ili kuelewa chimbuko na ufasiri wa utenzi huu, ni bora kufahamu maadili ya dini ya Kiislamu yaliyomkuza mtunzi katika mazingira ya utunzi.

Imebainika kwamba chanzo cha maudhui ya *Utenzi wa Mwana Kupona* ni mazingira halisi ya jamii kwa mujibu wa wakati maalum kihistoria. Nadharia mojawapo (Uhistoria Mpya) iliyouongoza utafiti huu inashikilia kwamba kazi ya mwandishi haina budi kukita katika matukio mbalimbali ya jamii kulingana na wakati. Ilibainika kwamba Mwana Kupona kama msanii mwanajamii hakuwa na budi ya kutunga utenzi huu kutokana na tajriba aliyoipata katika jamii yake. Utafiti ulipata kwamba maudhui ya utegemezi, utangamano, mausio ya mke bora, dua na maudhui ya mke aliyetimia yalitokana na mazingira na itikadi ya jamii ya Mwana Kupona.

Kuchunguza hali halisi za kisiasa, kiitikadi, kiuchumi, kimaendeleo na kitamaduni katika vipindi tofauti vya kihistoria katika mazingira ya mtunzi husaidia kuelewa uhusiano baina ya mazingira ya msanii na maudhui. Ilibainika kuwa mifumo iliyokuwepo wakati wa utunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* ilimwathiri Mwana Kupona katika utunzi wake kimaudhui na kifani kwa sababu ya uyakini ambao unafungamana na mazingira, wakati na mfumo wa jamii. Kwa hivyo, chimbuko la maudhui katika *Utenzi wa Mwana Kupona*

ni mazingira halisi ya jamii kulingana na wakati maalum. Imani ya Mwana Kupona ya dini pia iliathiri pakubwa mwelekeo wake kifalsafa.

Utafiti huu unaonyesha kwamba ni muhimu kuchunguza mabadiliko ya mawazo kupitia Mwitikio wa Msomaji au usomaji na ufasiri na jinsi mawazo hayo yanavyopata athari na kudhibitiwa na nguvu changamano za sasa zilizoko na jamii ya wakati wake. Katika hali hii, mabadiliko katika ufasiri wa kazi husika ya fasihi yatachukuliwa kama ukuaji wa mawazo ili kuyakabili mazingira ya wakati wa sasa.

Kutokana na data iliyohusisha mwongozo wa maswali kwa wasailiwa kutoka kaunti ya Lamu na Nairobi, ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona* kutokana na wasomaji mbalimbali ulibainishwa. Wasomaji wa *Utenzi wa Mwana Kupona* waliobainishwa ni pamoja na wasomaji wakisiwa, wasomaji walengwa na wasomaji bora zaidi. Wasomaji wakisiwa walikubaliana na wosia wa *Mwana Kupona*. Ufasiri wao ulichukua mkondo sawa na maoni ya mtunzi. Ilibainika kuwa kaunti ya Lamu ilikuwa na asilimia kubwa (61%) ya wasomaji wakisiwa kuliko wasomaji wakisiwa kutoka kaunti ya Nairobi ambao walikuwa asilimia kumi na tano (15%) ya jumla ya wasomaji waliosailiwa. Tofauti hii ilitokana na kauli kuwa, aghalabu wasomaji wakisiwa hutoka katika mazingira sawa na mtunzi. Kwa hivyo asilimia kubwa ya wasomaji wakisiwa ilitoka kaunti ya Lamu kwa kuwa ndiyo mazingira chipuzi ya *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Vilevile, utafiti uligundua kuwa asilimia kubwa (37.50%) ya jumla ya wasailiwa walikuwa wasomaji wakisiwa. Aidha kwa kuzingatia jinsia ya jumla ya wasomaji wakisiwa kutoka kaunti ya Lamu na Nairobi ilibainika kwamba wasomaji wakisiwa

wanaume katika kaunti zote mbili walikuwa asilimia kubwa (75%) tofauti na wasomaji wakisiwa wanawake ambao walikuwa asilimia ishirini (20%). Utafiti ulibainisha kuwa utofauti huu ulitokana na mabadiliko ya mazingira ambapo wanaume waliunga wosia mkono ilhali wanawake wa sasa walionelea kwamba mambo yamebadilika ukilinganisha na zama za Mwana Kupona. Hii inatokana na moja ya nadharia iliyoongoza utafiti huu kuwa suala la muktadha na utamaduni wa kijamii liangaliwe upya.

Utafiti huu pia ulibainisha wasomaji lengwa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Wasomaji hawa walikuwa vijana wa kike ambao Mwana Kupona alilenga. Asilimia thelathini (30%) ya wasailiwa kutoka Lamu na Nairobi kwa ujumla walikuwa wasomaji Lengwa. Wasomaji hawa walichukulia kuwa *Utenzi wa Mwana Kupona* hauna nafasi katika jamii ya sasa. Walichukulia wosia wa Mwana Kupona kuwa unamtweza mwanamume na kumshusha mwanamke. Katika hali hii wanaonelea kuwa utenzi huu unaendeleza ubabadume na kuwanyima wanawake haki zao za usawa.

Vilevile, utafiti ulibainisha wasomaji bora zaidi wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Katika kaunti ya Lamu, wasomaji bora zaidi walikuwa asilimia kumi (10%) pekee tofauti na kaunti ya Nairobi ambayo ilikuwa na asilimia hamsini na tano (55%). Tofauti hii ilitokana na hali kuwa wasomaji bora zaidi huwa wa kiwango cha juu na huangalia mambo kwa undani kutokana na usomi wao. Nairobi ilikuwa na asilimia kubwa kwa kuwa wasomaji wengi wa Nairobi waliusoma utenzi huu kwa nia ya kufanya mtihani au kuuhakiki. Katika hali hii waliufasiri kwa kuunga mkono na wakati huo huo kupinga baadhi ya vipengele.

## 5.3 Changamoto

Wasailiwa wengi hasa kutoka kaunti ya Lamu mwanzoni walisusia kuhojiwa wakishuku kuwa huenda wanapelelezwa kutokana na kukithiri kwa magaidi wa Al-shaabab na kutokuwepo kwa usalama katika kaunti hiyo. Hata hivyo, mtafiti msaidizi na mkuu wa taarafa ambaye alikuwa mwenyeji aliwashawishi na kuwafahamisha kuhusu lengo la utafiti huu na umuhimu wake.

Kwa kuwa utafiti uliazimia kuchunguza ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona*, ilibidi kutambua ombwe na ufasiri litokanalo na msingi kuwa hata fasiri rasmi kuhusu matini na kila msomaji ana haki ya kufasiri apendavyo kulingana na uelewa wake wa kibinafsi. Changamoto hii tuliikabili kwa kuhusisha kipengele cha nadharia ya Mwitikio wa Msomaji kuwa kuna wasomaji wa aina mbalimbali. Wasomaji hawa ni wakisiwa, lengwa na bora zaidi. Vigezo hivi ndivyo vilitumika kama nyenzo ya kukadiria na kutathminia usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia suala la usomaji na ufasiri sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Utafiti ulionyesha jinsi aina mbalimbali ya wasomaji wanafasiri *Utenzi wa Mwana Kupona*. Pamoja na hayo uliangalia jinsi mazingira yanaathiri usomaji na ufasiri wa utenzi huu. Mbali na kuangalia haya yote, kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha njia za usomaji na ufasiri wa kazi mbalimbali za fasihi.

Kutokana na ugunduzi kuwa asilimia kubwa ya wasomaji lengwa ambao ndio walilengwa na Mwana Kupona hawakubaliani na wosia wa *Mwana Kupona*. Ni vyema

utafiti zaidi ufanywe ili kubainisha ikiwa kuna watunzi wa sasa ambao utunzi wao unaenda sambamba na maoni ya wasomaji lengwa wa sasa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Vilevile, utafiti zaidi ufanywe kuhusu mwitikio wa wasomaji kuhusu mashairi ya kisasa kuhusu mke na jinsi wasomaji wakisiwa wanatofautiana na wasomaji lengwa katika usomaji na ufasiri wa mashairi haya.

Pia, ni vyema utafiti zaidi kufanywa kubainisha ikiwa wale wanawake ambao wamezingatia maadili ya Mwana Kupona wamefaulu katika ndoa zao. Aidha utafiti wa aina hii utabainisha ikiwa kuna nguvu zozote ndani ya Utenzi huu ambazo zinamkuza na kumfanya mwanamke amtawale mume wake.

Utafiti zaidi ufanywe kuhusu wosia wa Umama bint Harith kwa bintiye Ummu Iyas ili kulinganisha na kulinganua wosia huu na ule wa Mwana Kupona.

## Marejeleo


Abdalla, A. [1978] "*Wajibu wa Mshairi wa Kiswahili Katika Jamii Yake*," Katika Zinduko, Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Abdulaziz, M. (1979) *Muyaka: 19th Century Popular Swahili Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureu.

Ahmed, L. (1992) *Women and Gender in Islam: Historical Roots of Modern State*. London: Yale University Press.

Al- Farsy, A. (1969) *Kurani Takatifu*. Nairobi: The Islamic Foundation.

Ali, A. (1986) *The Spirit of Islam*. Lahore: Sajid Book Deport.

Allen, J. (1971) *Tendi: Six Examples of a Swahili Verse Form with translation and Notes*. Heinemann: Nairobi.

Allen, J. (1978) *Siyu in the 18th and Early 19th Centuries. A Chapter in the Interlectual History of East Africa.* Hak Annual Conference Papers, History Department, University of Nairobi.

Bell, M. (1985) *Arts of Deception: Hawthone Romance and Scarlet Letter*. Colarcurcio

Bennet, A. (1995).*Readers and Reading***.**London & New York.Longman.

Biersteker, A. (1991) *Language Poetry and Power. A reconsideration of Utendi wa Mwana Kupona: Faces of Islam in Africa Literature.* Portsmouth: Heinemann.

Butler, M. (1987) *Repossesing the Past: The Case for an Open Literary History*. Cambridge: Cambridge University Press.

Butter, R. (1987) *Task- Involving and Ego-Involving Properties of Evaluation*. Journal of Education and Psychology, 79, 474-482.

Cahill, M. (1996) *Reader Response Criticism and the Allegonizing Reader: Theological Studies,* Vol. 57, No. 1, pp. 89-97.

Chacha, N. (1987) *'The Meaning and Interpretation of Swahili Poetry'*.Ph.D Thesis. Yale University (Haijachapishwa)

Chittick, N. (1967) *The Swahili Coast*. London: George Allen & Unwin Ltd.

Davis, R. na Schleifer, R. (1986) *Contemporary Criticism: Literary & Cultural Studies*. London: Longman.

Durkheim, E. (1897) *Suicide*. Paris: Alcan.

El- Maawy, A.(2011) *Jawabu la Mwana Kupona: Mausio ya Mke wa Kisasa na Wasiya ya Mwana Kupona*. Dar es Salaam: Taasisi ya taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Farouk, T. (1969) *Utangulizi wa Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Farouk, T. (2006) *Why Does Swahili Write? Euphoria, Pain and Popular Aspiration in Swahili Literature*. KATIKA; Research Africa Literature, Vol. 8, No. 2, Pg. 236-237.

Fischer, E. (1959) *The Necesity of Art*. London: Penguin Books.

Fish, S. (1980) *Is Their a Text in This Class? The Authority of Interpretive Communities*. Cambridge: Havard University Press.

Foster, M. (2003) *Reader Response Theory*. Cambridge: Havard University Press.

Foucault, M. (1972) *The Archeology of Knowledge and the Discourse of Language*. New York: Routledge Publishers.

Foucault, M. (1977) *Politics, Philosophy Culture: Interviews and Other Writings*. London: Routledge.

Gauhar, S. (Mhariri) (1977) *The Challenge of Islam.* Islamic Council of Europe.

Gakuo, J. (1996) "*Fani katika Utenzi wa Vita vya Uhuru*." Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kiku Cha Moi: (Haijachapishwa)

Gakuo, J. (2014) "*Changamoto za Uchanganuzi na Ufasiri wa Ushairi katika Shule za Upili Nchini Kenya."*Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi: (Haijachapishwa)

Greenblatt, S. (1980) *Renaissance Self Fashioning. Chicago*: University of Chicago Press.

Gibbe, A. (1978) *'Fasihi na Jamii, Baadhi ya Washairi wa Kiswahili -1960 -1977'* Katika Jarida la TUKI - KISWAHIL1.

Gibbe, A. (1990) *'Ufumbaji na Ufumbuaji wa Mashairi'* Jarida la Kiswahili. Dar es Salaam: Education Service Centre Ltd.

Gibbe , A. na Mvungi, M. (1987) *Fasihi Simulizi ya Sekondari na vyuo.* Dar es Salaam: Standard Publishing Company.

Hirsch, E. (1987) *Contexts for Criticism*. Toronto: Mayfield Publishing Company Mountain View, California London.

Holland, (1968) *The Dynamics of Literary Response*. New York: Oxford.

Hoogvelt, M. (1976) *The Sociology of Developing Societies*. London: Macmillan.

Howthon, J. (1987) *Unlocking the Text: Fundermental Issues in Literary Theory.* London: Edward Anold.

Inyani, K. (1934) *Sexist Overtones in Kiswahili Female Metaphors: A Critical Analysis*. Makala ya OSSREA.

Iser, W. (1974) *The Implied Reader: Patterns of Communication in Prose Fiction From Bunyan to Becket.* Baltimore: John Hopkins Universi Press.

Iser, W. (1978) *The Act of Reading: A theory of Aesthetic Response.* London: John Hopkins University Press.

Joinet, B. (1997) *Step by Step Towards Democracy*. Nairobi: Paulines Publication.

Karuga, M. (2012) *"Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule ya Msingi Nchini Kenya."* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi: (Haijachapishwa)

Kezilahabi, E. (1974) *Kichomi.* Nairobi: H.E.B.

Kimaru, H. (2010) "*Ugumu wa Ufasiri wa Mashairi*." Taifa Leo, Jumanne Agosti 2010, Nation Media Group, Nation Centre, Nairobi.

King' ei, K. na Kemoli, A. (2001) *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Kirkman, J. (1964) *Man and the Monuments on the East African Coast*. London: Lutterworth Press.

Lemu, A. (1978) *Women in Islam*. Derbyshire: Islamic Faoundation.

Magayu, M. (1977) *The East African Literature and the East African Writer*. Journal of East African Literature and Creative Arts.

Masinde, E. (1992*) 'Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo'*. Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Masinde, E. (2003) *'Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui'*. Tasnifu ya Ph.D. Nairobi, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mbatiah, M. (2001*) Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Fotoform Ltd.

McGann, J. (1985*) Historical Studies and Literary Criticism.* Madison: University of

Mbaabu, I. (1985) *Utamaduni wa Waswahili. MWAMKO*. Toleo la 5 Jarida La Chama Cha Kiswahili, Chuo Kikuu, Nairobi.Winsconism.

Momanyi, C. (1991) "*Matumizi ya Taswira kama Kielezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al- Inkishaf*i" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyata, Nairobi: (Haijachapishwa)

Momanyi, C. (1998) "*Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili."* Tasnifu ya Ph.d. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Mpesha, N. (1996) "*Childrens Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of Its Grown and Development*." Tasnifu ya Ph.d. Chuo Kikuu cha Kenyatta; (Haijachapishwa)

Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East Africa Education Publishers.

Mugenda, A. (2008) *Social Science Research*. Nairobi: Kijabe Printing Press.

Mugomba, A. na Nyagah, M. (1980) Independence Without Freedom. Oxford: Clio Press.

Mulokozi, M. (1975) *'Revolution and Reaction in Swahili Poetry'*katika KISWAHILI. Juzuu 45/2.Chuo Kikuu cha Dar esSalaam.

Mulokozi, M. (1982) *Protest and Resistance in Swahili Poetry: 1600-1885.* KISWAHILI, JUZUU 49/1, Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. (1999) *Tenzi Tatu za Kale*. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mulokozi, M. na Sengo, T. (1995) *History of Kiswahili Poetry A.D. 1000-2000, TUKI.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Murfin, R. (1991) *Case Studies in Contemporary Criticism*. New York: St. Martins Press.

Ndungo, C. (1985) *'Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria Katika Fasihi ya Kiswahili.'* Tasnifu ya M.A. Nairobi.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Newton, K. (1990) *Interpreting the Text: A Critical Introduction to the Theory of Practice of Literary Interpretation*. London: Harvester.

Ngugi, T. (1972) *Home Coming*. Nairobi: Heinemann.

Ngugi, T. (1981) *Writers in Politics*. Nairobi: Heinemann

Njogu, K. na Chiremah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyenyembe, J. (1997) *Jinsia: Upeo wa Wanaume na Wanawake*. Nairobi: Paulines Publication.

O'connell, H. (1997) *Women and the Family*. London; Zed Books.

Odaga, A. (1985) *Literature for Children and Young People*. Nairobi. KLB.

Rice, P. et.al.(1983) *Case Studies in Contemporary Criticism*. New York: St. Martins Press

Ricoeur, P. (1976) *Interpretation Theory: Discourse and the Surplus of Meaning*. Texas: Christian University Press.

Robert, S. (1967) *Insha na Mashairi*. London: Nelson.

Sanchez, V. (1973) *Art and Society*. London: Monthly Review Press.

Senkoro, F. (1988) *Shairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: University Press.

Sharrif, N. (1988) *Tungo Zetu: Msingi wa Mashairi na Tungo Nyinginezo*. New Jersey: Red Sea Press.

Sheikh, A. na Nabhany, A. (1972) *Utendi wa Mwana Kupona: Utendi wa Ngamia na Paa*. Nairobi: Heinemann.

Simiyu, B. (2016) *Mwitikio wa Msomaji katika Riwaya ya Siku ya Siku ya Watenzi Wote.* KATIKA. International Journal of Africa Literature and Cultural Studies. Vol. 1, pp. 11-17.

Swaleh, A. (1992) *"Maudhui Katika Utenzi wa Mwanakupona"*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi:(Haijachapishwa)

Strobel, M. (1979) *Muslim Women in Mombasa: 1890-1975*. London: Yale University Press.

Syambo, B. na Mazrui A. (1992) *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Publishers.

Tompkins, J. (1980). *Reader – Response Criticism*. Baltimore and London: John Hopkins.

Veeser, H. (1989) *The new Historicism*. New York: Routledge.

Wafula, R. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002) *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Forcus Publication

Ltd.

Wellek, R. na Warren, A. (1949) *Theory of Literature*. Harmondsworth: Penguin Books Ltd.

Werner, A. (1934) *The advice of Mwana Kupona Upon the Wifely.* Hampshire: The Azani Press.

Weaner, A. (1915) *A Swahili History of Pate*. Journal of the Royal African Society Vol. 14, No. 54, pp. 154-161.

## KIAMBATISHO A:

**Mwongozo wa Maswali Kwa Wasomaji Mbalimbali Kutoka Kaunti ya Lamu na Nairobi wa Utenzi wa Mwana Kupona**

1. Ni nini kilichokuchochea kuusoma Utenzi huu?
2. Kwa maoni yako, ni nini kilichomchochea Mwana Kupona kutunga utenzi huu?
3. Ni yapi maoni yako kuhusu wajibu wa mke kwa mumewe namna inavyojitokeza katika *Utenzi wa Mwana Kupona*?
4. Ni yapi maoni yako kuhusu wosia wa Mwana Kupona kuhusu mwenendo wa mwanamke aliyeolewa?
5. Ni yapi maoni yako kuhusu wosia wa Mwana Kupona kuhusu namna mwanamke aliyeolewa anafaa kuishi katika jamii?
6. Utenzi huu una umuhimu upi kwa jamii ya sasa?
7. Toa maoni mengine yoyote ambayo yanatokana na usomaji wako wa *Utenzi wa Mwana kupona.*

**KIAMBATISHO B**

**Utenzi wa Mwana Kupona ( Nabhany, A. 1972)**

Negema wangu binti,
mchachefu wasanati,
upulike wasiyati,
saa ukazingatiya.

Maradhi yamenishika,
hata yametimu mwaka,
siyapata kutamka,
neno lema kukwambiya.

Ndoo mbe ujilisi,
na wino na qaratasi,
moyoni nina hadithi,
nimependa kukwambiya.

kwisakwe kutaqarabu,
Bismillahi kutubu,
umtaye na Habibu,
na sahabaze pamoya.

Ukisa kulitangaza,
Ina la Mola Muweza,
basi tuombe majaza,
Mungu tatuwafikiya.

Mwanadamu si kitu,
na ulimwengu si wetu,

walau hakuna mtu,
ambaye atasaliya.

Mwanangu twaa waadhi,
pamoya na yangu radhi,
mungu atakuhifadhi,
akuepue na baa.

Twaa nikupe hirizi,
uifungeto kwa uzi,
uipe na taazizi,
upate kuyangaliya.

Nikutungie kidani,
cha lulu na marijani,
nikuvike mke shani,
shingoni kikizagaa.

Penda nikupe kifungo,
kizuri kisicho ongo,
uvae katika shingo,
utaona manufaa.

Yangu utakaposhika,
mwanangu hutosumbuka,
duniani utavuka,
na Akhira utakiya.

La kwanda kamata dini,
faradhi usiikhini,

na sunna ikimkini,
na wajibu kuutiya.

Pili kuwa na adabu,
na ulimi wa thawabu,
uwe kitu mahabubu,
kula utakapongiya.

La tatu uwe sadiqi,
ushikalo ulithiqi,
mtu asoshika haqi,
sandamane naye ndiya.

Tena mwanangu idhili,
mbee za maqabaili,
uwaonapo mahali,
angusa kuwenukiya.

Wangiapo wenukie,
na moyo ufurahie,
kisa uwapeke mbee,
watokapo kwenda ndiya.

Ifanye mteshiteshi,
kwa maneno yaso ghashi,
wala sifanye ubishi,
watu wakayatukiya.

Nena nao kwa mzaha,
yaweteyao furaha,

yawapo ya ikraha,
kheri kuinyamaliya.

Wala situkue dhana,
kwa mambo usoyaona,
na kwamba na kunong'ona,
tahadhari nakwambiya.

Sitangane na watumwa,
illa mwinda wa khuduma,
watakuvutia tama,
la-buda nimekwambiya.

Sandamane na wainga,
wasoyuwa kuitunga,
ziumbe wasiyo tanga,
wata kuwaqurubiya.

Mama pulika maneno,
kiumbe ni radhi tano,
ndipo apate usono,
wa Akhira na duniya.

Nda Mungu na Mtumewe,
baba na mama wayuwe,
na ya tano nda mumewe,
mno imekaririwa.

Naawe radha mumeo,
siku zote mukaao,

siku mukhitariwao,
awe radhi mekuwiya.

Na ufapo wewe mbee,
radhi yake izengee,
wende uitukuzie,
ndipo upatapo ndiya.

Siku ufufuliwao,
nadhari nda mumeo,
taulizwa atakao,
ndilo takalotendewa.

Kipenda wende Peponi,
utapekwa dalihini,
kinena wende Motoni,
huna budi utatiwa.

Keti nae kwa adabu,
usimtie ghadhabu,
akinena simjibu,
itahidi kunyamaa.

Enda nae kwa imani,
Atakalo simkhini,
we nae sikindaneni,
mkindani huumiya.

Kitoka agana naye,

kingia mkongowee,
kisa umtandikie,
mahala pa kupumuwa.

Kilala si’ ikukuse,
mwegeme umpapase,
na upepo nasikose,
mtu wa kumpepeya.

Kivukia simondowe,
wala sinene kwa yowe,
keti papo siinuwe,
chamka kakuzengeya.

Chamka si’ imuhuli,
mwandikie ma’ akuli,
na kumtunda muili,
kumsinga na kumwowa.

Mnyowe umpalize,
sharafa umtengeze,
na udi mfukize,
bukurata wa ashiya.

Mwana Kupona (35)
Mtunde kama kijana,
Asiyeyuwa kunena,
Kitu changalie sana,
Kitokacho na kungiya.

Mpumbaze apumbae,
amrie sikatae,
maovu kieta yeye,
Mungu atakuteteya.

Mwanagu siwe mkoo,
tenda kama uonao,
kupea na kosha choo,
sidharau mara moya.

Na koa na kuisinga,
na nyee zako kufunga,
na yasimini kutunga,
na firashani kutiya.

Nawe ipambe libasi,
ukae kama harusi,
maguu tia kugesi,
na mikononi makowa.

Na kidani na kifungo,
sitoe katika shingo,
muili siwate mwengo,
kwa marashi na daliya.

Pete sikose zandani,
hina sikome nyaoni,
wanda siwate matoni,
na nshini kuitiya.

Nyumba yako inadhifu,
mumeo umsharifu,
wakutanapo sufufu,
msifu ukimtaya.

Muyuwe alipendalo,
nawe lifuate lilo,
yambo limtukialo,
siwe mwenye kumweteya.

Utukiwapo kutoka,
sharuti ruhusa taka,
uonapo meudhika,
rudi na kuiketiya.

Fuwata yake idhini,
awe radhi kwa yaki,
wala sikae ndiani,
saa ya 'ne ikasiya.

Wala sinene ndiani,
sifunue shiraani,
mato angalia tini,
na uso utie haya.

Rejea upesi kwako,
ukae na mume wako,
utengeneze matandiko,

mupate kuilalia.

Mume wako mtukuze,
sifa zake zieneze,
wala simsharutize,
asichoweza kutoa.

Akupacho mpokee,
na moyo ufurahie,
asolitenda kwa yeye,
huna haja kumwambia.

Uonapo uso wake,
funua meno uteke,
akwambialo lishike,
illa kuasi Jalia.

Mama sinue ulimi,
nioleza wako umi,
nalioa nyaka kumi,
tusitete siku moya.

Alinioa babako,
kwa furaha na ziteko,
tusondoleane mbeko,
siku zote twalokaa.

Siku moya tusitete,
ovu langu asipate,

na lake nisilikute,
hata akakhitariwa.

Yalipokuya faradhi,
kanikariria radhi,
nkashukuru nkafawidhi,
moyo wangu nikatoshea.

Tangu hapo hata yeo,
siyanyamaa kilio,
nikumbukapo pumbao,
na wingi wa mazoea.

Watu wakipulikana,
milele hukumbukana,
ila wenye kushindana,
daima huiyutia.

Mausiyo ya mvuli,
Allah Allah yaamini,
na nduguzo na ahali,
wapende nakuusiya.

Uwaonapo sahibu,
ambao wakusanibu,
wakikwambia karibu,
angusa kukurubia.

Na wachandika chakula,

uchambiwa nawe nla,
wala siweke muhula,
nyuma nyuma kurejeya.

Wala sifanye kiburi,
nla hata ushakiri,
usiyakuta siqiri,
ukambwa na kondolewa.

Watu wote waumini,
kwako na wawe wendani,
sipende masalatini,
washinde ukiwapuwa.

Sipende wenye jamali,
na utukufu wa mali,
fuqara ukawadhili,
Cheo ukamvundiya.

Akupendae mpende,
akuizao mwenende,
kwa zema mvundevunde,
la’ ala akaridhiya.

Na ayapo muhitaji,
mama kwako simuhuji,
kwa uwezalo mbuji,
angusa kumtendeya.

Mama haya yasikize,
tafadhali sinipuze,
utaona nafuuze,
za Akhira na duniya.

Tamati maneno yangu,
kukuusia mwanangu,
sasa tumuombe Mungu,
anipokelee dua.

Kwani yote tunenao,
mwanaadamu ni puo,
mola ndiye awezao,
kupoteza na kongowa.

Nakuambawe Manani,
unitilie auni,
ninenayo ulimini,
na yote nisoyatowa.

Yote nimezoyanena,
Rabi taqabali minna,
na yasaliyeo tena,
Rabi Mola nitendeya.

Niwekea wangu wana,
na umbu langu mnuna,
yakue yao maina,
yenee majimbo piya.

Rabi waweke nduzangu,
na wana wao na wangu,
wenee na ulimwengu,
kwa jamali na sitawa.

Na jamii Islamu,
Mola wangu warahamu,
matakwa yao yatimu,
nyoyo zikifurahiya.

Ya Allahu wangu Bwana,
nimekupa ni amana,
watunde Mola Rabana,
siwate kuwa’ ngaliya.

Nimekupa duniani,
watunde uwahizini,
unipe kesho Peponi,
mbee za Tumwa Nabiya.

Wangalie kwa huruma,
uwongoze ndia njema,
wapulie na tama,
za Akhira na duniya.

Kwako kuomba sikomi,
wala sifungi ulimi,
ya mufarijal’hami,

nikomesheze udhiya.

Nisimeme muhitaji,
mjao nakutaraji,
ajili bi'faraji,
ya afuwa na afiya.

Nondolea ndwee mbovu,
yaloningia kwa nguvu,
dhambi zangu na maovu,
ya Rabi nighufiriya.

kwetu yangawa mazito,
kwako wewe ni matoto,
nepulia uvukuto,
unepuke mara moya.

Nakuombawe Latifu,
unondolee mikhafu,
kwa Yaumu-li-Arafu,
na Idi ya Udhuniya.

Kwa siku hizi tukufu,
za kuhiji na kutufu,
niafu Rabi niafu,
unishushize afuwa.

Ya Allahu Ya Allahu,
ya Rabahu Ya Rabahu,

ya Ghayatu Raghbatahu,
nitika hukwamkuwa.

Nakuombawe Rabbana,
Bi asmaika ‘lhusuna,
tisia wa tisiina,
mia kupungua moya.

Nipulishie walimu,
wakinena yafahamu,
dua hini Isilamu,
akiomba hujibiwa.

Nami mjao dhaifu,
mwenye nyingi takilifu,
nakuomba takhafifu,
Rabi nitakhafifya.

Nakuomba taisiri,
mambo nisiyakadiri,
unegeshe kulla kheri,
shari ukinepuliya.

Ya Rabi nitimiliza,
mambo nisiyoyaweza,
wala moyoni kuwaza,
kwamba yatasikiliya.

Rabi unifurahishe,
Mambo mema unigeshe,

Maovu uyagurishe,
Tusikutane pamoya.

Uniweke duniani,
miongo ya wahusuni,
nifapo nende Peponi,
makao ya hifadhiya.

Ntungile utungo hunu,
kwa zakumu na zitunu,
kwa kadha yako Dayanu,
na hukumuzo Jaliya.

Ntungile nilisaqimu,
moyo usi na fahamu,
usomeni Islamu,
mukiongozana ndiya.

Na sababu ya kutunga,
ni shairi si malenga,
nina kijana muinga,
napenda kumuusiya.

K'apenda kumnabihi,
la'ala katanabahi,
kamfuata ilahi,
pamwe na wake rijaa.

Somani nyute huramu,

maana muyafamu,
musitukue laumu,
mbee za Mola Jaliya.

Somani mite ya nganu,
mutii waume wenu,
musipatwe na zitunu,
za Akhira na duniya.

Mwenye kutwii mvuli,
ndake jaha na jamali,
kulla endapo mahali,
hutangaa yake ndia.

Mwenye kutunga nudhumu,
ni gharibu mwenye hamu,
na ubora wa ithimu
Rabi tamghufiriya.

Ina lake mufahamu,
ni mtaraji Karimu,
Mwana Kupona Mshamu,
Pate alikozaliwa.

Tarakhiye kwa yakini,
alifu wa miateni,
khamsa wa Sabini,
hizi zote Hijiriya.

Na baitize idadi,
Ni miati maadudi,
Na mbili za mazidadi,
Ndiyo zimezozidiya.

Mola tatusahiliya,
kwa baraka za Nabiya,
na maswahaba pamoya,
dini walioteteya.

Nahimidi kisaliya,
kwa Tume wetu Nabiya,
Ali zake na dhuriya,
itwenee sute piya.

**KIAMBATISHO C**

**Orodha ya Baadhi ya Waliohojiwa**

1. **M1. Mahmoud Abdul Kadir**
   Shekhe katika Muskiti wa Pwani, Lamu mjini. Pia ni mwanamapokeo. Alikuwa msomaji wa kiwango bora zaidi. Aliufaa utafiti huu hasa katika kueleza historia ya *Utenzi wa Mwana Kupona*.
2. **M2. Abdulwahid Mohammed**
   Mkaazi wa eneo la Shela Lamu. Ni naibu wa mwalimu mkuu shule ya upili ya wasichana ya Tawheed kule Malindi. Pia ni ustadhi wa madrasa kule Lamu na Malindi. Alikuwa msomaji wa kukisiwa. Ufahamu wake katika maswala ya kidini na nafasi ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika kuendeleza mafunzo ya dini ya Kiisilamu hasa namna ya mke anavyostahili kuishi na mumewe nA jamii kwa jumla
3. **M3**. **Dkt Edwin Masinde**
   Mhadhiri katika chuo Kikuu cha Kenyatta, pia ni mtaalamu katikaa ushairi wa Kiswahili. Aliangazia katika ufafanuzi wa mazingira chipuzi na athari ya mazingira ya sasa katika usomaji na ufasiri wa *Utenzi wa Mwana Kupona*
4. **M4. Aisha Miraji**
   Mzaliwa wa Pate lakini mkaazi wa eneo la Mkomani kule Lamu. Alikuwa msomaji aliyelengwa mwenye maoni kuwa utenzi huu unawagandamiza wanawake.
5. **M6. Firdaus Nassir**
   Mkaazi wa eneo la Langoni kule Lamu Magharibi. Pia ni Mwanafunzi wa Fasihi ya Kingereza katika Chuo cha Pwani
6. **M6. Aisha Said**
   Mwanafunzi wa Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ni mzaliwa wa Malindi ambaye anaishi mjini Nairobi. Alikuwa msomaji Bora zaidi. Maelezo yake kuhusu maana ya jina la Mwana Kupona iliufaa sana utafiti huu.
7. **M7. Fauzia Shaban**
   Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mt. Kenya na Mzawa wa Lamu. Alikuwa msomaji aliyelengwa
8. **M8. Everlyne Mudhune**
   Muhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, idara ya Kiswahili. Alikuwa msomaji bora zaidi
9. **M9. Damary Werunga**
   Mwanafunzi wa uzamili katika idara ya Historia na masuala ya Kisiasa, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Alikuwa msomaji bora zaidi.

10. **M10. Dkt. Evans Mbuthia Murage**
    Mhadhiri Chuo Kikuu cha Nairobi, idara ya Kiswahili. Alikuwa msomaji bora zaidi

KIAMBATISHO D.

**Picha za Baadhi ya Wahojiwa**



P.1A.Wanawake wa Kiislamu akiwemo mhojiwa M4 katika eneo la Mkunguni baada ya mahojiano.



P. 2B.Ustadhi Abdulwahid Muhammad bin Muhammad ambaye pia ni mwalimu wa somo la dini ya Kiislamu katika shule ya upili ya Tawheed na Madrasa kule Lamu na Malindi. Picha ilichukuliwa nyumbani mwake kule Shela, Lamu.



Shekhe Mahmoud Abdul Kadir katika ofisi yake ndani ya Msikiti wa Pwani, mjini Lamu akinieleza kuhusu wosia wa Umama bint Harith ambao unashabihiana kwa karibu na *Utenzi wa Mwana Kupona*

Wahojiwa wengi hawakupendelea picha zao zichukuliwe.

**KIAMBATISHO E.**


**Ramani za Eneo la Utafiti**





P. 4. Ramani ya Kenya inayoonyesha kaunti za Nairobi na Lamu




P.5. Ramani inayoonyesha Kisiwa cha Lamu na Manda




P.6. Ramani ya Kisiwa cha Pate alikozaliwa Mwana Kupona




Chuo Kikuu cha Kenyatta

P.7. Ramani ya kaunti ya Nairobi